JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA

TAARIFA YA KWANZA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO KUHUSU UCHAMBUZI WA SHERIA NDOGO

Idara ya Kamati za Bunge
Ofisi ya Bunge
S. L. P. 941
DODOMA

Novemba, 2016

YALIYOMO

1.0 UTANGULIZI 1

1.0 MAELEZO YA AWALI 1

1.2 MADARAKA YA KUTUNGA SHERIA 1

1.3 DHANA YA UDHIBITI WA KIBUNGE WA SHERIA NDOGO 2

1.4 MSINGI WA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA KAMATI 6

1.5 NAMNA AMBAVYO KAMATI INATEKELEZA MAJUKUMU YAKE 7

2.0 UCHAMBUZI WA SHERIA NDOGO 12

2.1 SHERIA NDOGO ZILIZOCHAMBULIWA 12

2.2 UCHAMBUZI WA SHERIA NDOGO ZILIZOTUNGWA NA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA (BY – LAWS) 12

2.3 UCHAMBUZI WA KANUNI ZILIZOTUNGWA NA WIZARA NA TAASISI MBALIMBALI *(RULES AND REGULATIONS)* 22

2.4 MAJUKUMU MENGINE 42

3.0 MAONI YA JUMLA 48

3.1 UANDISHI WA SHERIA NDOGO 48

3.2 MCHAKATO WA UTUNGAJI WA SHERIA NDOGO 50

4.0 HITIMISHO 51

4.1 SHUKURANI 51

4.2 HOJA 54

TAARIFA YA KWANZA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO KUHUSU UCHAMBUZI WA SHERIA NDOGO

1.0 UTANGULIZI

1.1 MAELEZO YA AWALI

1.1.1 **Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo, nakushukuru kwa kutoa idhini kwa mamlaka uliyo nayo kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge[1] ili Kamati yangu iweze kuwasilisha **Taarifa ya Kwanza ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo Kuhusu Uchambuzi wa Sheria Ndogo** uliofanywa Kamati. Taarifa hii inajumuisha uchambuzi wa Sheria Ndogo mbalimbali zilizowasilishwa Mezani na Serikali katika Mkutano wa Pili, Mkutano wa Tatu na Mkutano wa Nne wa Bunge la Kumi na Moja.

1.1.2 **Mheshimiwa Spika**, natumaini kuwa Waheshimiwa Wabunge wataitumia Taarifa hii kutoa ushauri zaidi kuhusu Sheria Ndogo zilizochambuliwa na Kamati pamoja na Sheria Ndogo nyingine ambazo zinatumika. Aidha, Kamati inaamini kuwa Serikali itayafanyia kazi mapendekezo yaliyomo katika Taarifa hii na maoni yatakayotolewa na Wabunge.

1.2 MADARAKA YA KUTUNGA SHERIA

1.2.1 **Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Ibara ya 64 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndicho chombo kikuu chenye mamlaka yote ya kutunga Sheria juu ya mambo yote yahusuyo Tanzania bara. Aidha, Ibara ya 97 ya Katiba imeweka utaratibu ambao

[1] Toleo la Januari, 2016

utafuatwa na Bunge katika kutekeleza madaraka yake ya kutunga Sheria.

1.2.2 Hata hivyo, kwa kuzingatia kuwa Bunge halina muda wa kutosha wa kutunga Sheria kuhusu masuala yote ambayo utekelezaji wake unahitaji uwepo wa Sheria, Ibara ya 97 (5) inalipa Bunge mamlaka ya kukasimu madaraka yake ya kutunga Sheria kwa mtu yeyote au idara yoyote ya Serikali. Malengo ya Bunge kukasimu madaraka yake ya kutunga Sheria ni kuvipa vyombo hivyo fursa ya kuweka masharti ambayo ni mahsusi *(specific)* kwa utekelezaji wa masharti ambayo ni ya jumla yaliyowekwa kupitia Sheria mbalimbali *(Principal Acts)* zilizotungwa na Bunge.

1.2.3 **Mheshimiwa Spika**, Sheria zinazotungwa na mamlaka nyingine nje ya Bunge huitwa Sheria Ndogo *(subsidiary legislation/delegated legislation)* na hujumuisha Kanuni mbalimbali *(rules and regulations)* pamoja na Sheria Ndogo za Halmashauri *(By-Laws)*.

1.3 DHANA YA UDHIBITI WA KIBUNGE WA SHERIA NDOGO

1.3.1 **Mheshimiwa Spika**, Udhibiti wa Kibunge wa Utungaji wa Sheria Ndogo *(Parliamentary Control Over Subsidiary Legislation)* siyo dhana mpya katika mgawanyo wa madaraka ya dola katika nchi za Jumuiya ya Madola. Udhibiti huu una lengo la kuhakikisha kwamba, Bunge linajiridhisha kikamilifu kwamba madaraka ya kutunga sheria liliyokasimu kwa mamlaka nyingine yanatekelezwa ipasavyo kwa kuzingatia masharti ya Sheria Mama iliyoruhusu utungwaji wa Sheria Ndogo. Mwandishi maarufu wa vitabu vya sheria C. K. Takwani[2] aliandika yafuatayo:-

[2] Takwani C.K, (2008) Lectures on Administrative Law, 4th edition, Lucknow: Eastern Book Company.

"...it is open for the Parliament to confer power upon anyone it likes. If the Parliament delegates its legislative powers to any other authority such as executive, it also has the obligation to see if those powers are properly exercised by the administration..."

Kwa tafsiri isiyo rasmi kwa Kiswahili, tunaweza kusema kuwa:-

"…Bunge limeachwa liweze kutoa sehemu ya madaraka yake ya kutunga sheria kwa yeyote ambaye Bunge litapenda. Bunge likikasimu madaraka yake ya kutunga sheria kwa mamlaka nyingine yoyote kama vile Serikali, litakuwa na wajibu wa kuhakikisha kuwa madaraka hayo yanatekelezwa ipasavyo."

Kwa maoni ya mwandishi huyo, ni wazi kuwa Bunge lisipokuwa na utaratibu wa kudhibiti/kujiridhisha kuhusu utungaji wa Sheria Ndogo, litakuwa halijajipanga kutekeleza wajibu wake wa msingi.

1.3.2 **Mheshimiwa Spika**, dhana ya Udhibiti wa Kibunge wa Sheria Ndogo imeelezwa kwa kiasi cha kutosha kueleweka katika machapisho mbalimbali ya fani ya Sheria na masuala ya Bunge. Kwa mfano, katika insha ya kisheria iliyoandikwa na Bharat Raj, mwandishi huyo aliandika maneno yafuatayo kubainisha umuhimu wa uwepo wa mfumo wa utungaji wa Sheria Ndogo nje ya Bunge na ulazima wa Bunge kusimamia na kudhibiti utungaji wa Sheria Ndogo hizo:-

"Delegated legislation is often criticized as an excuse for the legislators, a shield for the administrators and a provocation for the Constitutional purists. However, the very mechanism of delegated legislation cannot and should not be reduced to an evil because it is at the end of the day a necessity. In the modern world where social, economic, technological, and administrative speed

outstrips the placid traditional legislative processes, delegated legislation is an essential means of survival. Thus, since it is the legislature which delegates power, it is primarily for it to supervise and control the exercise of this power, and ensure against its objectionable, abusive & unwarranted use.[3]*"*

1.3.3 **Mheshimiwa Spika**, kwa tafsiri isiyo rasmi, nukuu hiyo inasema:-

"Sheria Ndogo zinalalamikiwa kutumiwa kama udhuru wa Watunga Sheria, ngao kwa watawala na jambo linalowaudhi wanaufasaha wa Kikatiba. Hata hivyo, utaratibu wenyewe wa Sheria Ndogo hauwezi na haustahili kushushwa kiasi cha kuwa ubaya kwa sababu mwishowe ni jambo la lazima. Katika ulimwengu wa leo, ambapo kasi ya kijamii, kiuchumi, kiteknolojia na kiutawala inazidi mchakato wa kawaida wa utungaji Sheria, Sheria Ndogo ni njia ya lazima kuwepo. Hivyo, kwa kuwa ni Bunge linalokasimu madaraka yake ya kutunga Sheria, kimsingi linapaswa kusimamia na kudhibiti matumizi ya madaraka hayo na kuwa na uhakika kwamba madaraka hayo, hayatumiki isivyofaa, vibaya na wala isivyo kubalika."

1.3.4 **Mheshimiwa Spika**, Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1 *(The Interpretation of Laws Act, Cap 1 R.E. 2002)* imeweka masharti maalum ambayo yanalipa Bunge la Tanzania mamlaka ya udhibiti wa Sheria Ndogo zinazotungwa na Serikali pamoja na vyombo vyake. Udhibiti huo sio wa moja kwa moja kwa sababu Bunge halina mamlaka ya kuingilia mchakato wa kutungwa kwa Sheria Ndogo yoyote mpaka itakapotangazwa katika Gazeti la Serikali na kuwasilishwa Bungeni.

[3] Bharat Raj (2016) Parliamentary Control of Delegated Legislation with Refernce to Consultation of Affected Interest: Hidayatullah National Law University, Chhattisgarh

1.3.5 **Mheshimiwa Spika**, Sheria Mama inapotungwa na Bunge inaweza kuweka masharti kwamba, Sheria Ndogo yoyote inaweza kutungwa kwa madhumuni ya kuwezesha utekelezaji wa Sheria Mama. Kifungu cha 36 cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria[4] kinaweka masharti ya jumla ya kuzingatiwa wakati wa utungaji wa Sheria Ndogo na moja kati ya masharti hayo ni kwamba, Sheria Ndogo haipaswi kuwa kinyume na Sheria Mama.

1.3.6 **Mheshimiwa Spika**, baada ya Sheria Ndogo kutungwa na mamlaka husika na kuchapishwa katika Gazeti la Serikali kwa mujibu wa kifungu cha 37 cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria[5], Sheria Ndogo hiyo inapaswa kuwasilishwa Bungeni ndani ya siku sita (6) za vikao vya Bunge *(six sitting days)* kwa masharti yanayopatikana katika kifungu cha 38 (1).

1.3.7 **Mheshimiwa Spika**, kwa kuona umuhimu wa kufanya Udhibiti wa Utungaji wa Sheria Ndogo, Bunge la Tanzania kama ilivyo kwa Mabunge mengine katika Nchi za Jumuiya ya Madola, limeunda Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo ambayo inatekeleza majukumu hayo kwa niaba ya Bunge. Kwa mujibu wa Kifungu cha 11 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 majukumu ya Kamati hii ni kuchambua Sheria Ndogo zilizotungwa ili kujiridhisha iwapo zimekidhi matakwa na masharti ya Katiba, Sheria Mama na Sheria nyingine za nchi.

1.3.8 **Mheshimiwa Spika**, endapo itabainika kwamba, Sheria Ndogo yoyote iko kinyume na masharti ya Sheria Mama au Sheria nyingine yoyote, Sheria Ndogo hiyo itahesabika kuwa ni batili kwa kiwango ambacho imekiuka Katiba, Sheria Mama au Sheria nyingine yoyote ya nchi *(void to the extent of inconsistency)* kwa

[4] Sura ya 1, Toleo la 2002
[5] *ibid*

mujibu wa Kifungu cha 36 (1) ca Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1.

1.4 MSINGI WA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA KAMATI

1.4.1 **Mheshimiwa Spika**, msingi wa utekelezaji wa majukumu ya Kamati umejengwa katika Dhana ya Udhibiti wa Kibunge wa Sheria Ndogo. Msingi huu unaipa Kamati uwezo wa kufanya uchambuzi wa Sheria Ndogo kwa niaba ya Bunge ambalo ndicho chombo kikuu cha uwakilishi kinachoisimamia Serikali.

1.4.2 **Mheshimiwa Spika**, Sheria Ndogo huweka taratibu, kanuni, masharti na adhabu mbalimbali kwa lengo la kuratibu mwenendo, ustawi wa jamii na ukusanyaji wa mapato. Sheria Ndogo zinagusa moja kwa moja maisha ya kila siku ya mwananchi wa kawaida na shughuli za kiuchumi zinazofanywa na jamii kubwa ya Watanzania.

1.4.3 **Mheshimiwa Spika**, ikumbukwe kuwa Muundo wa Uchumi wa Tanzania *(Structure of Tanzania Economy)* unahusisha shughuli za kilimo, ufugaji, uchimbaji madini, gesi, uvuvi na biashara kama inavyothibitishwa katika Hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. John P. Magufuli aliyoitoa wakati wa Ufunguzi wa Bunge la Kumi na Moja aliposema:-

> *"Mheshimiwa Spika, nchi yetu kwa kiasi kikubwa ni nchi ya kilimo, ufugaji na uvuvi. Hii inatokana na ukweli kwamba, sehemu kubwa ya watu wetu wapatao asilimia sabini na tano (75%) wanaishi vijijini na wanategemea kilimo, ufugaji na uvuvi kwa ajili ya maisha yao."*

1.4.4 **Mheshimiwa Spika**, mwenendo wa shughuli hizo huwekewa taratibu mbalimbali ili kuzistawisha na kuziwezesha kuwa na manaufaa kwa watu kwa kutungiwa Sheria Ndogo. Hata hivyo,

utungaji wa Sheria hizo katika maeneo mengine umekuwa ukilalamikiwa. Mathalani, katika Sekta ya Kilimo, wakulima na wafanyabiashara wa mazao ya kilimo wamekuwa wakilalamika mara kwa mara kwamba Sheria Ndogo nyingi zinaweka tozo na kodi mbalimbali ambazo badala ya kuwapa unafuu, zinawaongezea gharama. Ni dhahiri kabisa, bila kuwepo kwa udhibiti madhubuti wa Kibunge wa Sheria Ndogo ambazo zinagusa jamii na shughuli za kiuchumi za wananchi walio wengi, uwepo wa Bunge kama chombo cha uwakilishi hautakuwa na tija inayokusudiwa.

1.4.5 **Mheshimiwa Spika**, Kamati inaamini kwamba, Bunge la Kumi na Moja lina malengo ya kuhakikisha kuwa, jitihada za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania za kuondosha kero mbalimbali, zinaungwa mkono kwa vitendo. Hivyo basi, Kamati ya Sheria Ndogo kwa niaba ya Bunge, itahakikisha kuwa inazishughulikia Sheria Ndogo ambazo ni kero bila kuathiri nia njema ya uwepo wa Sheria hizo.

1.5 NAMNA AMBAVYO KAMATI INATEKELEZA MAJUKUMU YAKE

1.5.1 **Mheshimiwa Spika**, wajibu wa msingi wa Kamati kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, kama ambavyo imeelezwa awali, ni kufanya uchambuzi wa Sheria Ndogo ili kujiridhisha iwapo zimekidhi matakwa na masharti ya Katiba, Sheria Mama na Sheria nyingine za nchi.

1.5.2 **Mheshimiwa Spika**, Sheria Ndogo hutungwa mara kwa mara kwa ajili ya utekelezaji wa Sheria Mama katika masuala mbalimbali. Baada ya kusainiwa na Mamlaka inayohusika, Sheria Ndogo hutangazwa katika Gazeti la Serikali ambalo huchapishwa kila Ijumaa kwa mwaka mzima. Kwa mujibu wa kifungu cha 4 cha

Sheria ya Tafsiri ya Sheria[6], Sheria Ndogo zinajumuisha yafuatayo:-

a) *Orders* (Amri)
b) *Proclamations* (Matamko)
c) *Rules* (Kanuni)
d) *Rules of Court* (Kanuni za Mahakama)
e) *Regulations* (Kanuni)
f) *Notices* (Taarifa)
g) *By - Laws* (Sheria Ndogo za Halmashauri)
h) *Instruments* (Hati)

1.5.3 **Mheshimiwa Spika**, Sheria Ndogo zilizotungwa ni nyingi na kwa hali yoyote, Kamati haiwezi kuzichambua zote na kwa ukamilifu katika Bunge la Kumi na Moja. Kwa sababu hiyo basi, kwa mamlaka inayopatikana katika Kanuni ya 117 (8) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati imejiwekea utaratibu wa kutekeleza wajibu wake kwa kufanya yafuatayo:-

a) **Kufanya Uchambuzi wa Sheria Ndogo zote zilizowasilishwa katika Mkutano wa Bunge uliotangulia**

Kifungu cha 38 (1) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, kinaweka sharti kwamba, Sheria Ndogo yoyote iliyotungwa na mamlaka nyingine nje ya Bunge ni lazima iwasilishwe Bungeni ndani ya siku sita (6) za vikao *(six sitting days)* baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali. Baada ya Bunge kupokea Sheria Ndogo hiyo, Kamati hufanya uchambuzi wake na baadae kutoa maoni na ushauri wake kuhusu yaliyomo katika Sheria Ndogo husika na hatua ambazo Bunge laweza kuchukua. Hatua hizo kwa mujibu wa Sheria ni pamoja na zifuatazo:-

[6] Toleo la 2002

i) **Kutoa Azimio la kuzuia kutumika kwa Sheria Ndogo husika *(disallowance resolution)* -** Kwa mujibu wa masharti yanayopatikana katika kifungu cha 38 (2) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Bunge linaweza kuchukua hatua hii endapo litajiridhisha kikamilifu kutokana na maoni ya Kamati, kwamba Sheria Ndogo fulani haikidhi masharti na matakwa ya Katiba, Sheria Mama na Sheria nyingine ya nchi.

Hatua hii hutokea endapo Waziri mwenye dhamana na Sheria Ndogo husika atakataa kufanya marekebisho ambayo Kamati imependekeza kabla ya kusomwa kwa Taarifa ya Azimio hilo Bungeni. Aidha, Bunge linaweza kuchukua hatua hii endapo litajiridhisha kuwa Sheria Ndogo fulani haikuwasilishwa Bungeni ndani ya siku sita (6) za vikao *(six sitting days)* baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali kinyume na Kifungu cha 38 (1) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria.

ii) **Kufanya marekebisho au kuibadili Sheria Ndogo yoyote kufuatia Azimio la kuzuia kutumika kupitishwa na Bunge *(amendment and substitution)*** - Kwa mujibu wa kifungu cha cha 38 (4) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Bunge linaweza kupitisha Azimio muda wowote ili kuirekebisha au kuibadili Sheria Ndogo yoyote iliyozuiwa kutumika kwa masharti yanayopatikana katika kifungu cha 38 (2) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria.

b) **Kufanya Uchambuzi wa Sheria Ndogo yoyote ambayo inatumika**

Mheshimiwa Spika, kwa madhumuni ya utekelezaji mpana wa Kifungu cha 11 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati inaweza kufanya uchambuzi wa Sheria Ndogo yoyote kwa kuzingatia vipaumbele inavyojiwekea. Uchambuzi huu huzingatia maoni ya Wajumbe na wadau wengine kuhusiana na utekelezaji wa Sheria Ndogo hizo katika Sekta mbalimbali**.**

c) **Kufanya mikutano ya wazi kwa lengo la kusikiliza maoni ya wadau kuhusu utekelezaji wa Sheria Ndogo zinazowagusa**

Kwa mujibu wa masharti yanayopatikana katika Kanuni ya 117 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati hualika wadau mbalimbali kwa madhumuni ya kusikiliza maoni yao *(public hearing)* kuhusu utekelezaji wa Sheria Ndogo zinazofanyiwa uchambuzi au Sheria Ndogo nyingine yoyote. Mikutano hii ni nyenzo muhimu kwa Kamati wakati wa uchambuzi katika kujiridhisha iwapo Sheria Ndogo zimekidhi matakwa na masharti ya Katiba, Sheria Mama na Sheria nyingine za nchi.

1.5.4 **Mheshimiwa Spika**, ni vyema Bunge lako tukufu likafahamu kwamba, wakati wa Uchambuzi wa Sheria Ndogo, Kamati huzingatia masuala mbalimbali ili kujiridhisha iwapo Sheria Ndogo hizo zimekidhi masharti na matakwa ya Katiba, Sheria Mama na Sheria nyingine za nchi. Mambo ambayo huzingatiwa ni pamoja na yafuatayo:-

a) Iwapo Sheria Ndogo husika inavunja Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

b) Iwapo Sheria Ndogo husika inavuka mipaka au kwenda kinyume na masharti ya Sheria inayotoa mamlaka ya kutunga Sheria Ndogo au Sheria nyingine yoyote;

c) Iwapo Sheria Ndogo husika imezingatia misingi bora ya uandishi wa Sheria *(drafting issues)*;

d) Iwapo Sheria Ndogo husika inakiuka misingi ya haki za binadamu;

e) Iwapo Sheria Ndogo inaendana na uhalisia wa mambo ikiwemo urahisi wa utekelezaji wake, hali ya uchumi wa walengwa na viwango vya adhabu na faini; na

f) Maudhui ya jumla ya Sheria Ndogo husika.

1.5.5 **Mheshimiwa Spika,** baada ya kukamilisha uchambuzi wake, Kamati huibua hoja mbalimbali zinazolenga kupata ufafanuzi katika maeneo ya Sheria Ndogo yenye dosari. Hoja hizo huwasilishwa Serikalini kwa lengo la kupendekeza marekebisho au kufutwa kwa kifungu chochote ambacho kina dosari zilizobainishwa na Kamati. Kila Wizara inayoguswa na hoja zinazoibuliwa na Kamati, huwajibika kutoa majibu kuhusiana na Sheria Ndogo ambayo inaisimamia.

1.5.6 **Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia utekelezaj bora wa masharti ya Ibara ya 59 (3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Kifungu cha 8 cha Sheria ya *The Office of the Attorney General (Discharge of Duties) Act, 2005*, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali hushirikishwa katika mchakato wa uchambuzi unaofanywa na Kamati.

2.0 UCHAMBUZI WA SHERIA NDOGO

2.1 SHERIA NDOGO ZILIZOCHAMBULIWA

2.1.1 **Mheshimiwa Spika**, kama ambavyo imefafanuliwa hapo awali, Kifungu cha 38 (1) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria[7] kikisomwa pamoja na Kanuni ya 37 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 kinaweka masharti ambapo Serikali inawajibika kuwasilisha Bungeni Sheria Ndogo zote ambazo zimetangazwa katika Gazeti la Serikali tangu Kikao cha mwisho cha Mkutano wa Bunge uliotangulia. Hivyo, Kamati imefanya uchambuzi wa Sheria Ndogo mbalimbali zilizowasilishwa katika Mikutano ya Bunge ifuatayo:-

a) Mkutano wa Pili wa Bunge
b) Mkutano wa Tatu wa Bunge
c) Mkutano wa Nne wa Bunge

2.1.2 **Mheshimiwa Spika,** uchambuzi uliofanywa na Kamati unahusisha Sheria Ndogo za Mamlaka za Serikali za Mitaa (By – Laws) pamoja na Kanuni za Wizara na Taasisi mbalimbali (Rules and Regulations). Maelezo ya ufafanuzi kuhusu uchambuzi wa kila Sheria Ndogo uliofanywa na Kamati yanapatikana katika Jedwali la Uchambuzi ambalo limeambatishwa pamoja na Taarifa hii.

2.2 UCHAMBUZI WA SHERIA NDOGO ZILIZOTUNGWA NA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA (BY – LAWS)

2.2.1 **Mheshimiwa Spika,** msingi wa kisheria wa kuwepo kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa ni Ibara ya 145 na 146 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977. Mamlaka za Serikali za Mitaa zimekasimiwa madaraka ya kutunga Sheria Ndogo chini ya Kifungu

[7] Op Cit

cha 153 cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) Sura ya 287, Kifungu cha 89 cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji) Sura ya 288 pamoja na Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura ya 290 kwa malengo yafuatayo:-

a) Kuweka misingi thabiti ya utawala bora katika mipaka ya halmashauri;

b) Kuimarisha ustawi wa jamii, afya na ulinzi wa wakazi wa halmashauri husika; na

c) Kuweka masharti ya utekelezaji bora wa Sheria mbalimbali za nchi.

2.2.2 **Mheshimiwa Spika,** Sheria Ndogo zinazotungwa na Halmashauri zinatarajiwa kukidhi matakwa ya katiba ya nchi, Sheria za Serikali za Mitaa, Sheria ya Tafsiri ya Sheria na Sheria nyingine yoyote ya nchi ili kuhakikisha kwamba kunakuwepo na amani, utii wa Sheria na ustawi bora wa Wananchi wa maeneo husika.[8]

2.2.3 **Mheshimiwa Spika,** katika uchambuzi uliofanywa, Kamati ilibaini kuwa baadhi ya Sheria Ndogo zilizotungwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa (By – Laws) zina dosari zifuatazo:-

a) **<u>Sheria Ndogo kwenda kinyume na Sheria Mama</u>**

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 36 (1) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria kinaweka masharti kwamba, Sheria Ndogo yoyote inapaswa kutokiuka masharti ya Sheria ya Bunge inayotoa mamlaka au Sheria nyingine yoyote.[9] Kamati ilibaini kuwa, baadhi ya Sheria Ndogo za Halmashauri *(By – Laws)* zinakwenda kinyume na masharti hayo.

[8] Kifungu cha 153 cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) Sura ya 287, Toleo la 2002
[9] Sura ya 1 Toleo la 2002

Kwa mfano, katika **Sheria Ndogo za (Ushuru wa Mazao ya Misitu) za Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge ya Mwaka, 2015**[10] ambayo imetungwa chini ya Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa (**Sura ya 290**), Kifungu cha 6 cha Sheria Ndogo hiyo kinaweka adhabu ya faini isiyopungua shilingi laki moja (100,000/=) kutokana na makosa yaliyoainishwa. Kifungu hicho kinasomeka kama ifuatavyo:-

> *"**6.** Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa iwapo;-*
>
> *(a) atavuna na kusafirisha mazao ya misitu bila kibali;*
>
> *(b) atakiuka masharti ya kibali;*
>
> *(c) atachoma au kusababisha moto;*
>
> *(d) atakataa au kukwepa kulipa Ushuru;*
>
> *(e) atamshawishi mtu au kundi la watu wasilipe Ushuru;*
>
> *(f) Kuchungia mifugo kwenye misitu ya Hifadhi.*
>
> *atakuwa ametenda kosa na atashitakiwa mahakamani na akipatikana na hatia atatozwa faini **isiyopungua** shilingi laki moja (100,000/=) au adhabu ya kifungo kisichopungua miezi sita jela au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo na kulipa ushuru huo."*

Mheshimiwa Spika, adhabu ya faini iliyotolewa na kifungu cha Sheria Ndogo hii iko kinyume na masharti yanayopatikana katika Kifungu cha 67 cha Sheria Mama (Sura ya 290) ambacho kinazitaka Halmashauri kuweka adhabu ya faini isiyozidi shilingi elfu hamsini (50,000/=). Aidha, adhabu hii haiwezi

[10] GN No. 578 ya tarehe 18 Desemba, 2015

kutekelezeka kwa mujibu wa masharti yanayopatikana katika Kifungu cha 74 (3) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1 kinachosema:-

> *"**74 (3)** Where in a written law a maximum penalty and a minimum penalty are specified in respect of an offence, the offence is punishable by a penalty not less than that minimum nor greater than that maximum."*

Kwa tafsiri isiyo rasmi ya kifungu hicho cha Sheria, iwapo Sheria yoyote iliyotungwa imeweka ukomo wa chini au ukomo wa juu wa adhabu katika kosa, kosa hilo litaadhibiwa kwa adhabu isiyopungua au kuzidi ukomo uliowekwa.

Kwa kuwa Kifungu hicho hakiweki ukomo wa juu wa adhabu, hakuna kizuizi kwa Mahakama kutoa adhabu ya faini ya shilingi laki tano (500,000/=) kwa sababu shilingi laki tano inazidi shilingi laki moja (100,000/=). Kamati inaamini kuwa, hilo sio lengo lilikusudiwa katika masharti ya Kifungu hicho.

Mheshimiwa Spika, mfano mwingine ni Sheria Ndogo za (Ushuru wa Madini ya Ujenzi na Chumvi) za Halmashauri ya Wilaya ya Babati, 2015 iliyotungwa chini ya Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa (Sura ya 290)[11]. Kifungu cha 6 cha Sheria Ndogo hiyo kinaweka ukomo wa faini ya shilingi laki tatu (300,000/=) kwa makosa mbalimbali yatokanayo na Sheria Ndogo hiyo. Kifungu hicho kinasomeka kama ifuatavyo:-

> ***"6.** Mtu atakayekiuka au kwenda kinyume na Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atalipa faini **isiyozidi shilingi 300,000/=** au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili au adhabu*

[11] GN No. 520 ya tarehe 20 Novemba, 2015

zote mbili yaani faini na kifungo, pamoja na kulipa ushuru anaodaiwa na gharama za usumbufu aliosababisha."

Adhabu ya faini iliyotolewa na kifungu cha Sheria Ndogo hii pia iko kinyume na masharti ya Sheria Mama (Sura ya 290) ambayo inazitaka Halmashauri kuweka adhabu ya faini isiyozidi shilingi elfu hamsini (50,000/=).

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Ofisi ya Rais (TAMISEMI) ifanye marekebisho katika Sheria Ndogo zote za Halmashauri ambazo ziko kinyume na Sheria Mama kwa kuvifuta na kuviandika upya vifungu vyote ambavyo vinaweka adhabu ya faini kubwa kuliko kiwango kilichowekwa na Sheria Mama.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa, baadhi ya Halmashauri hazizingatii kabisa misingi ya utungaji wa Sheria Ndogo kwa kuweka masharti na adhabu ambazo zinakiuka masharti ya Sheria Mama. **Hali hii inatokana na hisia kwamba, Sheria za Serikali za Mitaa zilizotungwa na Bunge zinaweka kiwango kidogo cha adhabu ya faini ukilinganisha na ukubwa wa baadhi ya makosa yanayoweza kutendwa na kushughulikiwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.**

Hata hivyo, hisia hizi kamwe hazipaswi kuhalalisha Halmashauri hizo kutunga Sheria Ndogo zinazoweka adhabu kubwa kinyume na masharti yaliyomo katika Sheria Mama. **Hivyo basi, Kamati inaishauri Ofisi ya Rais (TAMISEMI), kufanya marekebisho ya viwango vya faini na adhabu vilivyopitwa na wakati kwa kuwasilisha Bungeni Muswada**

wa Marekebisho ya Sheria Mama husika, iwapo kuna ulazima wa kufanya hivyo.

b) **Sheria Ndogo kuweka masharti yasiyoendana na uhalisia *(unreasonable provisions)***

Mheshimiwa Spika, moja kati ya sifa za Sheria Ndogo nzuri ni ile ambayo inaweka masharti ambayo yanaendana na uhalisia, masharti yanayotekelezeka, yasiyo kandamizi na ambayo hayana utata. Kifungu cha 157 (1) cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) Sura ya 287 kinasema kwamba, kila Sheria Ndogo itakayotungwa na Halmashauri inatakiwa kuweka viwango vya ada na tozo ambazo zinaendana na uhalisia *(reasonable fees, charges and tariffs)*.

Mheshimiwa Spika, katika Sheria Ndogo za (Afya na Usafi wa Mazingira) za Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro, 2015[12], kifungu cha 8 (1) kinaweka wajibu kwa kila mmiliki wa nyumba kuweka sehemu ya waenda kwa miguu yaani "pavement" mbele ya nyumba au biashara yake kwa kadri atakavyoelekezwa na Halmashauri.

Kifungu cha 3 cha Sheria Ndogo hii kinatoa tafsiri ya maneno mbalimbali na neno "pavement" maana yake ni sakafu imara ya mawe au matofali ya saruji au udongo yaliyochomwa na kujengewa kutoka katika nyumba hadi katika mfereji au barabara, kwa waendao kwa miguu au watazamaji wa vitu madukani.

Mheshimiwa Spika, bila kuathiri maudhui mema ya kuimarisha usafi wa mazingira wa Halmashauri hii, sharti hili la kisheria

[12] GN No. 15 ya tarehe 1 Januari, 2016

haliendani na uhalisia wa mambo kwa kuzingatia kuwa uamuzi wa kujenga "pavement" unabaki kwa mmiliki wa nyumba. Aidha, sharti hili linaweza kutafsiriwa kuwa linaingilia haki za kiuchumi za wananchi wa eneo hilo kwa kutaka kuwabebesha mzigo wa gharama za ujenzi zilizo nje ya uwezo wao.

Kamati inashauri kuwa kifungu hiki kifutwe na ikibidi kiandikwe tena kwa kuweka sharti la uhamasishaji kwa wamiliki wa nyumba kujenga "pavements" na sio kuwalazimisha.

Mheshimiwa Spika, mfano mwingine ni Sheria Ndogo za (Kuhifadhi Barabara) za Halmashauri ya Wilaya ya Babati, 2015[13] ambayo imetungwa chini ya Kifungu cha 153 cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) Sura ya 287. Kifungu cha 11 cha Sheria Ndogo hii kinaweka adhabu ya juu kabisa kwa mujibu wa Sheria (maximum fine) ya kulipa faini ya Shilingi 300,000/= kwa kosa la kutupa takataka ya aina yoyote katika eneo la barabara. Kifungu hiki kinasomeka kama ifuatavyo:-

> *"**11.** Ni marufuku kwa mtu yeyote kutupa **takataka ya aina yoyote** kwenye eneo la barabara. Mtu yeyote atakayekiuka masharti ya kifungu hiki cha Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na atalipa faini ya shilingi 300,000/= au kifungo kisichozidi mwezi mmoja au adhabu zote mbili yaani faini na kifungo."* Msisitizo ni wetu.

Mheshimiwa Spika, Katika Sheria Ndogo hii, hakuna tafsiri ya neno "takataka" na hivyo Kamati ilishindwa kujua takataka hizo zinahusisha nini na ni kwa kiwango gani. Kwa maoni ya Kamati, kiwango cha faini iliyowekwa na Sheria Ndogo hii ni kikubwa ukilinganisha na kosa linalotajwa la kutupa takataka ya aina

[13] GN. No. 521 ya tarehe 20 Novemba, 2015

yoyote kwenye eneo la barabara. Aidha, kifungu hicho hakijatoa nafasi kwa Mahakama kuamua adhabu kwa kuzingatia ukubwa wa kosa kwa kuwa kimeweka adhabu ya juu kabisa (maximum fine).

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba Kifungu cha 43 (2) (b) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1 kinaweka masharti kwamba Sheria Ndogo inaweza kuweka faini ya juu kabisa au ya chini, Kamati inazishauri Halmashauri kuweka masharti yenye urahisi wa kubadilika (flexible) kwa adhabu katika baadhi ya makosa ili Mahakama iweze kutoa adhabu mbalimbali kulingana na ukubwa wa kosa.

c) **Sheria Ndogo kuwa na makosa ya kiuandishi na kiuchapaji**

Mheshimiwa Spika, makosa ya kiuandishi na kiuchapaji katika Sheria Ndogo yoyote yanaweza kusababisha athari hasi kwa watumiaji endapo masharti yatakayoandikwa au kuchapwa yatakuwa si yale yaliyokusudiwa. Aidha, dosari hizo zinaweza kusabisha mkanganyiko wa maana endapo Sheria fulani itahitaji kutafsiriwa na vyombo vya utoaji haki.

Kwa mfano, katika Sheria Ndogo za (Uanzishaji wa Mfuko wa Afya ya Jamii) za Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe, 201514 ilibainika kuwa na makosa mengi ya uchapaji ambayo yanaweza kuharibu maana halisi iliyokusudiwa na kuleta mkanganyiko wa tafsiri. Makosa hayo yalibainika katika vifungu vya 7 (2), 21 (1), 26 (1) na 30 (1) kwa kukosekana kwa silabi mbalimbali. Kwa mfano, kifungu cha 26 (1) kinasomeka kama ifuatavyo:-

[14] GN No. 599 ya tarehe 25 Desemba, 2015

*"**26. (1)** Fedha na vyanzo vya mapato ya kituo cha afya vitakuwa vifuatavyo:-*

(a) ichango ya jamii;

(b) afadhili au michango ya washirika;

(c) uzuku kutoka serikalini;

(d) uzuku kutoka Halmashauari;

(e) hanzo chochote halali."

Aidha, dosari zilizobainika katika baadhi ya Sheria Ndogo, endapo zitabaki kama zilivyo, utekelezaji wa Sheria Ndogo hizo unaweza ukawa na changamoto. Kwa mfano, katika Sheria Ndogo za (Kuhifadhi Barabara) za Halmashauri ya Wilaya ya Babati, 2015[15] kifungu cha 4 kinaweka sharti na kuainisha makosa kwa "mkazi" tu na kutoa mwanya kwa mtu mwingine yeyote ambaye si "mkazi" wa Babati kufanya makosa bila kubanwa na Sheria Ndogo hiyo. Sehemu ya kifungu hicho inasomeka kama ifuatavyo:-

*"**4.-** (1) Ni wajibu wa **kila mkazi** wa eneo la Halmashauri kutunza na kuhifadhi barabara iliyoko katika eneo lake na iwe katika hali endelevu ya matumizi na kwamba hataruhusu kwa njia yoyote ile uharibifu wa barabara."* **Msisitizo ni wetu.**

d) **<u>Sheria Ndogo kukiuka misingi ya haki za binadamu</u>**

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni nchi inayofuata misingi ya haki za binadamu kwa mujibu wa Katiba na Mikataba ya Kimataifa iliyoridhiwa. Bunge la Jamhuri ya Muungano lina wajibu wa kutunga Sheria ambazo zinazingatia misingi hiyo ili kuhakikisha kuwa, haki za binadamu zinalindwa na kuhifadhiwa. Kila mamlaka ambayo imekasimiwa madaraka ya kutunga Sheria

[15] GN No. 521 ya tarehe 20 Novemba, 2015

Ndogo kwa niaba ya Bunge, nayo inawajibika kuhakikisha kuwa inatunga Sheria Ndogo ambazo zinalinda na kuhifadhi haki hizo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwepo kwa misingi ya haki za binadamu kwa mujibu wa Katiba na Sheria za Bunge, Kamati imebaini kuwepo kwa Sheria Ndogo za Halmashauri ambazo zina vifungu ambavyo vinaweza kutafsiriwa kuwa vinakiuka misingi ya haki za binadamu.

Kwa mfano, katika Sheria Ndogo za (Kilimo Kwanza na Usalama wa Chakula) za Halmashauri ya Wilaya ya Geita za Mwaka, 2015[16] kifungu cha 16 (d) cha Sheria Ndogo hiyo kinamlazimisha mfugaji kujiunga na vyama vya wafugaji na wajasiriamali. Kifungu hicho kinasomeka kama ifuatavyo:-

> "***16.*** *Kila Mfugaji..*
> *(d) Atalazimika kujiunga na vyama vya wafugaji wajasiriamali…"*

Mheshimiwa Spika, bila kuathiri dhamira ya kifungu hicho, kitendo cha kumlazimisha mfugaji kujiunga na kikundi chochote ni kinyume na Ibara ya 20 (1) ya Katiba[17] ambayo inampa kila mtu haki na uhuru wa kushirikiana na watu wengine kwa hiyari yake mwenyewe.

Kamati inaishauri Ofisi ya Rais (TAMISEMI) ifanye marekebisho ili kifungu hiki kibainishe masharti ya kuhamasisha wafugaji kujiunga na vyama vya wafugaji na wajasiriamali au kuweka sharti linalompa mfugaji uhuru wa

[16] GN No. 585 ya tarehe 18 Desemba, 2015
[17] Sura ya 2 Toleo la 2002

kujiunga na vyama hivyo kwa kutumia maneno "kila mfugaji anaweza kujiunga".

2.3 UCHAMBUZI WA KANUNI ZILIZOTUNGWA NA WIZARA NA TAASISI MBALIMBALI *(RULES AND REGULATIONS)*

2.3.1 **Mheshimiwa Spika**, Kanuni zinazotungwa na Wizara mbalimbali hutungwa kwa utaalam na mara nyingi uandishi wake unalenga kufafanua kwa kina masharti yanayopatikana katika Sheria Mama iliyotungwa na Bunge. Hata hivyo, katika uchambuzi uliofanywa na Kamati katika Kanuni mbalimbali zilizowasilishwa Bungeni, baadhi zilibainika kuwa na dosari ambazo Kamati imetoa maoni na ushauri kwa lengo la kuboresha maudhui ya Kanuni hizo kama ambavyo inaonekana katika **JEDWALI LA UCHAMBUZI** lililoambatishwa. Kwa madhumuni ya kulitaarifu Bunge kuhusu uchambuzi uliofanyika, baadhi ya Kanuni hizo zinafafanuliwa kama ifuatavyo:-

THE PETROLEUM (RETAIL OPERATIONS IN TOWNSHIPS AND VILLAGES) RULES, 2016 (GN No. 174 ya tarehe 13 Mei, 2016)

2.3.2 **Mheshimiwa Spika,** Kanuni hizi zimetungwa kwa malengo ya kuratibu shughuli zinazohusiana na biashara ya bidhaa za petroli katika miji na vijiji katika Tanzania Bara. Sheria Ndogo hii inatokana na Sheria ya Petroli ya Mwaka 2015 iliyotungwa na Bunge.

2.3.3 Uchambuzi wa Kamati katika Sheria Ndogo hii ulibaini dosari nyingi ambazo zinaweza kusababisha uhalali wa matumizi ya Sheria Ndogo hiyo kuhojiwa. Kwa mfano, Sheria Ndogo imerejea Kifungu cha 5 (3) cha Sheria ya Petroli kwamba ndicho kinachotoa mamlaka ya kutungwa kwake badala ya

Kifungu cha 259 (1) ambacho ndicho kinampa mamlaka Waziri kutunga Kanuni.

2.3.4 **Mheshimiwa Spika**, Kanuni ya 11 (3) inaweka adhabu ya faini ya shilingi milioni tano (5) kwa kosa la kuendesha shughuli bila kibali *(offence of conducting a regulated activity without a licence)*. Adhabu hiyo iko kinyume na masharti yanayopatikana katika Kifungu cha 131 (4) cha Sheria Mama ambacho kimeweka adhabu ya faini ya kiasi cha fedha kisichopungua shilingi milioni ishirini (20).

2.3.5 **Mheshimiwa Spika**, Kanuni ya 45 na 46 katika Sheria Ndogo hii zinazungumzia utaratibu ambapo mwenye leseni atalipa gharama za *decommission* na *site restoration*. Kifungu cha 197 cha Sheria Mama kimeweka utaratibu tofauti ambapo kutaanzishwa Mfuko Maalum *(Decommisioning Fund)* ambapo wenye leseni watatakiwa kuchangia katika kipindi cha leseni zao ili mwenye leseni atakayehitajika kufanya *decommission* na *site restoration* asiingie gharama kubwa wakati wa kufunga biashara husika.

2.3.6 Katika maelezo yake mbele ya Kamati, Naibu Waziri wa Nishati na Madini Mhe. Dkt. Medard Kalemani (Mb) alisema kuwa, Sheria Ndogo iliyochambuliwa na Kamati ilitungwa kutokana na Sheria ya Petroli ya Mwaka 2008 ambayo ilifutwa. Kifungu cha 260 (2) cha Sheria ya Petroli ya Mwaka 2015 kinaipa uhalali Sheria Ndogo hiyo kuendelea kutumika pamoja na kufutwa kwa Sheria iliyotoa mamlaka awali.

2.3.7 Hata hivyo, masharti yanayopatikana katika Kifungu cha 260 (2) katika Sheria ya Petroli ya Mwaka 2015 yakisomwa pamoja na masharti ya Kifungu cha 33 (1) (b) cha Sheria ya Tafsiri ya

Sheria, Sura ya 1, Sheria Ndogo hii itakuwa na uhalali wa kutumika chini ya Sheria iliyofutwa endapo tu, haitakuwa na masharti yanayokinzana na Sheria mpya inayotumika. Kifungu cha 33 (1) (b) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1 kinasema:-

> *"**33 (1) (b)** Where an Act repeals and re-enacts an Act, with or without modification, any subsidiary legislation made under the repealed Act and in operation immediately before the commencement of the repealing Act shall, so far as it is consistent with the repealing Act, continue in operation and have effect for all purposes as if made under the repealing Act."*

2.3.8 **Mheshimiwa Spika**, kwa sababu hiyo, na kwa kuzingatia dosari zilizobainika Katika Sheria Ndogo iliyochambuliwa, **Kamati inaishauri Wizara ya Nishati na Madini kuifuta mara moja Sheria Ndogo hii ili isiendelee kutumika na badala yake Wizara itunge Kanuni mpya haraka iwezekanavyo ambazo zitaendana na masharti ya Sheria ya Petroli ya mwaka 2015.**

THE PETROLEUM (BULK PROCUREMENT) REGULATIONS, 2015 (GN. No. 508 ya tarehe 6 Novemba, 2015)

2.3.9 **Mheshimwa Spika,** Sheria Ndogo hii imetungwa chini ya vifungu vya 168 na 258 vya Sheria ya *The Petroleum Act No. 21 Of 2015* kwa lengo la kuanzisha Mfumo wa Uagizaji wa Pamoja wa bidhaa za petroli *(Bulk Procurement System)*. Mfumo huu una malengo ya kuhakikisha kuwa bidhaa za petroli zinakuwepo katika soko kwa wakati na kwa kiwango stahiki.

2.3.10 **Mheshimiwa Spika**, Kamati ilibaini kuwepo kwa mambo kadhaa ambayo yanahitaji kufanyiwa kazi kwa ukamilifu ili

kuiboresha Sheria Ndogo hii ili iweze kukidhi matakwa na masharti ya Katiba, Sheria Mama na Sheria nyingine za nchi. Kwa mfano, Kanuni ya 15 (7) ya Sheria Ndogo hii inaweka masharti kwamba, Waziri anaweza kuzuia bidhaa za petroli zinazosafirishwa nje ya nchi *(on transit petroleum products)* ili zitumike ndani ya nchi katika mazingira ya dharura yatakayobainishwa na Waziri *(localization of transit petroleum products under emergency conditions declared by the Minister)*. Kwa maoni ya Kamati, Kanuni hii inampa mamlaka makubwa Waziri na endapo yasipotumika vyema yanaweza kuhatarisha mahusiano ya kibiashara na nchi za jirani.

2.3.11 **Mheshimiwa Spika**, katika maelezo yake mbele ya Kamati, Waziri wa Nishati na Madini Mhe. Prof. Sospeter Muhongo (Mb), alisema kwamba, Sheria ya Petroli imempa dhamana ya kuhakikisha kunakuwa na upatikanaji wa mafuta nchini ili kulinda uchumi na usalama wa nchi. Aidha alisema kuwa, katika Kifungu cha 5 (2) na Kifungu cha 253 (1) cha Sheria Mama, Waziri ana mamlaka ya kuamuru shehena ya mafuta inayokwenda nchi jirani *(transit petroleum products)* iuzwe nchini endapo kutatokea upungufu wa mafuta. Kifungu cha 253 (1) kinasomeka kama ifuatavyo:-

> *"**253**.- (1) Where there is shortfall in domestic gas commodities or petroleum products supplies or delivery, the Minister may direct a licensee to make supplies or deliveries from a licensee's facility to cover for such shortfall of gas commodities or petroleum products and may further direct on whom such gas commodities or petroleum products shall be delivered."*

2.3.12 **Mheshimiwa Spika**, kwa maoni ya Kamati, masharti yanayopatikana katika Sheria Mama yako wazi kuhusu

mazingira ambayo Waziri anaweza kuagiza mafuta yauzwe nchini endapo kutatokea upungufu wa bidhaa za petroli. Mazingira hayo ni pamoja na vita au hali yoyote ambayo inasababisha upungufu wa bidhaa za petroli kwa mujibu wa kifungu cha 253 (2) cha Sheria Mama. Hata hivyo, ukisoma Kanuni ya 15 (7) ya Sheria Ndogo iliyochambuliwa na Kamati, Kanuni inasema:-

> *"15 (7) Under emergency conditions declared by the Minister, the transit petroleum products may be localized."*

2.3.13 **Mheshimiwa Spika**, Kanuni hii inampa Waziri mamlaka ya kuamuru mafuta ambayo yako njiani kwenda nchi za nje *(transit petroleum products)* kutumika nchini katika mazingira ya tahadhari atakayotangaza Waziri *(emergency conditions declared by the Minister)*. **Bila kuathiri masharti ambayo yanapatikana katika Sheria Mama, Kamati inashauri kwamba, Kanuni ya 15 (7) ya Sheria Ndogo hii ifanyiwe marekebisho kufafanua masharti na maana halisi inayopatikana katika kifungu cha 253 cha Sheria Mama ili kuendana na dhamira ya Bunge wakati inatunga Sheria hiyo.**

2.3.14 **Mheshimiwa Spika**, maoni ya Kamati yana malengo ya kuhakikisha kuwa misingi ya uandishi wa Kanuni zinazotungwa na Wizara na Taasisi mbalimbali zinazingatia kikamilifu masharti yanayopatikana katika Kifungu cha 39 (1) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1 ambayo yanaitaka Sheria Ndogo yoyote kuwa na maudhui ambayo yanaendana na Sheria inayota madaraka. Kifungu hicho kinasomeka kama ifuatavyo:-

*"**39.-(1)** Words and expressions used in subsidiary legislation shall have the same respective meaning as in the written law under which the Subsidiary legislation is made."*

2.3.15 **Mheshimiwa Spika**, Kanuni ya 14 (4) ya Sheria Ndogo hii inazitaja bidhaa za petroli ambazo zitakuwa zinaagizwa kwa kutumia Mfumo wa Uagizaji kwa Pamoja *(Bulk Procurement System)*. Bidhaa hizo ni pamoja na mafuta ya taa *(illuminating kerosene)*, mafuta ya magari *(automotive gasoline)*, mafuta mazito ya kuendeshea mitambo *(heavy fuel oil)*, mafuta ya ndege *(jet-A1)* na gesi inayotumika majumbani *(liquefied petroleum gas)*.

2.3.16 **Kamati inashauri kwamba, Wizara ikamilishe haraka maandalizi ya utaratibu utakaowezesha bidhaa zote za mafuta ambazo Kanuni ya 14 (4) ya Sheria Ndogo hiyo inaagiza ziingizwe nchini kwa mfumo wa *Bulk Procurement System*. Hatua hii itawezesha kushuka kwa bei za bidhaa husika.**

THE DRUGS CONTROL AND ENFORCEMENT (GENERAL) REGULATIONS, 2016 (GN No. 173 ya tarehe 10 Mei, 2016)

2.3.17 **Mheshimiwa Spika**, Kanuni hizi zimetungwa chini ya Kifungu cha 67 cha Sheria inayoitwa *The Drugs Control and Enforcement Act, CAP. 95* ambayo imetungwa na Bunge kwa malengo ya kuweka masharti ya kudhibiti madawa ya kulevya, kuanzisha mamlaka ya kuzuia na kudhibiti matumizi ya madawa hayo na usafirishaji wake pamoja na masuala mengine yanayohusiana.

2.3.18 **Mheshimiwa Spika,** Kanuni ya 5 (5) inatoa katazo kwa mmiliki wa mali inayopigwa mnada pamoja na ndugu zake kununua mali iliyotaifishwa na Kamishna kutokana na biashara ya dawa za kulevya. Hata hivyo, Kanuni haijaweka katazo la kuizuia Kampuni ambayo mwenye mali ni mmiliki au mbia, kununua mali iliyotaifishwa kiasi ambacho inaweza kutoa mwanya kwa mali hiyo kurudi kwa mmiliki.

2.3.19 **Kamati inashauri kuwa Kanuni hiyo ifanyiwe marekebisho ili kuzuia mazingira ambayo mali iliyotaifishwa kutokana na biashara ya dawa za kulevya inaweza kurejeshwa kwa mmiliki.**

2.3.20 **Mheshimiwa Spika**, Kanuni ya 14 inaweka masharti yanayoratibu zoezi la kuharibu madawa ya kulevya yaliyokamatwa *(destruction of seized drugs)*. Kanuni ya 14 (1) imewataja watu ambao ni lazima wawepo wakati zoezi hilo linatekelezwa. Watu hao ni wafuatao:-

a) Jaji au hakimu;
b) Mwakilishi wa Kamishna wa Madawa ya Kulevya, Inspekta Jenerali wa Polisi, Mkurugenzi wa Mashtaka, Mkemia Mkuu wa Serikali;
c) Mwakilishi kutoka Baraza la Mazingira la Taifa na Usalama wa Taifa; na
d) Mtu mwingine yeyote ambaye Kamisha wa Madawa ya Kulevya atamteua.

2.3.21 Hata hivyo, Kanuni ya 14 (2) inaweka masharti kwamba, Kamishna wa Madawa ya Kulevya au Afisa Mwidhiniwa anaweza kuamuru madawa ya kulevya yaliyokamatwa yaharibiwe bila kuwashirikisha watu wanaotajwa katika Kanuni ya 14 (1).

2.3.22 **Mheshimiwa Spika**, masharti ya Kanuni hii yanakiuka misingi ya uandishi kwa kuwa yanakinzana kwa sababu Kanuni ya 14 (1) imetumia neno *"shall"* kuonesha ulazima wa kuwepo kwa watu waliotajwa wakati huo huo, Kanuni ya 14 (2) inatumia neno *"may"* kuonesha utashi anaoweza kutumia Kamishna kuamuru kuharibiwa kwa madawa ya kulevya bila kuwepo watu waliotajwa katika Kanuni ya 14 (1).

2.3.23 **Mheshimiwa Spika**, kwa upande mwingine matakwa ya Kanuni ya 14 (2) yanakinzana na Kanuni ya 14 (3) inayotaka wakati wa kuharibu madawa kuzingatiwe ulinzi wa afya, usalama hali kadhalika ulinzi wa mazingira; hivyo basi kukosekana kwa watu waliotajwa katika Kanuni ya 14 (1) kunaweza kuchangia ukiukwaji wa Kanuni ya 14 (3).

2.3.24 Aidha, Kanuni ya 14 (5) na 14 (7) zinaweka sharti kwa Jaji au Hakimu aliyeshuhudia kuharibiwa kwa madawa yaliyokamatwa kujiridhisha kwamba yote yameharibiwa na hatimaye kujaza fomu ya kuthibitisha hilo. Hivyo basi, kutokuwepo kwa Jaji au Hakimu kwa mujibu wa Kanuni ya 14 (2) kunaweza kusababisha zoezi hilo kutokamilika kisheria. **Kamati inashauri kuwa Kanuni ya 14 ifanyiwe marekebisho ili kuondoa mazingira yenye utata.**

KANUNI ZA MWENENDO WA MAHAKAMA ZA WATOTO ZA MWAKA 2014 (GN Na. 170 ya tarehe 13 Mei, 2016)

2.3.25 **Mheshimiwa Spika**, Kanuni hizi ni miongoni mwa Sheria Ndogo nyingi zilizochambuliwa na Kamati zinazotokana na Sheria ya Mtoto, Sura ya 13 ya Mwaka 2009. Kanuni Ndogo hizi

zimetungwa chini ya Kifungu cha 99 (1) cha Sheria hiyo. Lengo la Kanuni hizi ni kuanzisha mfumo wa Utendaji na mwenendo unaowiana na Mahakama za Watoto za Tanzania Bara na kuhakikisha kuwa haki za mtoto chini ya sheria zinalindwa.

2.3.26 **Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 21 (3)** inahusu hati ya wito shaurini kwa mtoto *(summons)* bila kutaja mazingira ambayo mtoto anaweza kuhudhuria Mahakamani akiwa au akisindikizwa na mtu mzima. Kifungu cha 99 (1) (f) cha Sheria Mama kinatoa haki kwa mtoto kuwa na ndugu wa karibu au wakili katika taratibu za kimahakama. Kamati inashauri kuwa Kanuni hii iweke sharti la kuwepo mtu wa kumsindikiza mtoto anapoitikia wito wa mahakama *(summons)*.

2.3.27 **Mheshimiwa Spika**, Kanuni ya 25 (1) inaipa Mahakama uhuru wa kutoa hati ya wito kwa mzazi/mlezi/mwangalizi kuhudhuria shauri la jinai linalomhusu mtoto pale ambapo ameshindwa kuhudhuria shauri la mtoto huyo kwa kutumia neno "*may*" (kwamba Mahakama yaweza). Katika hatua hii ya mwenendo wa shauri, Kamati inapendekeza kuwa Kanuni iweke masharti ambayo yatamlazimisha mzazi/mlezi/mwangalizi kuhudhuria shauri la jinai linalomhusu mtoto huyo kwa kutumia neno *(shall)* (kwamba Mahakama itamtaka).

2.3.28 Kanuni ya 54 (5) inaweka utaratibu wa kufuatwa pale ambapo mtoto aliyewekwa kizuizini kwa muda mrefu zaidi ya kipindi alichopangiwa kuwasilisha maombi ya kuachiwa huru kwa mamlaka husika. Hata hivyo kanuni haijaweka masharti ambayo yanamuwezesha mtoto kupata msaada wa kuwasilisha maombi hayo kutoka kwa mzazi/mlezi/mwangalizi/afisa ustawi wa jamii au mtu mwingine yeyote. **Kamati inashauri kuwa Kanuni hizi ziweke masharti ambayo yatamuwezesha**

mtoto kupata msaada wa kuwasilisha maombi kuachiwa huru kwa mamlaka husika.

KANUNI ZA AJIRA ZA WATOTO ZA MWAKA 2012 (GN Na. 168 ya tarehe 13 Mei, 2016)

2.3.29 **Mheshimiwa Spika**, Kanuni hizi zimetungwa chini ya Sheria ya Mtoto, Sura ya 13 ya Mwaka 2009. Sehemu ya Saba ya Sheria Mama inaweka masharti kuhusu haki ya mtoto kufanya kazi, makatazo na mazingira ambayo mtoto hapaswi kufanya kazi, haki za mtoto anayefanya kazi pamoja na taratibu za ufuatiliaji ustawi wa mtoto ambaye anafanya kazi.

2.3.30 **Mheshimiwa Spika,** katika uchambuzi wake, Kamati imebaini dosari kadhaa katika Sheria Ndogo hii. Moja kati ya dosari hizo ni kwamba, Kanuni hazijataja kifungu cha Sheria Mama inachotoa madaraka ya kutungwa kwa Sheria Ndogo hii.

2.3.31 Katika Kanuni ya 3 ambayo inatoa tafsiri ya maneno mbalimbali, Kamati imebaini dosari kadhaa. Kwa mfano, Kanuni zinatoa tafsiri ya neno "majengo" kwa kujumuisha magari, ndege na maeneo mengine ambayo yangeweza kutolewa tafsiri zinazojitegemea.

2.3.32 Aidha, Kanuni inatoa tafsiri ya maneno "kazi za hatari" ikimaanisha "**kazi yoyote ambayo inamuweka mtoto katika hatari ya magonjwa ya kimwili au majeraha ya kiakili**" wakati Sheria Mama inatoa tafsiri ya maneno "kazi hatarishi" kuwa ni "**kazi yoyote inayomuweka mtoto katika hatari ya kupata madhara ya kimwili au kiakili**". Tafsiri hizi mbili

zinazungumzia kitu kinachofanana lakini zinatofautiana kimaudhui na kimantiki.

2.3.33 **Kwa sababu hiyo, Kamati inashauri kuwa Kanuni ifanyiwe marekebisho ili tafsiri inayotumika katika Sheria Mama itumike katika Sheria Ndogo kwa lengo la kukidhi matakwa ya Kifungu cha 39 (1) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1.**

2.3.34 **Mheshimiwa Spika**, kwa upande mwingine Kanuni ya 7 (1) inazungumzia mtoto kutoajiriwa katika mazingira hatarishi lakini wakati huo huo inaweka masharti kuwa mazingira hayo hayatochukuliwa kuwa ni hatarishi ikiwa mtoto amefikisha umri chini ya miaka 16 na anafanya kazi chini ya uangalizi. **Kamati inashauri kuwa, maneno "chini ya miaka kumi na sita" yafutwe ili dhana ya mtoto mwenye miaka kumi na sita kufanya kazi hizo iweze kujumuishwa.**

2.3.35 Kanuni ya 9 (3) inaweka masharti yanayotambua mazingira ambayo ni hatarishi kufanya kazi ikijumuisha maeneo na hali ambazo kimsingi zinakosa uhalisia, mfano joto, kuinama, kusimama au kukaa. **Kanuni hii ifanyiwe marekebisho ili kuendana na uhalisia wa mazingira ambayo mtoto anaweza kufanya kazi.**

2.3.36 **Mheshimiwa Spika**, Kanuni ya 4 inazungumzia umri wa chini wa kuajiriwa kuwa ni miaka kumi na nne (14). Hata hivyo Kanuni 4 (2) inaweka masharti ambapo mtoto mwenye umri chini ya miaka kumi na nne anaweza kuajiriwa. **Kamati inashauri Kanuni hiyo iandikwe upya kuondoa maneno "chini ya" ili kuepuka mazingira ambayo mtoto mwenye umri chini ya miaka kumi na nne (14) anaweza kuajiriwa.**

KANUNI ZA UASILI WA WATOTO ZA MWAKA 2012 (GN Na.164 ya tarehe 13 Mei, 2016)

2.3.37 **Mheshimiwa Spika,** Kanuni hizi zimetungwa chini ya Sheria ya Mtoto, Sura ya 13 ya Mwaka 2009 kwa lengo la kufafanua masharti kuhusu taratibu za uasili wa watoto. Masharti hayo ni pamoja na maombi ya kuasili, ridhaa ya kuasili, amri ya kuasili, rejesta ya kuasili, uasili wa wazi, kuasili kwa Mtanzania asiye mkazi na kuasili kwa wageni.

2.3.38 Katika Kanuni hizi, Kamati ilibaini dosari kadhaa ambazo zinapaswa kufanyiwa kazi na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Kwa mfano, Kanuni ya 10 (1) inaweka masharti kuhusu taarifa ya kusikilizwa kwa shauri kwa mfumo ulioainishwa katika **Fomu Na. A. C6** katika majedwali. Kanuni hiyo inamtambua Afisa wa ustawi wa jamii lakini katika fomu inayotajwa hakuna sehemu inayotambua ushiriki wake.

2.3.39 Aidha, Katika Fomu Na. A.C7 aya ya 6.3 kuna maneno **"mtoto ana kilema"** yanaweza kutafsiriwa kuwa yana unyanyapaa. Maneno yanayoweza kutumika ni **"mtoto mwenye ulemavu"**. Kamati inashauri kuwa Kanuni hiyo ifanyiwe marekebisho.

2.3.40 **Mheshimiwa Spika**, Kanuni ya 16 (5) inampa Kamishna jukumu la kufuatilia taarifa za mtoto aliyeasiliwa na wazazi wanaoishi nje ya Tanzania bila kuainisha taratibu za kuzingatiwa katika kufuatilia taarifa za mtoto huyo.

2.3.41 **Kwa madhumuni ya kulinda ustawi wa watoto wanoasiliwa nje ya nchi, Kamati inashauri Kanuni ziweke bayana taratibu ambazo taarifa za mtoto huyo zitafuatiliwa kwa kuhusisha pia balozi zetu. Aidha, Kanuni ziweke bayana muda ambao**

ufuatiliaji huo utafanyika kama ilivyo katika kanuni ya 16 (1) inayohusu mtoto anayeasiliwa na wazazi wanaoishi Tanzania ambaye taarifa zake zitafuatilia miezi mitatu baada ya Amri ya kuasili kutolewa, ikihusisha kutembelea nyumba ambayo mtoto huyo anaishi.

2.3.42 **Mheshimiwa Spika**, maoni na mapendekezo ambayo Kamati imeyatoa yana lengo la kuhakikisha kuwa katika kila Kanuni ambayo imetungwa chini ya Sheria ya Mtoto, maslahi ya mtoto yanakuwa ndiyo msingi wa kuzingatiwa katika masuala yote yanayohusiana na ustawi wa mtoto *(welfare of a child should always be a priority)*.

THE COPYRIGHT AND NEIGHBOURING RIGHTS (COPYRIGHTED WORKS - COMMUNICATION TO THE PUBLIC) REGULATIONS, 2016 (GN No. 29 ya tarehe 8 Januari, 2016)

2.3.43 **Mheshimiwa Spika**, Sheria Ndogo hii imetungwa chini ya Kifungu cha 45 cha Sheria ya Hakimiliki inayoitwa *The Copyright and Neighbouring Rights Act (Cap. 218)* ambayo, pamoja na mambo mengine, ina malengo ya kulinda maslahi ya wabunifu na wasanii yatokanayo na kazi au ubunifu wao kwa kuzitambua haki za kipekee *(exclusive rights)* za watu hao na kuweka masharti ya matumizi ya kazi hizo.[18]

2.3.44 Sheria Ndogo hii inaweka masharti kuhusu namna za kuboresha mapato ya wasanii yatokanayo na kazi zao zinazotumika katika vyombo vya habari, makampuni ya simu, mitandao ya kijamii, tovuti na wavuti mbalimbali. Mapato hayo yanatokana na tozo

[18] Kifungu cha 2 cha Sheria ya Hakimiliki (The Copyright and Neighbouring Rights Act , Cap. 218)

ambazo Chama cha Hakimiliki cha Tanzania (COSOTA) kitatoza kwa watumiaji wa kazi za wasanii ambapo wasanii hao watapata mgao wa mrabaha *(royalty)* kulingana na matumizi ya kazi zao.

2.3.45 **Mheshimwa Spika,** katika Mkutano wa Kamati wa Kusikiliza Maoni ya Wadau *(Public Hearing)*, baadhi ya wadau waliofika kutoa maoni yao walidai kuwa hawakushirikishwa katika mchakato wa utungaji wa Sheria Ndogo hii. Madai hayo yalitolewa na baadhi ya wawakilishi kutoka katika vyombo vya habari na baadhi ya wanamuziki walioshiriki. Hii ilikuwa hoja kubwa ambayo iliibua mjadala mpana miongoni mwa Wajumbe wa Kamati.

2.3.46 **Mheshimiwa Spika**, moja kati ya masharti ya msingi katika mchakato wa utungaji wa Sheria yoyote ni ushirikishwaji wa wadau ili kupata maoni yao kuhusu maudhui ya Sheria husika. Hata hivyo, Sheria ya Tafsiri ya Sheria haijaweka bayana kuhusu utekelezaji wa masharti haya katika utungaji wa Sheria Ndogo.

2.3.47 Kwa utamaduni uliopo duniani katika utungaji wa Sheria Ndogo, suala la ushirikishwaji si kigezo kinachoweza kuzuia mchakato huo kukamilika na haibatilishi uhalali wa kutumika kwa Sheria Ndogo husika. Katika nchi ya Australia kwa mfano, Sheria inayoitwa *The Legislative Instruments Act, 2003* ambayo inasimamia masharti ya utungaji wa Sheria Ndogo, imeweka utaratibu katika Sehemu ya 3 wa kufanyika kwa ushirikishwaji katika mchakato wa utungaji wa Sheria Ndogo.

2.3.48 Hata hivvyo, Kifungu cha 19 cha Sheria hiyo kinabainisha kuwa Sheria Ndogo isipozingatia ushirikishwaji wa wadau,

haibatilishi uhalali wake. Hata hivyo, masharti ya ushirikishwaji yanaweza kuwa ni hoja ya msingi wakati Bunge linafanya uchambuzi wa Sheria Ndogo husika.

> *"Part 3 of the LIA provides for rule-makers to consult with interested parties before making instruments. Section 19, however, provides that failure to consult does not affect the validity of an instrument. It likewise does not affect parliamentary control, although it may be an issue in parliamentary scrutiny."*[19]

2.3.49 **Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia hayo, pamoja na kwamba Sheria yetu ya Tafsiri ya Sheria haijaweka bayana masharti kuhusu umuhimu wa ushirikishaji katika utungaji wa Kanuni *(rules and regulations)*, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo huwa haipuuzi wala kuacha kuzingatia umuhimu wa ushirikishwaji iwapo Sheria Ndogo inayozungumziwa kwa maslahi mapana ya utekelezaji wake. Kifungu cha 36 (3) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1 kinafafanua kwamba, Sheria Ndogo yoyote inatarajiwa kuwa itakuwa imezingatia hatua zote za awali katika kutungwa kwake iwapo hakuna ushahidi wa jambo hilo kutofanyika. Kifungu hicho kinasema:-

> *"**36.-** (3) It shall be presumed, in the absence of evidence to the contrary, that all conditions and preliminary steps precedent to the making of subsidiary legislation have been complied with and perfomed"*

2.3.50 **Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitaka ufafanuzi kutoka Serikalini kuhusu ukweli wa madai kwamba wadau hawakushirikishwa. Mhe. Charles Mwijage (MB), Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji alikanusha madai hayo kwa kusema kuwa, Wizara yake kwa kushirikiana na COSOTA iliwashirikisha wadau katika

[19] Odger's Australian Senate Practice, 13th Ed., Pg. 437

maandalizi ya Sheria Ndogo hii. COSOTA iliwasilisha nakala za vielelezo mbalimbali vinavyoonesha namna ambavyo Wizara ilishirikisha wadau.

2.3.51 **Mheshimiwa Spika**, baada ya Kamati kufanya uchunguzi wake ilibaini kuwa, mwitikio wa baadhi ya wadau kushiriki katika maandalizi ya Sheria Ndogo hii ulikuwa hafifu. Iwapo wadau wengine ambao wanalalamika kutoshirikishwa walipata barua za mwaliko lakini hawakushiriki kwa sababu yoyote, malalamiko yao hayatakuwa na msingi. Lakini iwapo taarifa hazikufika, wadau hao wana hoja ya msingi.

2.3.52 **Mheshimiwa Spika,** kwa namna yoyote, kwa kuwa malalamiko yapo na kwa kuzingatia kuwa, wadau wanaolalamika wana maslahi muhimu katika utekelezaji wa Sheria Ndogo hii, Kamati inashauri yafuatayo:-

a) Kwa kuwa Sheria Ndogo hii imeanza kutumika kisheria baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali kwa GN Na. 29 ya tarehe 8 Januari, 2016, Wizara ya Viwanda na Biashara kwa kushirikiana na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ifanye mikutano na makundi ya wadau wote wanaoathirika na Sheria Ndogo hii ili kuwapa elimu ya kutosha kuhusu maudhui yake. Aidha, mikutano hiyo itumike kama jukwaa la mjadala wa maudhui ya Sheria Ndogo hii ili Serikali ipate mawazo mapya ambayo yataiboresha na kurahisisha utekelezaji wake.

b) Wadau ambao wanaathirika na Sheria Ndogo hii, watumie fursa hii kuhamasishana kushiriki mikutano hiyo na kutoa maoni yatakayoboresha maudhui yake. Kwa mfano, vyombo

vya habari kwa kutumia rasimilimali zake vitoe matangazo ili ushiriki wa wadau wote uwe na tija zaidi.

2.3.53 **Mheshimiwa Spika**, mapendekezo haya yana lengo la kuhakikisha kuwa, wasanii na wabunifu wanashiriki kikamilifu na wanafaidika na kazi zao kwa mapato yatokanayo na matumizi ya kazi hizo. Aidha, kwa kuzingatia jitihada za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John P. Magufuli katika kuhakikisha uchumi wa nchi unaendeshwa kwa viwanda, kazi za wasanii na wabunifu zinakuwa ni sehemu ya ongezeko la pato la nchi na kukuza uchumi.

2.3.54 **Mheshimiwa Spika**, katika Mkutano baina ya Kamati na wadau, baadhi ya walioshiriki walikuwa na maoni kuhusu utendaji wa COSOTA. Wapo wanaodhani kuwa chombo hiki muhimu kwa ustawi wa wasanii na wabunifu kingefaa kuwa chini ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Mapendekezo haya yalitolewa na washiriki katika vikao vya Kamati ambao wanadhani kuwa COSOTA haitekelezi majukumu yake ipasavyo ya kuwasaidia wasanii na wabunifu chini ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

2.3.55 Maoni haya pia yalitolewa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii katika taarifa yao kuhusu Bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017[20] ambapo walisema:-

> *"**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuwa Chama cha Hakimiliki nchini (COSOTA) kinasimamiwa na Wizara ya Viwanda na Biashara. Hii imekuwa changamoto katika*

[20] Taarifa Kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 Pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017, Uk. 15

uratibu wa shughuli za wasanii na hivyo ***Kamati inashauri COSOTA iwe chini ya Wizara ya Habari ili kurahisisha uratibu wa kazi za Wasanii na hata kuipa dhamana Wizara ya Habari kuisimamia ipasavyo.****"*

2.3.56 **Mheshimiwa Spika,** Kamati yangu inashauri kuwa, Serikali ifanye upembuzi yakinifu na kufanya uamuzi kuwa chombo hiki muhimu kinapaswa kutekeleza majukumu yake chini ya Wizara gani kwa kuzingatia maoni yaliyotolewa. Aidha, taarifa ya uamuzi huo iwasilishwe ndani ya Bunge hili ili Wabunge wapate mrejesho kuhusu maoni yao kwa Serikali.

THE INSTITUTE OF JUDICIAL ADMINISTRATION LUSHOTO (STUDENTS' GENERAL WELFARE, CONDUCT AND DISCIPLINARY MATTERS) REGULATIONS, 2015 (GN No. 511 ya tarehe 6 Novemba, 2015)

2.3.57 **Mheshimiwa Spika**, Sheria Ndogo hii imetungwa chini ya Kifungu cha 23 cha Sheria iliyotungwa na Bunge inayoitwa ***The Institute Of Judicial Administration Lushoto (CAP 405)***. Sheria Ndogo hii inahusu masuala ya ustawi na nidhamu kwa wanafunzi wa Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto (IJA).

2.3.58 **Mheshimiwa Spika**, Kanuni ya 13 (1) ya Sheria Ndogo hii inatoa adhabu ya mwanafunzi kusimamishwa masomo *(suspension)* endapo atashitakiwa kwa kosa la jinai. Aidha, Kanuni ya 13 (4) inaweka sharti kwamba muda wa kusimamishwa kwa mwanafunzi huyo ukizidi miaka miwili (2) mfululizo *(two consecutive academic years)* atakuwa amekoma kuwa mwanafunzi. Kanuni ya 13 ya Sheria Ndogo hii inasomeka kama ifuatavyo:-

"13.- (1) The Institute ***shall suspend*** *any student* ***charged with any criminal*** *offence in any court of law.*

(2) Where a student is suspended under the provisions of sub-regulation (1) of this Regulation, he shall not be reinstated as a student until he produces the judgment of a court acquitting him.

(3) Any student who has been reinstated under sub-regulation (2) of this Regulation shall be re-suspended where an appeal has been preferred against him in the case he was facing and, such suspension shall continue until the final determination of the appeal.

(4) A student whose ***suspension period exceeds two consecutive academic years shall cease to be a student*** *of the Institute.*

(5) Any student who is convicted of any criminal offence shall cease immediately upon such a conviction to be a student of the Institute." Msisitizo ni wetu.

2.3.59 **Mheshimiwa Spika**, kwa maoni ya Kamati, masharti ya Kanuni hii yako kinyume na masharti ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya Ibara ya 13 (6) (b) inayosema:-

"ni marufuku kwa mtu yeyote aliyeshitakiwa kwa kosa la jinai kutendewa kama mtu mwenye kosa hilo mpaka itakapothibitika kuwa anayo hatia ya kutenda kosa hilo."

2.3.60 Ibara hii inaweka masharti ya msingi ya haki za binadamu ya kutomchukulia mtu aliyeshitakiwa kuwa mkosaji mpaka pale mahakama itakapothibitisha kuwa ni mkosaji yaani "*presumption of innocence*".

2.3.61 **Mheshimiwa Spika**, Kamati iliwasilisha hoja hiyo kwa Wizara ya Katiba na Sheria ili iweze kutoa ufafanuzi. Kwa maelezo ya Wizara, Sheria Ndogo hii **ni lazima** isomwe pamoja na Sheria Ndogo inayoitwa ***The Institute Of Judicial Administration Lushoto (Students' Performance Assessment) Regulations, 2015*** (GN No. 510 ya tarehe 6 Novemba, 2015) inayohusu masuala ya masomo na mitihani ya Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto (IJA).

2.3.62 Kwa maelezo ya Wizara, Kanuni ya 19 ya Sheria Ndogo hiyo, inaweka sharti kwamba ili mwanafunzi afanye mitihani anapaswa kuwa amehudhuria vipindi vya darasani kwa asilimia themanini (80%). Kama hatahudhuria kwa muda huo hata kama hana kesi ya jinai, anaweza kuwa mgonjwa na hivyo chini ya Kanuni ya 37 ya Sheria Ndogo hiyo anaweza kuomba kuahirisha masomo kwa mwaka mmoja na akarudia baada ya mwaka mmoja kuendelea alipoishia ila ikizidi miaka miwili anapaswa kuomba upya kujiunga na kimsingi hawezi kukataliwa ila ni kwa ajili ya kuangalia muda ambao amekuwa nje ya masomo ni vigumu kuwa sambamba na wenzake.

2.3.63 **Mheshimiwa Spika**, maelezo ya Wizara hayakuiridhisha Kamati kwa sababu, ukisoma Kanuni ya 13 (1) ya Sheria Ndogo iliyochambuliwa na Kamati, inasema bayana maneno yafuatayo "*The Institute **shall suspend** any student **charged** with any criminal offence in **any court of law**.*" Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii, *suspension* ya mwanafunzi huyo itatokea mara tu **atakaposhitakiwa** *(charged)*. Kitendo cha kumsimamisha mwanafunzi masomo *(suspension)* kinaweza kutafsiriwa kuwa ni kumpa adhabu mwanafunzi huyo kwa sababu tu ameshitakiwa katika mahakama fulani.

2.3.64 **Mheshimiwa Spika**, Kamati inashauri Wizara ya Katiba na Sheria kuifanyia marekebisho Sheria Ndogo hiyo. Iwapo Kanuni za Sheria Ndogo kama zitabaki kubaki kama zilivyo, ni wazi kwamba Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itaendela kuvunjwa na watu kukosa haki zao za msingi.

2.4 MAJUKUMU MENGINE

a) Mikutano na Wadau wa Mchakato wa Utungaji wa Sheria Ndogo

2.4.1 **Mheshimiwa Spika,** kwa nyakati tofauti kati ya tarehe 15 – 18 Machi, 2016 Kamati ilikutana na taasisi zinazohusika na mchakato wa utungaji wa Sheria Ndogo kwa lengo la kupata elimu kuhusu hatua mbalimbali za utungaji wa Sheria Ndogo na kubaini changamoto zilizopo. Taasisi hizo ni zifuatazo:-

i) Idara ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali;

ii) Ofisi ya Rais TAMISEMI; na

iii) Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria wa Serikali.

2.4.2 **Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Sheria Ndogo ilitembelea Ofisi ya Mpiga Chapa Mkuu **wa** Serikali tarehe 15 Machi, 2016 ambapo wajumbe walipata fursa ya kujionea maeneo mbalimbali ambayo Sheria Ndogo hupitia katika hatua za uchapaji. Katika ziara hiyo Wajumbe walipata fursa pia ya kuuliza maswali kadhaa juu ya changamoto zinazoikabili Ofisi ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali katika hatua za uchapaji wa Sheria Ndogo.

2.4.3 **Mheshimiwa Spika**, Idara ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali ni muhimu katika mchakato wa utungaji wa Sheria Ndogo kwa kuwa huchapisha Sheria Ndogo zote nchini na kuzitangaza

katika Gazeti la Serikali. Idara hii isipotekeleza majukumu yake kwa ufanisi, Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni hawezi kuwasilisha kwa wakati Sheria Ndogo kwa mujibu wa masharti ya Kifungu cha 38 cha Sheria ya Tafsiri, Sura ya 1.

2.4.4 Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa Idara hii haiendeshwi kwa viwango vinavyokidhi mahitaji yaliyopo. Kwa mfano, katika vikao vya Kamati vilivyopita, Kamati haikupokea kwa wakati Sheria Ndogo mbalimbali kwa sababu hazikuwa zimechapishwa na Mpiga Chapa wa Serikali. Dosari hii inatokana na ukweli kwamba, Idara ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali inatekeleza majukumu yake chini ya kiwango kinachotakiwa kwa maendeleo ya teknolojia iliyopo.

2.4.5 Katika ziara hiyo, Wajumbe walijionea mitambo ambayo ni chakavu, majengo yaliyo chini ya kiwango pamoja na uhaba mkubwa wa vitendea kazi. Haya yote yalibainika huku Serikali nzima na vyombo vyake ikiitegemea Ofisi hii kuchapisha nyaraka mbalimbali muhimu zikiwemo Sheria Ndogo zote nchini.

2.4.6 **Mheshimiwa Spika**, Kamati haikuridhishwa na maelezo ya Menejimenti ya Idara ya Mpigachapa Mkuu wa Serikali kuhusu uendeshaji na utendaji wa Idara hiyo. Kwa upande mwingine, Kamati haikuridhishwa na hatua ya Idara hiyo kutumia fedha za umma kununua mashine ya uchapaji kwa gharama kubwa na mashine hiyo kufanya kazi kwa muda mfupi. Kamati inashangaa kwa nini hadi wakati Kamati inafanya ziara hiyo, mashine hiyo ilikuwa haifanyi kazi.

2.4.7 **Mheshimiwa Spika**, Kamati ilibaini pia kuwa kazi nyingi za Idara ya Mpigachapa wa Serikali zinafanywa nje ya Idara kwa

sababu printa ya ofisi hiyo huzidiwa na kazi. Kwa kutoa kazi hizo nje, kazi kuchelewa na kutomalizika kwa wakati na hata kupoteza usiri wa kazi za Serikali na gharama pia huongezeka. Kamati inashauri Serikali kuchukua hatua za haraka kuiboresha Idara hii ili iachane na tabia ya kuchapisha nyaraka za Serikali nje ya Idara hiyo ambayo inahatarisha usalama wa nyaraka na kuongeza gharama kwa Serikali.

2.4.8 **Mheshimiwa Spika**, Kamati yangu inaunga mkono maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria katika Taarifa yao kuhusu Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu[21] ambapo walishauri kwamba, Ofisi ya Waziri Mkuu iboreshe mitambo na mazingira ya Idara ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa kuiwezesha kufanya shughuli zake kibiashara zaidi.

2.4.9 **Kamati inashauri kwamba, menejimenti ya Ofisi ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali ifanyiwe mabadiliko kwa sababu kwa muda mrefu, Ofisi hii muhimu imekuwa haitekelezi majukumu yake kwa ufanisi. Aidha, maslahi na mazingira ya kazi kwa watumishi wa Ofisi hiyo yanapaswa kuboreshwa ili kuendana na shughuli wanazozifanya.**

2.4.10 **Mheshimiwa Spika**, tarehe 18 Machi, 2016 Kamati ilikutana na Bi. Sara Barahomoka, Mwandishi Mkuu wa Sheria wa Serikali, kwa lengo la kufahamu taratibu juu za uandishi wa Sheria Ndogo. Katika kikao hicho, Bi. Barahomoka alitoa ufafanuzi kuhusu masuala yafuatayo:-

i) Nafasi na majukumu ya Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria kwa mujibu wa Sheria

[21] Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria Kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi Hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2016, Uk. 21

ii) Hatua za msingi katika mchakato wa utungaji wa Sheria Ndogo

iii) Changamoto zinazoikabili Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria katika mchakato wa utungaji wa Sheria Ndogo

2.4.11 **Mheshimiwa Spika**, hatua hii ya Kamati kukukutana na Mwandishi Mkuu wa Sheria wa Serikali, iliwawezesha Wajumbe kupata ufahamu wa kutosha kuhusu masuala mbalimbali ya uandishi wa Sheria Ndogo, elimu ambayo imewasaidia kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi.

2.4.12 **Mheshimiwa Spika**, kutokana na Kamati kufanya ziara na kukutana na Taasisi hizi, iliweza kupata taarifa ya kutosha ya rejea mbalimbali ambazo ziliisaidia Kamati kutekeleza kazi ya uchambuzi kwa ufanisi zaidi.

b) Mikutano na Wadau wa Mazao

2.4.13 **Mheshimiwa Spika**, Kamati pia ilipata fursa ya kukutana na wadau wa mazao mbalimbali katika jitihada za kuanza kuzishughulikia Sheria Ndogo zinazowagusa ili waweze kutoa maoni yao kuhusu utekelezaji wa Sheria Ndogo hizo, changamoto wanazokabiliana nazo katika uzalishaji na uuzaji wa mazao hayo. Baadhi ya wadau waliofika mbele ya Kamati ni wafuatao:-

i) Western Zone Tobacco Growers Cooperative Union Ltd.

ii) Wakulima wa Tumbaku

iii) Watafiti wa Zao la Pamba

2.4.14 **Mheshimiwa Spika,** uamuzi wa Kamati kuweka utaratibu wa vikao na wadau wa mazao una lengo la kuunga mkono jitihada za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. John P. Magufuli katika kupunguza au kuondoa kero kwa wakulima wa mazao mbalimbali zitokanazo na tozo mbalimbali zinazowekwa na Sheria Ndogo tofauti.

2.4.15 **Mheshimiwa Spika**, katika hotuba ya Mhe. Dkt. John P. Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati wa ufunguzi wa Bunge la Kumi na Moja alinukuliwa akisema:-

> *"Mheshimiwa Spika, wakulima wote wa kahawa wa Kagera wanataka kahawa yao wakaiuze Uganda lakini tulipouliza, wana kodi zaidi ya ishirini na sita. Kwa kuzingatia kuwa na kodi hizo zaidi ya ishirini na sita, bei wanayopewa wakulima wa kahawa kule Kagera na maeneo mengine inakuwa ndogo zaidi ukilinganisha na bei wanayopewa katika nchi jirani ya Uganda na ndiyo maana wananchi wanachukua risk hata ya kwenda kuzama kwenye maji lakini wawe wanasafirisha kahawa. Ndiyo maana nasema, kodi hizi za hovyo na ambazo ni kero kwa wakulima wetu katika mazao ya kahawa, mahindi, chai, pamba, korosho, mkonge, ngozi, nyama, maziwa na samaki tutahakikisha tutaziondoa kama si kuzipunguza kwa kiasi kikubwa sana."*

2.4.16 **Mheshimiwa Spika**, kwa mfano katika kusikiliza maoni ya wadau hao, Kamati ilibaini kuwepo kwa mlolongo wa kodi na tozo katika zao la pamba. Kodi na tozo hizo ni pamoja na

i) ushuru wa mazao
ii) ushuru wa elimu
iii) leseni ya biashara
iv) leseni ya kituo cha manunuzi
v) leseni ya uchambuzi
vi) mchango wa mwenge
vii) maombi ya leseni ya manunuzi

viii) ada ya kikao cha halmashauri

ix) faini ya uendeshaji na

x) kodi ya mapato.

2.4.17 **Mheshimiwa Spika**, mlolongo wa kodi na tozo hizi unaleta mzigo mkubwa kwa mkulima na hivyo kuathiri uzalishaji na kipato cha mkulima.

2.4.18 **Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua kwamba, tozo ambazo zinazungumziwa zinatokana na Sheria Ndogo mbalimbali zikiwemo Sheria Ndogo za Halmashauri *(By – Laws)* pamoja na Sheria Ndogo za Wizara *(Regulations)* katika mazao tofauti zikiwemo zifuatazo:-

i) Kanuni zinazoratibu uzalishaji na soko la zao la pamba *(The Cotton Industry Regulations, 2011)*

ii) Kanuni zinazohusu soko la zao la korosho *(The Cashewnut (Marketing) Regulations, 1998)*

iii) Kanuni zinazohusu uzalishaji na soko la zao la kahawa *(The Coffee Industry Regulations, 2013)*

iv) Kanuni za Mazao Mchanganyiko *(The Cereals and Other Produce Regulations, 2011)*

2.4.19 **Mheshimiwa Spika**, kwa kadri ya muda utakavyoruhusu na kwa kadri itakavyowezekana, Kamati itafanya uchambuzi wa kina wa Sheria Ndogo mbalimbali katika maeneo yafuatayo:-

i) Kilimo cha mazao ya biashara na chakula

ii) Ufugaji

iii) Uvuvi

iv) Biashara za mama lishe

v) Bodaboda

2.4.20 Uchambuzi wa Sheria Ndogo hizo na nyingine, unaweza kusaidia juhudi za Rais katika kupunguza migogoro baina ya wakulima na wafugaji, kupunguza kero kwa wananchi na kuongeza ufanisi wa ukusanyaji wa mapato ya Serikali.

3.0 MAONI YA JUMLA

3.1 UANDISHI WA SHERIA NDOGO

3.1.1 **Mheshimiwa Spika**, Kamati inapendekeza kwamba, mamlaka zote zilizokasimiwa na Bunge madaraka ya kutunga Sheria Ndogo zihakikishe kuwa zinazingatia misingi ya Katiba na haki za binadamu wakati wa uandishi. Aidha, kwa madhumuni ya utekelezaji bora wa masharti ya Kifungu cha 39 (1) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1, masharti yanayopatikana katika Sheria Ndogo yaendane na masharti ya Sheria Mama zinazotoa madaraka.

3.1.2 **Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwa baadhi ya Halmashauri zimekuwa zikinakili Sheria Ndogo kutoka katika Halmashauri nyingine neno kwa neno *(copying and pasting)* bila kufanya marekebisho ya msingi na kusababisha kunakili dosari za Sheria Ndogo hizo.

3.1.3 Kwa mfano, katika **Sheria Ndogo za (Afya na Usafi wa Mazingira) za Halmashauri ya Wilaya ya Geita, 2015** na **Sheria Ndogo za (Afya na Usafi wa Mazingira) za Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe, 2015** zote kwa pamoja zimeweka marufuku kupanda mimea mirefu maeneo ya mjini katika kifungu cha 6 cha kila Sheria Ndogo. Aidha katika kifungu cha 8 cha kila Sheria Ndogo za halmashauri hizo, imeweka wajibu

kwa mmiliki wa nyumba kuweka *"pavements"* mbele ya nyumba yake. Sheria Ndogo hizo, kwa sehemu kubwa zinafanana neno kwa neno bila kuzingatia dosari zilizopo au utofauti wa mazingira ya halmashauri husika.

3.1.4 **Kamati inazishauri halmashauri zote kuhakikisha kuwa zinajiridhisha kikamilifu kabla ya kunakili Sheria Ndogo yoyote kutoka Halmashauri nyingine ili kutunga Sheria Ndogo kulingana na hali halisi ya Halmashauri husika.**

3.1.5 **Mheshimiwa Spika**, katika baadhi ya Sheria Ndogo zilizofanyiwa uchambuzi na Kamati zilibainika kuwa na makosa mengi ya kiuandishi na kiuchapaji kiasi cha masharti ya Sheria Ndogo hizo kupoteza maana. Aidha, baadhi ya rejea za vifungu katika majedwali zilikosewa kiasi cha kuleta mkanganyiko wa tafsiri. **Kamati inashauri kuwa mapitio ya Sheria Ndogo mbalimbali yafanyike ili kuondoa dosari hizo.**

3.1.6 **Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Ofisi ya Rais (TAMISEMI) kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, iandae programu ya mafunzo ya mara kwa mara kwa Wanasheria wa Wizara na Halmashauri zote nchini ili kuwajengea uwezo wa kuandika Sheria Ndogo ambazo zinakidhi matakwa na masharti ya Katiba, Sheria Mama na Sheria nyingine za nchi.

3.2 MCHAKATO WA UTUNGAJI WA SHERIA NDOGO

3.2.1 Kamati inashauri mamlaka zote ambazo zimekasimiwa na Bunge madaraka ya kutunga sheria kuzingatia kikamilifu ushirikishwaji wa wadau wanaolengwa na Sheria Ndogo yoyote.

3.2.2 Ofisi ya Rais (TAMISEMI) ianze kutumia mfumo wa kielektroniki wa ufuatiliaji wa upitishaji wa Sheria Ndogo katika hatua mbalimbali *(The By – Laws Database)* ili kuhakikisha kuwa Sheria Ndogo hizo zinakidhi vigezo vinavyotakiwa kabla ya hatua ya uchapishwaji katika magazeti ya Serikali na kuanza kutumika.

3.2.3 Serikali iongeza idadi ya Rasilimali watu katika Idara za Ofisi ya Rais (TAMISEMI) na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali hasa vitengo vinavyohusika na upitiaji wa Sheria Ndogo ili kuhakikisha makosa yanayojitokeza katika Sheria Ndogo yanafanyiwa kazi kabla ya Sheria hizo kuanza kuchapishwa katika Gazeti la Serikali na kuanza kutumika.

3.2.4 Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua za haraka katika kuzifanyia marekebisho Sheria Ndogo zote zenye dosari na ambazo zinalalamikiwa kuwa zinawakandamiza wananchi. Baada ya marekebishao hayo kufanyika, Sheria Ndogo hizo ziwasilishwe Bungeni kwa mujibu wa Sheria ili Kamati yangu ipate fursa ya kuzifanyia uchambuzi wa kina. Hatua hii itaiwezesha Serikali kulifanyia kazi tamko la Waziri Mkuu kuhusu kupunguza kodi katika mazao mbalimbali, kupunguza tozo zinazohusiana na masuala ya maliasili na utalii kama vile tozo za kitanda na Sheria Ndogo nyingine yoyote ambayo ni kero kwa wananchi.

3.2.5 Kwa kuzingatia masharti yanayopatikana katika Kifungu cha 38 cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1, Kamati inaishauri Serikali kujiwekea utaratibu wa kuwasilisha kwa wakati katika kila Mkutano wa Bunge, Sheria Ndogo zote zilizochapishwa tangu Kikao cha mwisho cha Mkutano wa Bunge uliopita. Hatua hii italiwezesha Bunge kutekeleza majukumu yake kikamilifu laini pia litaepusha mgogoro wa kiutendaji wa Sheria Ndogo yoyote ambayo Bunge linaweza kuazimia isitumike kwa kutowasilishwa Bungeni kwa wakati

4.0 HITIMISHO

4.1 SHUKURANI

4.1.1 **Mheshimiwa Spika**, napenda kutumia fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwako binafsi na Bunge lako tukufu kwa kuweka utaratibu wa taarifa ya Kamati ya Sheria Ndogo kuwasilishwa katika Bunge lako tukufu. Ni matumaini yangu kwamba, utaratibu huu utakuwa endelevu na umuhimu wa Kamati hii katika maendeleo ya nchi yetu utaonekana.

4.1.2 Kwa moyo wa dhati kabisa nimshukuru Mhe. Jenista Mhagama (MB) – Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Walemavu) kwa uratibu ambao uliiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha, niwashukuru Mawaziri na Naibu Mawaziri wa sekta mbalimbali kwa kufika mbele ya Kamati na kujibu hoja zilizoibuliwa na Wajumbe wa Kamati. Kwa heshima na taadhima naomba niwatambue kwa jinsi walivyofika mbele ya Kamati kama ifuatavyo:-

1. Mhe. George Simbachawane (Mb) – Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI)

2. Mhe. William Lukuvi (Mb) –Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

3. Mhe. Prof. Sospeter Muhongo (Mb) - Waziri wa Nishati na Madini

4. Mhe. Dkt. Harrison Mwakyembe (Mb) –Waziri wa Katiba na Sheria

5. Mhe. Ummy Mwalimu (Mb) – Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto

6. Mhe. Prof. Joyce Ndalichako (Mb) – Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi

7. Mhe. Charles Mwijage (Mb) - Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji

8. Mhe. Selemani Jafo (Mb) – Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa) -TAMISEMI

9. Mhe. Eng. Stella Manyanya (Mb) - Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi

10. Mhe. Dkt. Medard Kalemani (Mb) – Naibu Waziri wa Nishati na Madini

11. Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji (Mb) – Naibu Waziri wa Fedha na Mipango

4.1.3 Aidha, napenda kuchukua fursa hii kuishukuru Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ushiriki wao katika vikao vya uchambuzi wa Sheria Ndogo mbalimbali. Vilevile niwashukuru wadau mbalimbali waliofika mbele ya Kamati na kuwasilisha maoni yao na wale wote ambao waliwasilisha maoni yao kwa maandishi *(submissions).* Ushiriki wao katika

vikao vya Kamati pamoja na maoni waliyowasilisha ni muhimu kwa Kamati katika utekelezaji bora wa shughuli zake.

4.1.4 **Mheshimiwa Spika**, kipekee kabisa niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Sheria Ndogo kwa kazi kubwa na nzuri ya kuchambua Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Pili, Mkutano Tatu na Mkutano wa Tatu wa Bunge la Kumi na Moja na hatimaye kufanikisha kazi hii. Kwa heshima kubwa naomba kuwatambua majina yao kama ifuatavyo:-

1.	Mhe. Andrew John Chenge (Mb)	**Mwenyekiti**
2.	Mhe. William Mganga Ngeleja (Mb)	Makamu Mwenyekiti
3.	Mhe. Abdallah Ally Mtolea (Mb)	Mjumbe
4.	Mhe. Halima James Mdee (Mb)	Mjumbe
5.	Mhe. Tundu Antipas Mughway Lissu (Mb)	Mjumbe
6.	Mhe. Daniel Edward Mtuka (Mb)	Mjumbe
7.	Mhe. Rashid Ali Abdallah (Mb)	Mjumbe
8.	Mhe. Aida Joseph Khenani (Mb)	Mjumbe
9.	Mhe. Ridhiwani Jakaya Kikwete (Mb)	Mjumbe
10.	Mhe. Esther Michael Mmasi (Mb)	Mjumbe
11.	Mhe. Salome Wycliffe Makamba (Mb)	Mjumbe
12.	Mhe. Hassani Seleman Kaunje (Mb)	Mjumbe
13.	Mhe. Sadifa Juma Khamis (Mb)	Mjumbe
14.	Mhe. Khamis Mtumwa Ali (Mb)	Mjumbe
15.	Mhe. Hassan Elias Massala (Mb)	Mjumbe
16.	Mhe. Leonidas Tutubert Gama (Mb)	Mjumbe
17.	Mhe. Almas Athuman Maige (Mb)	Mjumbe
18.	Mhe. Goodluck Asaph Mlinga (Mb)	Mjumbe
19.	Mhe. Kiteto Zawadi Koshuma (Mb)	Mjumbe
20.	Mhe. Elibariki Emmanuel Kingu (Mb)	Mjumbe

4.1.5 **Mheshimiwa Spika**, aidha napenda kuwashukuru kwa dhati Watumishi wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi mahiri wa Dkt. Thomas D. Kashililah, Katibu wa Bunge kwa ushirikiano wanaoipatia Kamati hii ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Nimshukuru pia Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein akisaidiwa na Bi. Angelina Sanga, Mkurugenzi Msaidizi kwa usimamizi mzuri katika uratibu wa Shughuli za Kamati.

4.1.6 Mwisho lakini si kwa umuhimu, niwashukuru Makatibu wa Kamati ya Sheria Ndogo, Ndg. Yona Kirumbi, Ndg. Angela Shekifu, Ndg. Mkuta Masoli, Ndg. Stanslaus Kagisa wakisaidiwa na Ndg. Paul Chima kwa kuratibu vyema Shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

4.2 HOJA

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja.

Andrew J. Chenge (Mb)
MWENYEKITI
KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO
NOVEMBA, 2016

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA

KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO

JEDWALI LA UCHAMBUZI WA SHERIA NDOGO ZILIZOWASILISHWA KATIKA MKUTANO WA PILI, MKUTANO WA TATU NA MKUTANO WA NNE WA BUNGE

BUNGE LA KUMI NA MOJA

ORODHA YA SHERIA NDOGO ZILIZOWASILISHWA KATIKA MKUTANO WA PILI, MKUTANO WA TATU NA MKUTANO WA NNE WA BUNGE NA KUFANYIWA UCHAMBUZI NA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO

1. REGULATIONS UNDER THE PEGROLEUM (BULK PROCUREMENT) 2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 508 OF 2015)

2. REGULATIONS UNDER THE EXAMINATION,2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 509 0F 2015)

3. REGULATION UNDER THE INSTITUTE OF JUDICIAL ADMINISTARTION LUSHOTO (STUDENT'S GENERAL WELFARE, CONDUCT AND DISCIPLINARY MATTERS)2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 511 OF 2015)

4. SHERIA YA KODI YA MAJENGO YA MAMLAKA YA MIJI HALMASHAURI YA MANISPAA YA KIGOMA UJIJI (TANGAZO LA SERIKALI NA. 516 LA MWAKA 2015)

5. SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA MIFUGO) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA BABATI,2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 518 LA MWAKA 2015)

6. SHERIA NDOGO (ADA NA USHURU) ZA HALMASHAURI YA WILAYA BABATI, 2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 519 LA MWAKA 2015)

7. SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA MADINI YA UJENZI NA CHUMVI) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA BABATI, 2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA.520 LA MWAKA 2015)

8. SHERIA NDOGO ZA (KUHIFADHI BARABARA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA BABATI (TANGAZO LA SERIKALI NA. 521 LA MWAKA 2015)

9. SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA MAZAO) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA BABATI, 2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 522 LA MWAKA 2015)

10. SHERIA NDOGO ZA (UANZISHAJI WA BODI YA MFUKO WA ELIMU) ZA HALMASHAURI YA MJI WA KOROGWE, 2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 523 LA MWAKA 2015)

11. SHERIA NDOGO ZA UANZISHAJI WA MFUKO WA AFYA YA JAMII (TIBA KWA KADI) ZA HALMASHAURI YA MJI WA KOROGWE ZA MWAKA 2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 524 LA MWAKA 2015)

12. SHERIA NDOGO ZA (MATUMIZI YA BARABARA) ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINONDONI ZA MWAKA 2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 525 LA MWAKA 2015)

13. SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA HUDUMA) ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINONDONI 2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 526 LA MWAKA 2015)

14. SHERIA NDOGO ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINONDONI (ADA NA USHURU) (MAREKEBISHO) 2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 527 LA MWAKA 2015)

15. SHERIA NDOGO ZA UANZISHAJI WA MFUKO WA AFYA YA JAMII (TIBA KWA KADI) ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINONDONI,2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 528 LA MWAKA 2015)

16. HATI RASMI (UANZISHAJI WA BODI YA HUDUMA ZA AFYA) YA HALMASHAURI YA MJI WA KOROGWE ZA MWAKA 2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 529 LA MWAKA 2015)

17. REGULATION UNDER THE FIRE AND RESCUE FORCE (FIRE PRECAUTIONS IN BUILDINGS, 2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 533 LA MWAKA 2015)

18. KANUNI ZA KUDUMU ZA HALMASHAURI YA JIJI LA MBEYA ZA MWAKA 2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 534 LA MWAKA 2015)

19. KANUNI ZA KUDUMU ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA BUKOBA, 2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 535 LA MWAKA 2015)

20. KANUNI ZA KUDUMU ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINONDONI, 2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA 536 LA MWAKA 2015)

21. REGULATION UNDER THE PUBLIC PRIVATE PARTNERSHIP, 2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 542 OF 2015)

22. KANUNI ZA KUDUMU ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA ILEJE ZA MWAKA 2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 547 LA MWAKA 2015)

23. KANUNI ZA KUDUMU ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA BUKOMBE ZA MWAKA 2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 548 LA MWAKA 2015)

24. KANUNI ZA KUDUMU ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA MBOGWE ZA MWAKA 2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 549 LA MWAKA 2015)

25. KANUNI ZA KUDUMU ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA TEMEKE, 2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 555 LA MWAKA 2015)

26. SHERIA NDOGO ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA KOROGWE (USHURU WA MAZAO) (MAREKEBISHO) 2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA 556 LA MWAKA 2015)

27. SHERIA NDOGO HALMASHAURI YA WILAYA YA KOROGWE (USHURU WA MADINI YA UJENZI) (MAREKEBISHO) 2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 557 LA MWAKA 2015)

28. SHERIA NDOGO ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA KOROGWE (ADA NA USHURU) (MAREKEBISHO) 2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 558 LA MWAKA 2015)

29. SHERIA NDOGO ZA (AFYA NA USAFI WA MAZINGIRA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA KOROGWE,2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 559 LA MWAKA 2015)

30. KANUNI ZA KUDUMU ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOSHI MWAKA 2014 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 562 LA MWAKA 2015).

31. SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA STENDI YA MABASI) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA SAME ZA MWAKA 2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA 563 LA MWAKA 2015)

32. SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA PUMBA ZA NAFAKA) ZA HALMASHAURI WILAYA YA SAME ZA MWAKA 2015 (TANGAZO LA SERIKALI N. 564 KA MWAKA 2015)

33. SHERIA NDOGO ZA (KUDHIBITI UNYWAJI HOLELA WA VILEO) ZA HALMASHAURI ZA WILAYA YA SAME ZA MWAKA 2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 565 LA MWAKA 2015)

34. SHERIA NDOGO ZA (ADA NA USHURU) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA LINDI ZA MWAKA 2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 556 LA MWAKA 2015)

35. SHERIA NDOGO ZA (UANZISHAJI WA BODI YA MFUKO WA ELIMU) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA LINDI, 2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 567 LA MWAKA 2015)

36. SHERIA NDOGO ZA (UANZISHAJI WA MFUKO WA AFYA YA JAMII) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA SIKONGE ZA MWAKA 2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 568 LA MWAKA 2015)

37. SHERIA NDOGO ZA (UANZISHAJI WA BODI YA MFUKO WA ELIMU) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA SIKONGE ZA MWAKA 2015 (TANGAZO LA SERIKALI LA NA. 569 LA MWAKA 2015)

38. SHERIA NDOGO ZA (KODI YA HUDUMA) ZA HALMASHAURI ZA WILAYA YA SIKONGE, 2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 570 LA MWAKA 2015)

39. SHERIA NDOGO ZA (KILIMO NA UHIFADHI WA CHAKULA) ZA HALMASHAURI YA WALAYA YA SIKONGE, 2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 571 LA MWAKA 2015)

40. SHERIA NDOGO ZA (HIFADHI YA MAZINGIRA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA SIKONGE ZA MWAKA 2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 572 LA MWAKA 2015)

41. SHERIA NDOGO ZA (ADA NA USHURU) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA SIKONGE ZA MWAKA 2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 573 LA MWAKA 2015)

42. SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA MADINI YA UJENZI) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA SIKONGE, 2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 574 LA MWAKA 2015)

43. SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA KUEGESHA MAGARI, PIKIPIKI NA BAJAJI STENDI KUU) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA SIKONGE ZA MWAKA 2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 575 LA MWAKA 2015)

44. SHERIA NDOGO ZA (USAFI WA MZINGIRA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA SIKONGE ZA MWAKA 2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 576 LA MWAKA 2015)

45. SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA UOGESHAJI NA UCHINJAJI WA MIFUGO) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA SIKONGE ZA MWAKA 2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA 577 LA MWAKA 2015)

46. SHERIA NDOGO ZA (USURU WA MAZAO NA MISITU) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA SIKONGE ZA MWAKA 2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 578 LA MWAKA 2015)

47. SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA MINADA NA MIFUGO) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA SIKONGE ZA MWAKA 2015. (TANGAZO LA SERIKALI NA. 579 LA MWAKA 2015)

48. SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA VIBAO VYA MATANGAZO YA BIASHARA) HALMASHAURI YA WILAYA YA SIKONGE ZA MWAKA 2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 580 LA MWAKA 2015)

49. SHERIA NDOGO ZA (UTUNZAJI WA BARABARA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA SIKONGE ZA MWAKA 2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 581 LA MWAKA 2015)

50. SHERIA NDOGO ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA GEITA (ADA NA USHURU) (MAREKEBISHO) ZA MWAKA 2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA 582 LA MWAKA 2015)

51. SHERIA NDOGO ZA (AFYA NA USAFI WA MAZINGIRA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA GEITA, 2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 583 LA MWAKA 2015)

52. SHERIA NDOGO ZA (KODI YA HUDUMA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA GEITA ZA MWAKA 2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 584 LA MWAKA 2015)

53. SHERIA NDOGO ZA (KILIMO KWANZA NA USALAMA WA CHAKULA) HALMASHAURI YA WILAYA YA GEITA ZA MWAKA 2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 585 LA MWAKA 2015)

54. KANUNI ZA KUDUMU ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA IRINGA ZA MWAKA 2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 588 LA MWAKA 2015)

55. KANUNI ZA KUDUMU ZA HALMASHAURI YA MJI WA MASASI ZA MWAKA 2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 589 LA MWAKA 2015)

56. SHERIA NDOGO ZA (UANZISHAJI WA BODI YA MFUKO WA ELIMU) ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILALA ZA MWAKA 2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 590 LA MWAKA 2015)

57. SHERIA NDOGO ZA (UENDESHAJI NA USHURU WA SOKO LA SAMAKI FERI, MAGOGONI) ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILALA ZA MWAKA 2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 591 LA MWAKA 2015)

58. SHERIA NDOGO ZA (BIASHARA YA MAZAO YA NGOZI NA ADA ZA MACHINJIO) ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILALA ZA MWAKA 2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 592 LA MWAKA 2015)

59. SHERIA NDOGO ZA (MATUMIZI YA BARABARA) ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA IALA ZA MWAKA 2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 593 LA MWAKA 2015)

60. SHERIA NDOGO ZA (UENDESHAJI WA MASOKO) ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILALA ZA MWAKA 2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 594 LA MWAKA 2015)

61. SHERIA NDOGO ZA (USAFI WA MAZINGIRA) ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILALA ZA MWAKA 2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 595 LA MWAKA 2015)

62. SHERIA NDOGO ZA (HIFADHI YA MAZINGIRA NA RASILIMALI ZA ASILI) ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILALA ZA MWAKA 2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 596 LA MWAKA 2015).

63. SHERIA NDOGO ZA (ADA NA USHURU) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOLO ZA MWAKA KILOLO ZA MWAKA, 2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA.598 LA MWAKA 2015)

64. SHERIA NDOGO ZA (UANZISHAJI WA MFUKO WA FAYA YA JAMII) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA MBONGWE, 2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 599 LA MWAKA 2015)

65. SHERIA NDOGO ZA (KILIMO KWANZA NA USALAMA WA CHAKULA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA MBONGWE, 2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 600 LA MWAKA 2015)

66. SHERIA NDOGO ZA (UVUNAJI WA MAJI YA MVUA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA MBONGWE, 2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 601 LA MWAKA 2015)

67. SHERIA NDOGO ZA (UTUNZAJI WA BARABARA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA MBONGWE, 2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 602 YA MWAKA 2015)

68. SHERIA NDOGO ZA (ADA NA USHURU) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA MBONGWE (TANGAZO LA SERIKALI NA. 603 LA MWAKA 2015)

69. SHERIA NDOGO (HIFADHI,AFYA NA USAFI WA MAZINGIRA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA MBONGWE, 2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 604 LA MWAKA 2015)

70. SHERIA NDOGO ZA (UANZISHAJI WA BODI YA MFUKO WA ELIMU) ZA SERIKALI YA HALMASHAURI YA WILAYA YA MBONGWE,2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 605 LA MWAKA 2015)

71. SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA MADINI YA UJENZI NA CHUMVI) HALMASHAURI YA WILAYA YA UVINZA,2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 606 LA MWAKA 2015)

72. SHERIA NDOGO ZA (USHURU NA HUDUMA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA UVINZA YA MWAKA, 2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 607 LA MWAKA 2015)

73. SHERIA NDOGO ZA (UANZISHAJI WA BODI YA MFUKO WA AFYA YA JAMII) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA UVINZA, 2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 608 LA MWAKA 2015)

74. SHERIA NDOGO ZA (UANZISHAJI WA BODI YA MFUKO WA ELIMU ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA UVINZA,2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 609 LA MWAKA 2015)

75. SHERIA NDOGO ZA (HIFADHI YA MAZINGIRA) YA HALMASHAURI YA WILAYA YA UVINZA ZA MWAKA, 2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 610 LA MWAKA 2015)

76. SHERIA NDOGO ZA (KUIMARISHA AFYA NA USAFI WA MAZINGIRA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA UVINZA ZA MWAKA 2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 611 LA MWAKA 2015)

77. SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA MAEGESHO) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA UVINZA ZA MWAKA 2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 612 LA MWAKA 2015)

78. SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA MAZAO NA VIBANDA SOKONI) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA UVINZA ZA MWAKA 2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 613 LA MWAKA 2015)

79. HATI RASMI YA (UANZISHAJI WA BODI YAHUDUMA ZA AFYA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA MBONGWE, 2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 614 LA MWAKA 2015)

80. KANUNI ZA KUDUMU ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILALA ZA MWAKA 2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA 615 LA MWAKA 2015).

81. SHERIA NDOGO ZA (KODI YA HUDUMA) HALMASHAURI YA WILAYA KILWA, 2016 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 19 LA MWAKA 2016)

82. SHERIA NDOGO ZA (HIFADHI YA MAZINGIRA NA VYANZO VYA MAJI) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA KILWA, 2016 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 20 LA MWAKA 2016)

83. SHERIA NDOGO ZA (UANZISHAJI WA BODI YA MFUKO WA ELIMU) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA KILWA, 2016 (TANGAZO LA SERIKALI LA MWAKA 2016)

84. SHERIA NDOGO ZA (ADA NA USHURU) ZA HLMASHAURI YA WILAYA YA KILWA, 2016 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 22 LA MWAKA 2016)

85. SHERIA NDOGO ZA (ADA NA USHURU) ZA HALMASHAURI ZA WILAYA YA BARIADI, 2016 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 23 LA MWAKA 2016)

86. SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA MAGULIO NA MINADA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA BARIADI, 2016 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 24 LA MWAKA 2016)

87. SHERIA NDOGO ZA (HIFADHI YA MAZINGIRA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA BARIADI, 2016 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 25 LA MWAKA 2016)

88. SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA MAZAO) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA BARIADI, 2016 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 26 LA MWAKA 2016)

89. SHERIA NDOGO ZA (KILIMO NA HIFADHI YA CHAKULA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA BARIADI, 2016 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 27 LA 2016)

90. SHERIA NDOGO ZA (ADA NA USHURU) ZA HALMASHAURI YA WILAYA NGORONGORO, 2016 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 28 LA MWAKA 2016)

91. REGULATION UNDER THE COPYRIGHT AND NEIGHBOURING RIGHTS ACT, 2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 29 OF 2016)

92. KANUNI ZA KUDUMU ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA KILWA, 2016 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 47 LA MWAKA 2016)

93. SHERIA NDOGO ZA (KILIMO KWANZA NA USALAMA WA CHAKULA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA MSALALA ZA MWAKA 2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 1 LA MWAKA 2016)

94. SHERIA NDOGO ZA USHURU WA HUDUMA) ZA HALMASHAURI YA MSALALA ZA MWAKA 2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 2 LA MWAKA 2016)

95. SHERIA NDOGO ZA (UTUNZAJI WA BARABARA) ZA HALMASHAURI ZA WILAYA ZA MSALALA ZA MWAKA 2016 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 3 LA MWAKA 2016)

96. SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA KUSAFIRISHA NA KUPITISHA MIFUGO) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA MSALALA ZA MWAKA 2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 4 LA MWAKA 2016)

97. SHERIA NDOGO ZA (AFYA NA USAFI WA MAZINGIRA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA MSALALA ZA MWAKA 2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 5 LA MWAKA 2016)

98. SHERIA NDOGO ZA (UZALISHAJI WA BODI YA MFUKO WA ELIMU) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA MSALALA ZA MWAKA 2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 6 LA MWAKA 2016)

99. SHERIA NDOGO ZA (HIFADHI YA MAZINGIRA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA MSALALA,2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 7 LA MWAKA 2016)

100. SHERIA NDOGO ZA (UANZISHAJI WA MFUKO WA AFYA YA JAMII) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA MSALALA, 2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 8 LA MWAKA 2016)

101. SHERIA NDOGO ZA (UANZISHAJI WA BODI YA HUDUMA ZA AFYA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA MSALALA, 2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 9 LA MWAKA 2016)

102. SHERIA NDOGO ZA (ADA NA USHURU) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA MSALALA, 2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 10 LA MWAKA 2016)

103. SHERIA NDOGO ZA (KILIMO NA USALAMA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA MOROGORO, 2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 11 LA MWAKA 2016)

104. SHERIA NDOGO ZA (HIFADHI YA MAZINGIRA) ZA HIFADHI YA WILAYA YA MOROGORO, 2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 12 LA MWAKA 2016)

105. SHERIA NDOGO ZA (ADA NA USHURU) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA MOROGORO, 2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 13 LA MWAKA 2016)

106. SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA HUDUMA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA MOROGORO, 2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 14 LA MWAKA 2016)

107. SHERIA NDOGO ZA (AFYA NA USAFI WA MAZINGIRA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA MOROGORO, 2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 15 LA MWAKA 2016)

108. SHERIA YA UTUNZAJI WA BARABARA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA MOROGORO, 2015 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 16 LA MWAKA 2016)

109. SHERIA NDOGO (UANZISHAJI WA MFUKO WA AFYA YA JAMII – TIBA KWA KADI ZA HALMASHAURI YA MANISPAA MOROGORO – MAREKEBISHO YA MWAKA, 2016 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 48 LA MWAKA 2016)

110. SHERIA NDOGO ZA (KODI YA HUDUMA) ZA HALMASHAURI YA MJI WA MASASI, 2016 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 49 LA MWAKA 2016)

111. SHERIA NDOGO ZA (UANZISHAJI WA MFUKO WA AFYA YA JAMII) ZA HALMASHAURI YA MJI WA MASASI ZA MWAKA, 2016 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 50 LA MWAKA 2016)

112. HATI RASMI (UANZISHAJI WA BODI YA HUDUMA ZA AFYA YA HALMASHAURI) HALMASHAURI YA MJI MASASI ZA MWAKA, 2016 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 51 LA MWAKA 2016)

113. KANUNI ZA KUDUMU ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA SHINYANGA ZA MWAKA 2016 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 52 OF 2016)

114. KANUNI ZA KUDUMU ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA BABATI ZA MWAKA, 2016 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 53 OF 2012)

115. KANUNI ZA KUDUMU ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA ILEJE ZA MWAKA 2016 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 54 OF 2016)

116. KANUNI ZA KUDUMU ZABUNGE LA TANZANIA, 2016 (TANGAZO LA SERIKALI NA 56 LA MWAKA 2016)

117. SHERIA NDOGO ZA (HIFADHI YA MAZINGIRA) ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA LINDI ZA MWAKA 2016 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 58 LA MWAKA 2016)

118. SHERIA NDOGO ZA (KODI YA MAJENGO) ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA LINDI ZA MWAKA 2016 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 59 LA MWAKA 2016)

119. SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA MASOKO) ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA LINDI ZA MWAKA 2016 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 60 LA MWAKA 2016)

120. SHERIA NDOGO ZA (ADA YA MAENDELEO YA ELIMU) ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA LINDI YA 2016 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 61 LA MWAKA 2016)

121. KANUNI ZA KUDUMU ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA BUTIAMA ZA MWAKA 2016 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 62 LA MWAKA 2016)

122. KANUNI ZA KUDUMU ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA KIGOMA ZA MWAKA 2016 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 70 LA MWAKA 2016)

123. RULES UNDER THE ENERGY AND WATER UTILITIES REGULATORY AUTHORITY (PETROLEUM PRODUCTS PRICES SETTING) (AMMENDMENT), 2016 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 70 OF 2016).

124. REGULATION UNDER THE TOBACCO INDUSTRY LICENCING (FEES), 2016 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 71 OF 2016).

125. SHERIA NDOGO ZA (UANZISHAJI YA MFUKO WA AFYA YA JAMII) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA IKUNGI ZA MWAKA 2016 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 77 LA 2016)

126. SHERIA NDOGO ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA IKUNGI (ULINZI WA UMMA) ZA MWAKA, 2016 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 78 LA MWAKA 2016)

127. SHERIA NDOGO ZA HATI RASMI YA (UANZISHAJI WA BODI YA HUDUMA ZA AFYA) YA HALMASHAURI YA WILAYA YA IKUNGI, 2016 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 79 LA MWAKA 2016)

128. REGULATIONS AND THE ROAD AND FUELS TOLLS, 2016 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 80 OF 2016)

129. KANUNI ZA KUDUMU ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA KOROGWE, 2016 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 81 LA MWAKA 2016)

130. KANUNI ZA KUDUMU ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA UVINZA, 2016 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 82 LA MWAKA 2016)

131. REGULATIONS UNDER THE PARLIAMENTARY SERVICES (AMMENDMENT), 2016 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 85 OF 2016)

132. REGULATIONS UNDER THE EXAMINATION REGULATIONS, 2016 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 89 OF 2016)

133. KANUNI ZA KUDUMU ZA MIKUTANO NA SHUGHULI ZA HALMASHAURI – HALMASHAURI YA WILAYA YA MSALALA, 2016 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 90 LA MWAKA 2016)

134. RULES UNDER THE LOCAL AUTHORITIES (ELECTIONS) (DESIGNATION OF DISTRICTS COURTS), 2016 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 91 0F 2016)

135. REGULATIONS UNDER THE NON - GOVERNMENTAL ORGANISATION (THE NATIONAL COUNCIL OPERATIONAL), 2016 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 92 OF 2016)

136. KANUNI ZA UCHAGUZI ZA BARAZA LA TAIFA LA MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI, 2016 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 95 LA MWAKA 2016)

137. SHERIA NDOGO ZA (USAFI WA MAZINGIRA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA MERU, 2016 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 96 LA MWAKA, 2016)

138. RULES UNDER THE PETROLEUM (MARINE LOADING AND OFF LOADING OPERATION), 2016 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 98 OF 2016)

139. RULES UNDER THE PETROLEUM (BITUMEN AND PETCOKE OPERATION), 2016 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 99 OF 2016)

140. REGULATIONS UNDER THE CAPITAL MARKETS AND SECURITIES (ESTABLISHMENT OF STOCK EXCHANGE)(AMMENDMENTS), 2016 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 100 OF 2016)

141. REGULATIONS UNDER THE TAX ADMINISTRATION (GENERAL), 2016 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 101 OF 2016).

142. REGULATION UNDER THE COMMISSION FOR AIDS ACT, 2016 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 145 LA MWAKA 2016)

143. REGULATION UNDER THE COMMODITY EXCHANGES ACT,2016 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 146 LA MWAKA 2016)

144. KANUNI ZA KUDUMU ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA SONGEA ZA MWAKA 2016 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 162 LA MWAKA 2016)

145. KANUNI ZA MAHABUSU ZA WATOTO ZA MWAKA 2012 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 163 LA MWAKA 2016)

146. KANUNI ZA UASILI WA WATOTO ZA MWAKA 2012 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 164 LA MWAKA 2016)

147. KANUNI ZA MALEZI YA KAMBO ZA MWAKA 2012 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 165 LA MWAKA 2016)

148. KANUNI ZA MAKAO YA WATOTO ZA MWAKA 2012 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 166 LA MWAKA 2016)

149. KANUNI ZA VITUO VYA KULELEA WATOTO WADOGO MCHANA NA WATOTO WACHANGA ZA MWAKA 2014 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 167 LA MWAKA 2016)

150. KANUNI ZA AJIRA ZA WATOTO ZA MWAKA 2012 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 168 LA MWAKA 2016)

151. KANUNI ZA USALAMA WA WATOTO ZA MWAKA 2014 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 169 LA MWAKA 2016)

152. KANUNI ZA MWENENDO WA MAHAKAMA ZA WATOTO ZA MWAKA 2014 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 170 LA MWAKA 2016)

153. TAFSIRI YA SHERIA ZA TASNIA YA NYAMA (TANGAZO LA SERIKALI NA. 171 LA MWAKA 2016)

154. KANUNI ZA MAFUNZO YA UANAGENZI ZA MWAKA, 2012 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 172 LA MWAKA 2016)

155. REGULATION UNDER THE DRUGS CONTROL AND ENFORCEMENT (GENERAL) 2016 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 173 LA MWAKA 2016)

156. RULES UNDER THE PETROLEUM (RETAIL OPEREATIONS IN TOWNSHIPS AND VILLAGES) 2014 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 174 LA MWAKA 2016)

157. RULES UNDER THE ELECTRICITY (SUPPLY SERVICES) 2014 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 175 LA MWAKA 2016)

158. RULES UNDER WATER SUPPLY AND SANITATION (QUALITY OF SERVICE) 2014 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 176 LA MWAKA 2016)

159. CODE OF CONDUCTS (DISTRICT LAND AND HOUSING TRIBUNALS) 2016 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 177 LA MWAKA 2016)

160. RULES UNDER THE WATER SUPPLY AND SANITATION SERVICE (LICENSING FEES) 2016 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 179 LA MWAKA 2016)

161. THE WORKERS' COMPENSATION REGULATION, 2016 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 185 LA MWAKA 2016)

162. REGULATION UNDER THE ENVIRONMENTAL MANAGEMENT (SOLID WASTE MANAGEMENT) (AMENDEMENT) 2016 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 190 LA MWAKA 2016)

163. REGULATION UNDER THE ENVIRONMENTAL MANAGEMENT (FEE AND CHARGES) (AMENDEMENT) 2016 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 191 LA MWAKA 2016)

164. REGULATION UNDER THE CIVIL AVIATION AUTHORITY (CONTRIBUTION AND ADMINISTRATION OF THE TRAINING FUND) (AMENDMENT) 2016 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 193 LA MWAKA 2016)

165. RULES UNDER THE NGORONGORO CONSERVATION AREA (AMENDMENT) 2016 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 194 LA MWAKA 2016)

166. KANUNI ZA UENDESHAJI WA SHUGHULI ZA SEKRETARIETI YA AJIRA KATIKA UTUMISHI WA UMMA (TANGAZO LA SERIKALI NA. 196 LA MWAKA 2016).

167. REGULATION UNDER THE MERCHANT SHIPPING (VERIFIED GROSS MASS OF A CONTAINER CARRYING CARGO) (TANGAZO LA SERIKALI NA. 197 LA MWAKA 2016).

168. REGULATION UNDER THE SURFACE AND MARINE TRANSPORT REGULATORY AUTHORITY (DRY PORT) 2016 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 198 LA MWAKA 2016).

169. REGULATION UNDER THE BUDGET (AMENDMENT) 2016 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 201 LA MWAKA 2016).

170. REGULATION UNDER THE VALUE ADDED TAX (GENERAL) (AMENDMENT) 2016 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 212 LA MWAKA 2016).

171. REGULATION UNDER THE WORKERS COMPENSATION (PAYMENT OF TARIFF) 2016 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 212A LA MWAKA 2016)

172. RULES UNDER THE ELECTRICITY (DEVELOPMENT OF SMALL POWER PROJECTS) 2016 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 217 LA MWAKA 2016)

173. REGULATION UNDER THE BUDGET (AMENDMENT) 2016 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 220 LA MWAKA 2016)

174. REGULATION UNDER THE CYBERCRIME ACT (TANGAZO LA SERIKALI NA. 224 LA MWAKA 2016).

175. REGULATIONS UNDER THE TOWN PLANERS REGISTRATION (PROFESSIONAL EXAMINATIONS) 2016 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 227 LA MWAKA 2016).

176. REGULATIONS UNDER THE ELECTRONIC TRANSACTIONS (CRYPTOGRAPHIC AND CERTIFICATION SERVICES PROVIDERS) 2016 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 228 LA MWAKA 2016)

177. REGULATION UNDER THE WEIGHTS AND MEASURES (GENERAL) 2016 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 229 LA MWAKA 2016)

178. THE MERCHANT SHIPPING (TRAINING, CERTIFICATION AND MANNING), REGULATION, 2016 (TANGAZO LA SERIKALI NA. 243 LA MWAKA 2016)

179. REGULATION UNDER THE IMMIGRATION (AMENDMENT) (TANGAZO LA SERIKALI NA. 246 LA MWAKA 2016)

180. REGULATION UNDER THE IMMIGRATION (VISA) (TANGAZO LA SERIKALI NA. 247 LA MWAKA 2016)

JEDWALI LA UCHAMBUZI WA SHERIA NDOGO ZILIZOWASILISHWA KATIKA MKUTANO WA PILI HADI WA NNE WA BUNGE

S/N	NAMBA YA TANGAZO LA SERIKALI (GN NUMBER)	JINA LA SHERIA NDOGO (NAME)	SHERIA INAYOTOA MADARAKA (ENABLING PROVISION)	MAMLAKA INAYOHUSIKA	YATOKANAYO NA UCHAMBUZI (OBSERVATIONS)	MAONI NA MAPENDEKEZO (RECOMMENDATIONS)	MAJIBU YA SERIKALI
1.	**GN Na. 508** 6/11/2015	THE PETROLEUM (BULK PROCUREMENT) REGULATIONS, 2015	THE PETROLEUM ACT (No. 21 of 2015) Kifungu 168 na 258	WIZARA YA NISHATI NA MADINI	**1. Kifungu cha 258 (2) (xiv)** cha Sheria Mama kinampa Waziri mamlaka ya kutunga masharti yatakayoainisha njia za upimaji *(measurement methods)* lakini Sheria Ndogo hii **haijaweka wazi** kuwa uingizaji na utoaji utatumia kipimo cha kisasa katika kupima kiasi cha mafuta kudhibiti wizi katika uingizaji wa mafuta na kuongeza mapato kwa TRA badala ya ***deepstic*** kilichokuwa kikitumika awali.	Waziri atoe ufafanuzi	Kifungu cha 258 (2) (xiv) cha Shirika la Petroli ya 2015, kinahusiana na upimaji wa petrol, maji na dutu nyingine *(Other substance)* zinazozalishwa kwenye mkondo wa juu wa petrol *(upstream)* na sio mkondo wa chini *(downstream).* Lakini Kanuni zinazojadiliwa ni za mkondo wa chini ambazo zinahusiana na mafuta safi yanayoagizwa kutoka nje ya nchi. Suala la upimaji linafanywa kitaalamu. PBPA, TRA na EWURA wote wana "surveyors" wao ambao hushiriki katika kujua kiasi cha mafuta kilichoingizwa. *Weight and Measures Agency* (WMA) wanahusika katika kudhibiti upimaji wa mafuta yanayoingizwa nchini. Utaratibu huu huu umezingatiwa na Kanuni katika Kifungu 21(5). Aidha, ili kudhibiti mapato ya Serikali,

S/N	NAMBA YA TANGAZO LA SERIKALI (GN NUMBER)	JINA LA SHERIA NDOGO (NAME)	SHERIA INAYOTOA MADARAKA (ENABLING PROVISION)	MAMLAKA INAYOHUSIKA	YATOKANAYO NA UCHAMBUZI (OBSERVATIONS)	MAONI NA MAPENDEKEZO (RECOMMENDATIONS)	MAJIBU YA SERIKALI
							TRA huchukua kiasi kikubwa kati ya kiasi kinachoonyeshwa kwenye bill of lading na kiasi halisi cha mafuta yaliyofika *(arrival quantity)*.
					2. Kanuni ya 15 (1) inasema "*The Bulk Procurement System for transit petroleum product shall be* ***optional***" na kinakinzana na masharti ya kifungu cha 3 cha tafsiri ambapo mfumo wa BPS unapaswa kuzingatiwa kikamilifu wakati wa uingizaji (importation) mafuta. Kifungu hicho kinaweka masharti ambayo si fungani kwa mafuta yanayoingizwa na kusafirishwa nje ya nchi hivyo kutokuwepo na udhibiti wa wizi. Aidha sharia ndogo ilipaswa kuweka masharti yaliyo bayana kwamba iwapo mtu ataleta mafuta nje ya mfumo wa BPS kwa madhumuni ya kusafirisha nje, hata baada ya kupita kwa siku 30 asiruhusiwe ku-localize)	Kifungu hiki kifutwe/kirekebishwe au Waziri atoe ufafanuzi.	Kifungu cha 15 (1) cha Kanuni kinatoa hiari *(option)* kwa Makampuni ya uuzaji mafuta (OMC) yanayosafirisha mafuta nje ya nchi kutumia mfumo wa ununuaji mafuta kwa pamoja *(Bulk Procurement System) (BPS).* Sheria ya Petroli inamtaka Waziri kuandaa utaratibu wa kuhakikisha kuwa mafuta yote yanayotumika nchini yananunuliwa kwa *"efficient procurement".* Kupitia mamlaka hayo, Waziri ameanzisha utaratibu wa BPS ambao unataka mafuta yote yanayoingizwa kwa matumizi ya ndani nchini yapitie mfumo wa BPS. Aidha, kuhusiana na ku-*localise* Baada ya siku 30 mafuta ambayo yameingizwa kwa mfumo wa BPS kwa

S/N	NAMBA YA TANGAZO LA SERIKALI (GN NUMBER)	JINA LA SHERIA NDOGO (NAME)	SHERIA INAYOTOA MADARAKA (ENABLING PROVISION)	MAMLAKA INAYOHUSIKA	YATOKANAYO NA UCHAMBUZI (OBSERVATIONS)	MAONI NA MAPENDEKEZO (RECOMMENDATIONS)	MAJIBU YA SERIKALI
							madhumuni ya kusafirishwa nje ya nchi haya ni matakwa ya kisheria ambayo yamempa madaraka Kamishna wa Forodha wa TRA kuamuru kuwa mafuta yeyote yaliyoanzishwa kwa madhumuni ya kusafirishwa nje yawe *localize* endapo yatakaa nchini kwa kipindi cha siku 30. Katika ku-*localise* mafuta yaliyoingizwa nje ya mfumo wa BPS katika mazingira ambayo sio shindani kunaweza kutokea *"unfairness"* kwa baadhi ya washiriki. Hivyo, basi suala hili litaendelea kushughulikiwa na taasisi husika ili kuleta usawa wa kibiashara suala hili linapojitokeza.
					3. **Kanuni ya 15 (7)** inaweka masharti **kwamba** Waziri anaweza kuyazuia mafuta ya petroli yanayosafirishwa nje ya nchi ili yatumike ndani ya nchi *(localization of transit petroleum products)* katika mazingira ya dharura *(emergency conditions)* yatakayobainishwa na Waziri. Kifungu hiki kinampa mamlaka makubwa Waziri na endapo yasipotumika vyema	Waziri aweke bayana kwa kuainisha mazingira ambayo yanaweza kumsababisha azuie mafuta kusafirshwa nje ya nchi. Kamati inashauri kuwa	Sheria ya Petroli imempa Waziri dhamana ya kuhakikisha upatikanaji wa mafuta nchini ili kulinda uchumi na kuhakikisha usalama wa nchi. Katika Kifungu cha 5 (2) na Kifungu cha 253 (1) cha Sheria mama ya Petroli

S/N	NAMBA YA TANGAZO LA SERIKALI (GN NUMBER)	JINA LA SHERIA NDOGO (NAME)	SHERIA INAYOTOA MADARAKA (ENABLING PROVISION)	MAMLAKA INAYOHUSIKA	YATOKANAYO NA UCHAMBUZI (OBSERVATIONS)	MAONI NA MAPENDEKEZO (RECOMMENDATIONS)	MAJIBU YA SERIKALI
					yanaweza kuibua migogoro.	Kanuni hiyo kiandikwe kama ifuatavyo:- **"15 (7) Under emergency conditions provided for under Section 253 of the Act, the Minister may localize transit petroleum products after notice has been given to both the licensee and the consignee."**	imempa Waziri wa Nishati mamlaka ya kuamuru mafuta yauzwe nchini. Pia, endapo kutatokea dharula au vita, au kwasababu za kiusalama wan chi, Waziri anaweza kuamuru mafuta yaliyoagizwa kwa ajili ya kusafirishwa kwenda nje ya nchi yauzwe nchini. Hivyo, hata kama Kanuni hazijatamka hali ya dharula ambapo Waziri anaweza kuamuru mafuta yaliyoagizwa kwa ajili ya kuuzwa nje, kuuzwa ndani ya nchi, lakini mazingira hayo tayari yako katika Sheria Mama ambayo ni kama kukiwa na upungufu wa mafta nchini, vita, majanga an au kwasababu za kiusalama wan nchi.
					4. Kanuni ya 19 (2) kinazungumzia muundo wa Kamati ya Zabuni *(Tender Committee)* ambayo pia inaundwa wajumbe wa OMCs na hivyo kuwepo kwa mgongano wa maslahi	Waziri atoe ufafanuzi	Uundwaji wa Bodi ya Zabuni ya Wakala wa Ununuaji wa Mfuta kwa pamoja (PBPA) ulizingati wadau wakuu katika uingizwaji wa mafuta ambao ni OMC na Serikali. Ndio maana ili kuhakikisha kuna uwazi katika mfumo wa BPS, ilikubaliwa kuwa ni budi OMC pia wakawa na

S/N	NAMBA YA TANGAZO LA SERIKALI (GN NUMBER)	JINA LA SHERIA NDOGO (NAME)	SHERIA INAYOTOA MADARAKA (ENABLING PROVISION)	MAMLAKA INAYOHUSIKA	YATOKANAYO NA UCHAMBUZI (OBSERVATIONS)	MAONI NA MAPENDEKEZO (RECOMMENDATIONS)	MAJIBU YA SERIKALI
							uwakilishi wao ndio waagizaji wa mafuta. Hata hivyo, katika uandaaji wa Kanuni, uepushaji wa mgongano wa maslahi ulizingatiwa. Ndio maana kifungu kidogo cha 3 cha Kifungu cha 19 kinatamka wazi kuwa wajumbe wa Bodi ya Zabuni *(pre-qualified suppliers)* au washirika wao hawataruhusiwa kuwa wajumbe wa Bodi ya Zabuni.
					5. Uandishi wa Jedwali la adhabu linalotokana na **Kanuni ya 27** una mapungufu kadhaa yakiwemo kukosekana kwa *proper numbering*, ambayo inaweza kuleta shida katika *citation*. Aidha, adhabu iliyowekwa kwa kosa la "*delay to open LC or to make pre-payment*" ya 20 millions haitaji iwapo ni Shillings au vinginevyo kitu ambacho kinaweza kuleta mkanganyiko wa tafsiri. Aidha adhabu nyingine zinazotolewa katika Jedwali ni kubwa (excessive) na zinapaswa kuwa rafiki kibiashara *(business friendly)*	Jedwali lifanyiwe marekebisho. Aidha, waziri atoe ufafanuzi iwapo kiwango cha faini ya milioni 20 ni kwa Shilingi, adhabu hiyo inaendana na kosa la "*delay to open LC or to make pre-payment*" na adhabu nyingine zilizoainishwa.	Jedwali litafanyiwa marekebisho ya kuliboresha kama ilivyopendekezwa na Waheshimiwa wabunge. Aidha adhabu ya milioni 20 ni ya Shilingi za kitanzania. Adhabu zinaendana na madhara ambayo yanaweza kusababishwa na makosa chini ya Kanuni. Moja ya madhara yanaweza kuwa kutokea kwa upungufu wa mafuta nchini ambapo madhara yake yanaweza kuwa makubwa sana kwa usalama na uchumi wan chi. Pia, makosa kama hayo yanaweza kusababisha hasara kubwa sana.

S/N	NAMBA YA TANGAZO LA SERIKALI (GN NUMBER)	JINA LA SHERIA NDOGO (NAME)	SHERIA INAYOTOA MADARAKA (ENABLING PROVISION)	MAMLAKA INAYOHUSIKA	YATOKANAYO NA UCHAMBUZI (OBSERVATIONS)	MAONI NA MAPENDEKEZO (RECOMMENDATIONS)	MAJIBU YA SERIKALI
							Hivyo, hizi adhabu zimewekwa makusudi ili kuzuia *(deter)* makosa yanayoweza kuleta madhara makubwa kwa nchi.
2.	**GN NA. 509** 6/11/2015	THE EXAMINATION REGULATIONS, 2015	THE NATIONAL EXAMINATION COUNCIL, ACT (CAP. 107)	WIZARA YA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA MAFUNZO YA UFUNDI	**1.** **Kanuni ya 7 (2)** haibainishi hali ya ulemavu *(disability status)* kama suala la muhimu kuonekana katika taarifa za mwanafunzi anayesajiliwa kuanza masomo. Hii ni kwa sababu **Kanuni ya 29 (1)** inaweka sharti la kuzingatia mahitaji ya wanafunzi wenye ulemavu kupatiwa mahitaji muhimu kufanikisha mitihani yao. Hivyo basi kuwekwa kwa hitaji hili katika fomu ya kujisajili itasaidia kutambua idadi ya wanafunzi wenye mahitaji maalum na hitaji la kila mmoja.	Kifungu kifanyiwe marekebisho	Fomu za usajili zinazotumika sasa zinawataka watahiniwa kuonyesha iwapo wana ulemavu na wa aina gani. Ushauri wa Kamati unapokelewa na utafanyiwa kazi kwa kupitia fomu hizo ili kuziboresha. Aidha, Wizara itafanya mapitio ya Kanuni ili kuweka masuala ya watu wenye ulemavu kwa uwazi zaidi.
					2. Uandishi wa **Kanuni ya 4 (2)** na **4 (6) (a)** hauridhishi kwa kuwa kanuni hizo zinataja maneno kama FTNA, CSEE na ACSEE pasipo kuyatolea tafsiri sehemu yeyoyote. Mathalani **Kanuni ya 10 (1)** neno STNA limeonyeshwa na limefafanuliwa kuwa "*Candidate For Standard Two National Assessment".*	Vifungu vifanyiwe marekebisho stahiki	Ushauri wa Kamati kuhusu kufafanua maneno yote yaliyoandikwa kwa ufupi unapokelwa na utafanyiwa kazi.

S/N	NAMBA YA TANGAZO LA SERIKALI (GN NUMBER)	JINA LA SHERIA NDOGO (NAME)	SHERIA INAYOTOA MADARAKA (ENABLING PROVISION)	MAMLAKA INAYOHUSIKA	YATOKANAYO NA UCHAMBUZI (OBSERVATIONS)	MAONI NA MAPENDEKEZO (RECOMMENDATIONS)	MAJIBU YA SERIKALI
					3. **Jedwali la Kwanza (b)** kipengele cha 8 kimeweka ada kubwa ya Shs. 50,000/- kwa Shule ya msingi na 100,000/ kwa shule za Sekondari kwa kupata nakala ya cheti cha masomo, kiwango hiki ni kikubwa hakina uhalisia wa gharama ya utengenezaji kinyume *(unreasonable).* Pia kiwango hiki kinapingana na Mpango wa Elimu Bure.	Waziri wa Elimu atoe ufafanuzi	Maandalizi ya cheti mbadala yanahusisha uhakiki wa taarifa za uhalali wa mwombaji unaofanywa na vyombo vya usalama (Forensic Bureau) pamoja na maandalizi ya gamba la cheti lenye alama mficho (security features) ambavyo vyote vinagharamiwa. Aidha, utaratibu wa kutoa cheti mbadala unatekelezwa kwa angalizo la kutotota mwanya kwa watu wasio waaminifu kufanya kufanya udanganyifu na kuhakikisha anayepewa ni Yule aliyetunukiwa cheti hicho awali. Kwa msingi huo, Wizara inaona kuwa gharama hizo ni sahihi hasa ukizingatia kuwa mchakato wa kuandaa cheti mbadala ni mrefu na wenye gharama kubwa.
					4. **Kanuni za 20, 22** (1) (2), **24**(1), **25, 27** na **28** zinatoa madaraja ya ufaulu kwa mfumo wa GPA ambao kwa mujibu wa Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Mafunzo ya Ufundi mfumo huo hautatumika tena, hivyo uwepo wa Kanuni hizi bado unapelekea uhalali	Waziri wa Elimu atoe ufafanuzi iwapo Kanuni mpya zimetungwa kufuta madaraja hayo.	Kanuni za Mitihani za mwaka 2015 (GN. 509/2015) za tarehe 6/11/2015 zimefutwa kwa Kanuni za Mitihani za Mwaka 2016 zilizotangazwa kwenye Gazeti la Serikali Na. 89 terehe 4/3/2016 kwa jumla zimefuta utaratibu wa

S/N	NAMBA YA TANGAZO LA SERIKALI (GN NUMBER)	JINA LA SHERIA NDOGO (NAME)	SHERIA INAYOTOA MADARAKA (ENABLING PROVISION)	MAMLAKA INAYOHUSIKA	YATOKANAYO NA UCHAMBUZI (OBSERVATIONS)	MAONI NA MAPENDEKEZO (RECOMMENDATIONS)	MAJIBU YA SERIKALI
					wa madaraja hayo kutumika.		kutunuku kwa kutumia mfumo wa GPA na badala yake unatumika Mfumo wa *"Division"*.
3.	**GN Na. 511** 6/11/2015	THE INSTITUTE OF JUDICIAL ADMINISTRATION LUSHOTO (STUDENTS' GENERAL WELFARE, CONDUCT AND DISCIPLINARY MATTERS) REGULATIONS, 2015	THE INSTITUTE OF JUDICIAL ADMINISTRATION LUSHOTO (CAP. 405) KIFUNGU 23	WAZIR WA KATIBA NA SHERIA	**Kanuni ya 13** inatoa adhabu ya mwanafunzi kusimamishwa masomo *(suspension)* endapo atashitakiwa kwa kosa la jinai. Aidha, **Kanuni ya 13 (4)** inaweka sharti kwamba muda wa kusimamishwa kwa mwanafunzi huyo ukizidi miaka miwili mfululizo *(two consecutive academic years)* atakuwa amekoma kuwa mwanafunzi. Sharti hili ni kinyume na haki za msingi za mwanafunzi huyo kwa suala ambalo liko nje ya uwezo wake katika mwenendo wa kesi wa Mahakama.	Waziri atoe ufafanuzi	Tangazo la Serikali Na. 511 linahusu masuala ya usatwi na nidhamu kwa *wanafuzi (student general welfare, conduct and disciplinary matters) Regulations* of 2015 hivyo Kanuni ya 13 inayotajwa ni lazima isomwe pamoja na Tangazo la Serikali Na. 510 linalohusu masuala ya masomo na mitihani *(student Perfomance Assessment), Regulations*, 2015 ambapo Kanuni ya 19 inataka ili mwanafunzi afanye mitihani anapaswa kuwa amehudhuria vipindi vya darasani kwa asilimia 80%. Kama hatahudhuria kwa muda huo hata kama hana kesi ya jinai anaweza kuwa mgonjwa na hivyo chini ya Kanuni ya 37 anaweza kuomba kuahirisha masomo kwa mwaka mmoja na akirudia baada ya mwaka mmojakuendelea alipoishia ili ikizidi miaka miwilianapaswa kuomba

S/N	NAMBA YA TANGAZO LA SERIKALI (GN NUMBER)	JINA LA SHERIA NDOGO (NAME)	SHERIA INAYOTOA MADARAKA (ENABLING PROVISION)	MAMLAKA INAYOHUSIKA	YATOKANAYO NA UCHAMBUZI (OBSERVATIONS)	MAONI NA MAPENDEKEZO (RECOMMENDATIONS)	MAJIBU YA SERIKALI
							kujiunga na kimsingi hawezi kukataliwa ila ni kwa ajili ya kuangalia muda ambao amekuwa nje ya masomo ni vigumu kuwa sambamba na wenzake.
4.	**GN Na. 518** 20/11/2015	SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA MIFUGO) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA BABATI, 2015	SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA (SURA YA 290) Kifungu cha 7 (i) na 16 (i)	OFISI YA RAIS/TAMISEMI	1. Kosa dogo la uchapaji wa vifungu vinavyotoa madaraka. Inapaswa kusomeka Kifungu cha 7 (1) na 16 (1) badala ya Kifungu cha 7 (i) na 16 (i).	Marekebisho yafanyike	Hoja imezingatiwa Halmashauri ya Wilaya ya Babati itaelekezwa kuifanyia marekebisho Sheria Ndogo ya Ushuru wa Mifugo) ili kuondoa makosa ya uchapaji kwa kuweka Vifungu sahihi kama Kamati inavyoshauri.
					2. Masuala yanayozungumziwa na **Jedwali la Pili** yanatofautiana na maudhui ya Sheria Ndogo husika	Marekebisho yafanyike	Halmashauri itaelekezwa kurekebisha Jina la Sheria Ndogo ya Ushuru wa Mifugo ili maudhui yalingane na Jina la Sheria ndogo hiyo.
5.	**GN Na. 520** 20/11/2015	SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA MADINI YA UJENZI NA CHUMVI) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA BABATI, 2015.	SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA SURA 290 KIFUNGU CHA 7 (e), (k) NA (16)	OFISI YA RAIS/TAMISEMI	**Kifungu cha 6** cha Sheria Ndogo hii kinaweka ukomo wa faini wa shilingi 300,000/= kinyume na Sheria Mama (Sura ya 290) inayoweka ukomo wa faini ya Shilingi 50,000/=. Kifungu kinakwenda kinyume na Sheria Mama na kinakiuka Kifungu cha 36 (1) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1 *(Interpretation of Laws Act, CAP 1. R. E. 2002)*	Kifungu kifanyiwe marekebisho	Halmashauri itaelekezwa kurekebisha Sheria Ndogo hiyo kwa kuweka faini isiyozidi shilingi Tshs 50,000/= kama Kamati inavyoshauri

S/N	NAMBA YA TANGAZO LA SERIKALI (GN NUMBER)	JINA LA SHERIA NDOGO (NAME)	SHERIA INAYOTOA MADARAKA (ENABLING PROVISION)	MAMLAKA INAYOHUSIKA	YATOKANAYO NA UCHAMBUZI (OBSERVATIONS)	MAONI NA MAPENDEKEZO (RECOMMENDATIONS)	MAJIBU YA SERIKALI
6.	**GN Na. 521** 20/11/2015	SHERIA NDOGO ZA (KUHIFADHI BARABARA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA BABATI, 2015.	SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA(MAMLAKA ZA WILAYA) (SURA YA 287) Kifungu cha 153	OFISI YA RAIS/TAMISEMI	1. Sheria Ndogo haijaweka "Wajibu wa Halmashauri" kutengeneza njia za kupitisha mifugo na wakati huo inaweka kosa kwa mkazi ambaye atakayepitisha mifugo katika eneo ambalo haliruhusiwi.	Sheria ibainishe wajibu wa Halmashauri kutenga maeneo ya kupitisha mifugo.	Moja ya majukumu ya msingina yakisheria ya Halmashauri ni kutengenezabarabara za halmashauri na kuzihifadhi dhidi ya uharibifu wa aina yoyote ikiwemo upitishaji holela wa mifugo kwenye barabara zake. Halmashauri ina wajibu wakuhakikisha njia na barabara za aina zote katika eneo la Halmashauri zinatengenezwa kupitia mipango na bajeti ya Halmashauri, wajibu ambao umetajwa kwenye kipengele cha 81 cha Jedwali la kwanza *(First schedule)* la Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Sura 290. Kuwepo kwa jukumu hili kwenye Sheria mama hakutoi tena ulazima wa Halmashauri kuonyesha kwenye Sheria Ndogo itafanya nini kuhusu barabara au njia zitakazo tumika kupitishia mifugo.
					2. Uandishi wa **Kifungu cha** 4 una mapungufu kwa kuainisha makosa kwa "mkazi" tu na hivyo kutoa mwanya kwa mtu mwingine yeyote kutenda makosa bila kubanwa na	Sheria Ndogo ifanyiwe marekebisho kwa kuondoa neno "mkazi" badala yake kuwe na neno "mtu	Halmashauri itaelekezwa kufanya marekebisho kwenye Sheria Ndogo ili kupanua wigo wa matumizi ya sheria kwa kuwabana na

S/N	NAMBA YA TANGAZO LA SERIKALI (GN NUMBER)	JINA LA SHERIA NDOGO (NAME)	SHERIA INAYOTOA MADARAKA (ENABLING PROVISION)	MAMLAKA INAYOHUSIKA	YATOKANAYO NA UCHAMBUZI (OBSERVATIONS)	MAONI NA MAPENDEKEZO (RECOMMENDATIONS)	MAJIBU YA SERIKALI
					Sheria Ndogo hiyo. Kifungu hiki pia ni kinyume na masharti ya Katiba kuhusu usawa mbele ya Sheria.	yeyote".	wasio wakazi wa eneo hilo.
					3. **Kifungu cha 11** cha Sheria Ndogo hii kinaweka adhabu ya juu kabisa kwa mujibu wa Sheria *(maximum fine)* ya kulipa faini ya Shilingi 300,000/= kwa kosa la kutupa takataka ya aina yoyote katika eneo la barabara. Bila kuathiri masharti ya Kifungu cha 43 (2) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1 *(Interpretation of Laws Act, CAP 1. R. E. 2002)*, kiwango faini iliyowekwa na Sheria Ndogo hii ni kubwa ukilinganisha na kosa. Aidha haijatoa nafasi kwa Mahakama kuamua adhabu kwa kuzingatia ukubwa wa makosa.	Kifungu kifanyiwe marekebisho.	Halmashauri itaelekezwa kuifanyia marekebisho Sheria Ndogo kama Kamaiti inavypendekeza. Hata hivyo, ni vyema ikaeleweka kwamba, Sheria haizuii Halmashauri kuweka kiwango cha juu cha adhabu kilichowekwa na Sheriana kwamba kuweka kiwango cha shilingi faini ya Shs. 300,000 kwa kosa la kutupa takataka ni kutaka kudhibiti madhara *(deterance)* yatokanayo na uchafuambayo ni makubwa mno kulinganisha na kiwango hiki cha faini kinachotozwa na Halmashauri, kwani Serikali hutumia muda na fedha nyingi kuhudumia wagonjwa hususani wa kipindupindu hivyo ni vyema kudhibiti kwa kuweka adhabu kubwa. Mahakama kwa upande mwingine inao uwezo wa kuamua kumpa adhabu mkosaji chini ya Sheria Ndogo hizi kutegemea na

S/N	NAMBA YA TANGAZO LA SERIKALI (GN NUMBER)	JINA LA SHERIA NDOGO (NAME)	SHERIA INAYOTOA MADARAKA (ENABLING PROVISION)	MAMLAKA INAYOHUSIKA	YATOKANAYO NA UCHAMBUZI (OBSERVATIONS)	MAONI NA MAPENDEKEZO (RECOMMENDATIONS)	MAJIBU YA SERIKALI
							jinsi alivyojitetea.
7.	**GN Na. 529** 20/11/2015	SHERIA NDOGO (BODI YA HUDUMA ZA AFYA) MJI WA KOROGWE	SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA(MAMLAKA ZA MIJI) (SURA YA 288) Kifungu cha 58	OFISI YA RAIS/TAMISEMI	Bila kuathiri uwezo wa wananchi wa halmashauri hii kuchangia, **Kifungu cha 21** kinaweka kiwango cha Sh. 50,000/= ambacho ni kikubwa kwa mwananchi wa kawaida kumudu.	Kifungu kirekebishwe.	Kifungu cha 21 cha GN Na. 529 kinahusu majukumu na Kazi ya Kamati ya Usimamizi wa Hospitali na kifungu hiki hakihusiki na chochote kuhusu kiwango cha malipo. Hoja hiyo itazamwe upya ili iweze kujibiwa.
8.	**GN Na. 556** 11/12/2015	SHERIA NDOGO ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA KOROGWE (USHURU WA MAZAO), 2015	SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA (SURA YA 290) Kifungu cha 7 (1) na 16 (1)	OFISI YA RAIS/TAMISEMI	**Kifungu cha 3 (1)** kinafanya marekebisho kwa **Kifungu cha 3** cha Sheria Ndogo ambapo Halmashauri hii inatoza ushuru wa mazao ya chakula (3%) na ya biashara (5%) ya bei ya soko kutoka katika kila mnunuzi wa mazao. Wakati huo huo, **Kifungu cha 3 (2)** kinaongeza wajibu kwa mkulima/mzalishaji atakayeuza mazao hayo nje ya halmashauri kulipa ushuru wa 5% ya bei ya mauzo kwa mazao yote. Kwa mfanyabiashara anayeishi katika halmashauri ambaye anauza nje ya halmashauri, vifungu hivi vinaweza kuonekana kama analipishwa kodi mara mbili.	Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (TAMISEMI) atoe ufafanuzi.	Marekebisho ya Kifungu cha 3 yalilenga kudhibiti uuzaji holela wa mazao ya chakula nje ya Halmashauri, kwamba endapo Mkulima/Mzalishaji ataamua kuuza mazao ya chakula nje ya Halmashauri basi alipe ushuru wa 5% badala ya 3%. Marekebisho ya Vifungu hivi hayaweki mazingira ya Mkulima/Mzalishaji kutozwa kodi mara mbili,bali yanalengo kuzuia uuzaji wa mazao hayo nje ili kuepusha upungufu wa chakula katika mamlaka husika. Hata hivyo, kwa lengo la kuondoa utata wakati wa utekelezaji wa vifungu hivi, Halmashauri itaelekezwa kuvifanyia marekebisho ili kufafanua zaidi utekelezaji

S/N	NAMBA YA TANGAZO LA SERIKALI (GN NUMBER)	JINA LA SHERIA NDOGO (NAME)	SHERIA INAYOTOA MADARAKA (ENABLING PROVISION)	MAMLAKA INAYOHUSIKA	YATOKANAYO NA UCHAMBUZI (OBSERVATIONS)	MAONI NA MAPENDEKEZO (RECOMMENDATIONS)	MAJIBU YA SERIKALI
							wake. Mfano kwa mkulima/Mzalishaji wa mazao ya chakula aliyelipa ushuru wa 3% akitaka kuuza nje ya Wilaya atalipa tofauti ya 2% tu ili kuepusha kulipishwa mara mbili.
9.	**GN NA. 559** 11/12/2015	SHERIA NDOGO ZA (AFYA NA USAFI WA MAZINGIRA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA KOROGWE, 2015	SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA) (SURA YA 287)	OFISI YA RAIS/TAMISEMI	1. **Kifungu cha 6** kinaweka marufuku ya kupanda mazao au mimea mirefu katika maeneo ya mjini pamoja na maeneo mengine yaliyozuiliwa bila kuainisha aina/jamii ya mimea au mazao hayo. Matumizi ya kifungu hiki yanaweza kuwa na matokeo hasi ya kuzuia utunzaji wa mazingira kinyume na **Kifungu cha 6** cha Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004 upandaji wa miti maeneo ya mjini kwakuwa nayo inaangukia katika kundi la mimea mirefu.	Kifungu kifutwe auWaziri wa Nchi Ofisi ya Rais (**TAMISEMI**) atoe ufafanuzi	Zuio la kupanda mimea mirefu linahusu maeneo ya Mjini kama Sheria Ndogo inavyoeleza. Kwa mujibu wa Kifungu cha 3 cha Sheria Ndogo GN Na. 559, Neno Mazao au mimea mirefu limetafsiriwa kumaanisha:- *"ni mazao au mimea inayozidi sentimita 15 kwenda juu kama vile Mtama, Mihogo, Mahindi, Mbaazi, Uwele na mengine yote yale yanayofanana na hayo"* Hivyo Sheria Ndogo hii haizuii mimea mingine kama vile miti na mingine ya aina hiyo hasa tukizingatia kwamba, umbali kati ya mti mmoja hadi mti mwingine kwa kawaida ni mrefu ukilinganisha na umbali

S/N	NAMBA YA TANGAZO LA SERIKALI (GN NUMBER)	JINA LA SHERIA NDOGO (NAME)	SHERIA INAYOTOA MADARAKA (ENABLING PROVISION)	MAMLAKA INAYOHUSIKA	YATOKANAYO NA UCHAMBUZI (OBSERVATIONS)	MAONI NA MAPENDEKEZO (RECOMMENDATIONS)	MAJIBU YA SERIKALI
							baina ya mazao yaliyotajwa hapo juu na Sheria.
					2. **Kifungu cha 8 (1)** haki kinaweka wajibu wa kila mwananchi kujenga *"Pavement"* mbele ya nyumba yake pasipo kubainisha juu ya umiliki wa hilo eneo atakalopaswa kujenga. Wajibu wa mwananchi kuingia gharama ya kugharamia eneo ambalo si mali yake ni kumbebesha gharama zisizo za lazima.	Kifungu kifutwe au Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (TAMISEMI) atoe ufafanuzi	Sheria Ndogo hii inamlenga zaidi mmiliki wa jengo na hususani kwa majengo ya Mijini. Mpangaji au mtu mwingine yeyote anayeishi kwenye jengo hilohutekeleza kwa niaba ya mmiliki. Hatua ya kuwataka wamiliki wa majengo kutengeneza *pavement* ni kuuweka Mji katika hali ya usafi na pavement hizi hujengwa ndani ya Mita tano kutoka kwenye jengo.
					3. **Kifungu cha 21** kinahusu upimaji wa afya na kina mapungufu yafuatayo:- a) Kinaingilia uhuru wa mtu binafsi kwani kupima afya ni suala la hiyari; b) Hakijaweka bayana kuhusu ada ya upimaji wa afya ya Shilingi 5,000/= inawasilishwa kwa nani. c) Haijatamkwa bayana iwapo wafanyakazi katika sehemu tajwa watachukuliwa hatua gani ikibainika kuwa na magonjwa. Kifungu hiki kinaweza kusababisha ukiukaji wa Sheria ya mahusiano kazini Na. 6 ya 2004 ambayo imekataza	Kifungu kifutwe au Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (TAMISEMI) atoe ufafanuzi	Suala la kupima afya za watoa huduma za vyakula na vinywaji ni la msingi na linahitaji usimamizi thabiti wa Sheria. a) Lengo la Sheria Ndogo hii si kuingilia uhuru wa mtu binafsi bali kuweka wajibu kwa watoa huduma za vyakula na vinywaji kupima afya zao. Lengo ni kuona kama wana magonjwa ya kuambukiza ili watibiwe na kuepusha wasiambukize wateja

S/N	NAMBA YA TANGAZO LA SERIKALI (GN NUMBER)	JINA LA SHERIA NDOGO (NAME)	SHERIA INAYOTOA MADARAKA (ENABLING PROVISION)	MAMLAKA INAYOHUSIKA	YATOKANAYO NA UCHAMBUZI (OBSERVATIONS)	MAONI NA MAPENDEKEZO (RECOMMENDATIONS)	MAJIBU YA SERIKALI
					ubaguzi maeneo ya kazi chini ya **Kifugu cha 7 (4)**. Aidha, **Kifungu cha 17** (1) cha Sheria ya Ukimwi Na. 28 ya 2008 kinawataka waajiri kutunza siri za wajiiriwa wanaoishi na virusi vya ukimwi.		magonjwa. b) Kwa kuwa Sheria Ndogo hii ni mali ya Halmashauri, ada ya upimaji wa afya inapokusanywa huingizwa kwenye akaunti za Halmashauri kama chanzo cha mapato ya Halmashauri kwanikinapaswa kuonyeshwa kwenye bajeti ya Halmashauri, c) Kifungu cha 21 cha Sheria Ndogo hii kinatoa wajibu wa kupima afya ili kujua afya ya Mfanyakazi, Sheria ndogo hii inatoa adhabu kwa atakayekataa au kuacha kupima ili kujua hali yake, na haitoi adhabu kwa atakayebainika na ugonjwa, bali itamsaidia Mfanyakazi KUGUNDUA ugonjwa alionao na hivyo kumshauri kuanza matibabu mapema.Hatua hii itasaidia kuzuia kuenea kwa ugonjwa huo. KUMBUKA: Upimaji huu

S/N	NAMBA YA TANGAZO LA SERIKALI (GN NUMBER)	JINA LA SHERIA NDOGO (NAME)	SHERIA INAYOTOA MADARAKA (ENABLING PROVISION)	MAMLAKA INAYOHUSIKA	YATOKANAYO NA UCHAMBUZI (OBSERVATIONS)	MAONI NA MAPENDEKEZO (RECOMMENDATIONS)	MAJIBU YA SERIKALI
							haufanywi na halmashauri na endapo mfanyakazi atakutwa na ugonjwa ni wajibu wa Mwajiri kumhudumia na sio kumnyayapaa.Na kwa mujibu wa Sera ya Ukimwi mwajiri anapaswa kumpatia mfanyakazi wake mwenye Ukimwi huduma maalum. Hivyo upimaji wa afya ni wa manufaa zaidi kwa mfanyakazi
10.	**GN Na. 564** 18/12/2015	SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA PUMBA ZA MAZAO YA NAFAKA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA SAME, 2015	SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA (SURA YA 290) Kifungu 7 (1) na 16 (1)	OFISI YA RAIS/TAMISEMI	**Kifungu cha 6 (2)** kinaweka adhabu ya juu ya kifungo cha miezi kumi na miwili tofauti na Sheria Mama ambayo inatoa nafasi kwa Mahakama kuamua adhabu ya kifungo jela isiyozidi miezi kumi na miwili kulingana na ukubwa wa kosa.	Kifungu kirekebishwe	Halmashauri itaelekezwa kufanya marekebisho kwenye Sheria Ndogo kama Kamati ilivyoelekeza.
11.	**GN Na. 568** 18/12/2015	SHERIA NDOGO ZA (UANZISHAJI WA MFUKO WA AFYA YA JAMII) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA SIKONGE, 2015	SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA YA WILAYA) (SURA 287) Kifungu cha 153	OFISI YA RAIS/TAMISEMI	**Kifungu cha 23** hakijitoshelezi na kinaweza kuleta shida ya tafsiri kwa sababu hakijaainisha malipo ya Sh. 10,000/= yanatolewa kwa huduma gani.	Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (TAMISEMI) atoe ufafanuzi	Sheria Ndogo hii inawataka wananchi kujiunga na Mfuko wa Afya ya jamii kwa kuchangia Shilingi 10,000/= kila mwaka ili kupata huduma ya matibabu. Kifungu cha 23 kinawahusu wale tu ambao siyo wananchama wa Mfuko wa afya ya Jamii. Kifungu hiki

S/N	NAMBA YA TANGAZO LA SERIKALI (GN NUMBER)	JINA LA SHERIA NDOGO (NAME)	SHERIA INAYOTOA MADARAKA (ENABLING PROVISION)	MAMLAKA INAYOHUSIKA	YATOKANAYO NA UCHAMBUZI (OBSERVATIONS)	MAONI NA MAPENDEKEZO (RECOMMENDATIONS)	MAJIBU YA SERIKALI
							kinamtaka mtu ambaye siyo mwananchama wa Mfuko kila anapokwenda kupata matibabu kwenye Kituo cha kutolea Huduma za Afya alipe malipo ya papo kwa papo ya Shilingi 10,000/= kwa huduma zote atakazopatiwa siku hiyo. Endapo atakuja tena atapaswa kulipa papo kwa papo kiasi kama hicho. Lengo la kifungu hiki ni kuhamasisha wananchi kujiunga na Mfuko wa Bima ya Afya kwa kulipia mara moja tu kwa mwaka kiasi cha shilingi 10,000/= tu kwa mwaka.
12.	**GN Na. 571** 18/12/2015	SHERIA NDOGO ZA (KILIMO NA UHIFADHI WA CHAKULA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA SIKONGE ZA MWAKA 2015	SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA) (SURA YA 287) KIFUNGU CHA 153	OFISI YA RAIS/TAMISEMI	**Kifungu cha 9 (1) (a)** kinaweka kosa la kwa mtu atakayeshindwa kulima mazao ya chakula akiwa anamiliki ardhi ya kilimo. Kitendo cha kumlazimisha mtu matumizi ya ardhi anayoimiliki kinaweza kutafsiriwa kuwa kinakiuka haki za binadamu.	Kifungu kifutwe	Lengo la kifungu hiki cha Sheria Ndogo ni kutoa wajibu kwa wananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge kulima mazao ya chakula ili kuwa naakiba ya kutosha na kudhibiti njaa. Baadhi ya wananchi wenye mashamba wamekuwa wakilima mazao ya biashara tu na kuachana na kilimo cha mazao ya chakula, hali hii imekuwa ikisababisha njaa kwenye baadhi ya

S/N	NAMBA YA TANGAZO LA SERIKALI (GN NUMBER)	JINA LA SHERIA NDOGO (NAME)	SHERIA INAYOTOA MADARAKA (ENABLING PROVISION)	MAMLAKA INAYOHUSIKA	YATOKANAYO NA UCHAMBUZI (OBSERVATIONS)	MAONI NA MAPENDEKEZO (RECOMMENDATIONS)	MAJIBU YA SERIKALI
							maeneo hususan inapotokea zao la biashara mfano tumbaku au pamba inapoathiriwa na magonjwa au bei ya zao hilo inaposhuka.Hali hii husababisha wananchi kukumbwa na uhaba wa chakula na lawama kutupiwa Serikali, hali hii pia imekuwa ikisababisha Serikali kutumia fedha nyingi kuagiza chakula cha msaada kwa wananchi wenye ardhi ambao endapo wangelima pia mazao ya chakula, Serikali isingetumia fedha hizo bali zingetumika kwa shughuli zingine za maendeleo.
13.	**GN NA. 574** 18/12/2015	SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA MADINI YA UJENZI) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA SIKONGE ZA MWAKA 2015	SHERIA YA FEDHA ZA SHERIKALI ZA MITAA (SURA 290) Kifungu cha 7 (1) na 16 (1)	OFISI YA RAIS/TAMISEMI	**Kifungu cha 12** hakijaiwajibisha Halmashauri kwa hasara ambayo wataipata Mnunuzi au Muujazi wa Madini ya ujenzi itasababishwa na Afisa Muidhiniwa kwa uzembe wake au kwa kukusudia wakati wa kukusanya ushuru.	Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (TAMISEMI) atoe ufafanuzi	Halmashauri itaelekezwa kurekebisha kifungu hicho.
14.	**GN Na. 576** 18/12/2015	SHERIA NDOGO ZA (USAFI WA MAZINGIRA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA	SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA)	OFISI YA RAIS/TAMISEMI	1. **Kifungu cha 15** kinaweka adhabu ya juu ya kifungo cha miezi kumi na miwili tofauti na Sheria Mama ambayo inatoa nafasi kwa Mahakama kuamua adhabu ya kifungo jela isiyozidi miezi	Kifungu kirekebishwe au Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (TAMISEMI) atoe ufafanuzi	Halmashauri itaelekezwa kufanya marekebisho ya kifungu hicho iliyaendane na matakwa ya Sheria Mama.

S/N	NAMBA YA TANGAZO LA SERIKALI (GN NUMBER)	JINA LA SHERIA NDOGO (NAME)	SHERIA INAYOTOA MADARAKA (ENABLING PROVISION)	MAMLAKA INAYOHUSIKA	YATOKANAYO NA UCHAMBUZI (OBSERVATIONS)	MAONI NA MAPENDEKEZO (RECOMMENDATIONS)	MAJIBU YA SERIKALI
		SIKONGE ZA MWAKA, 2015.	(SURA YA 287) KIFUNGU CHA 153		kumi na miwili.		
					2. **Kifungu cha 13 (2)** kinamlazimu mtu yeyote ambaye atakiuka Sheria Ndogo hii kukiri kosa hilo kwa kujaza fomu maalum mbele ya Mkurugenzi. Hata hivyo, kifungu cha 158 (2) cha Sheria mama hakijaweka ulazima kwa mkosaji kukiri kosa ila akiamua kufanya hivyo, Mkurugenzi atamtaka kulipa faini pamoja na kujaza fomu ya kukiri kosa/kufifilisha kosa *(compounding of an offence)* ili kuepuka kupelekwa mahakamani.	Kifungu kirekebishwe au Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (TAMISEMI) atoe ufafanuzi	Halmashauri itaelekezwa kufanya marekebisho ya Sheria ndogo hiyo ili kuondoa ulazima wa mkosaji kukiri kosa na kumpa nafasi ya kukiri kwa hiari ndipo ajaze fomu maalum kwa mujibu wa Sheria Ndogo hiyo
15.	**GN Na. 577** 18/12/2015	SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA UOGESHAJI NA UCHANJAJI WA MIFUGO) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA SIKONGE ZA MWAKA, 2015.	SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA) (SURA 290) KIFUNGU 7 (1) na 16 (1)	OFISI YA RAIS/TAMISEMI	1. **Kifungu cha 7** kimeweka kiwango cha Adhabu iliyowekwa ni kubwa kuliko ya Sheria ya Fedha Sura 290. Kwa hiyo Sheria hii ipo kinyume na Sheria Mama.	Kifungu kirekebishwe au Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (TAMISEMI) atoe ufafanuzi	Halmashauri itaelekezwa kufanya marekebisho kwenye Sheria Ndogo hiyo ili kuweka faini inayokubalika kwa mujibu wa Sheria Mama.
					2. **Kifungu cha 3** cha Sheria kina tafsiri ya Neno mnyama ambayo haina wigo mpana,kwa kuondoa aina nyingine za wanyama ilihali wamejitokeza katika sheria,mfano katika jedwali kuna mnyama mbwa ambao si sehemu ya tafsiri ya neno mnyama.	Kifungu kirekebishwe au Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (TAMISEMI) atoe ufafanuzi	Kifungu cha 3 hakina tafsiri ya Neno mnyama bali kinatafsiri neno Mifugo kumaaniasha:-*Ng'ombe, Punda, Mbuzi na Kondoo*. Kutokana na makosa ya kiuchapaji, Halmashauri itaelekezwa kuifanyia marekebisho Sheria Ndogo hiyo ili tafsiri iweze kuhusisha pia Mbwa na Paka wanaotajwa kwenye

S/N	NAMBA YA TANGAZO LA SERIKALI (GN NUMBER)	JINA LA SHERIA NDOGO (NAME)	SHERIA INAYOTOA MADARAKA (ENABLING PROVISION)	MAMLAKA INAYOHUSIKA	YATOKANAYO NA UCHAMBUZI (OBSERVATIONS)	MAONI NA MAPENDEKEZO (RECOMMENDATIONS)	MAJIBU YA SERIKALI
							Jedwali.
					3. Jedwali halijabainisha limetokana na Kifungu gani cha Sheria Ndogo. Kimsingi ilipaswa kuanishwa kuwa linatokana na kifungu cha 4 cha Sheria Ndogo	Jedwali lifanyiwe marekebisho	Halmashauri itaelekezwa kuifanyia marekebisho Sheria Ndogo hii kulingana na Hoja ya Kamati kwa kuweka kifungu kitakachorejea Jedwali la Sheria Ndogo hiyo.
16.	**GN Na. 578** 18/12/2015	SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA MAZAO YA MISITU) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA SIKONGE ZA MWAKA, 2015	SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA (SURA YA 290) KIFUNGU CHA 7 (1) na 16 (1)	OFISI YA RAIS/TAMISEMI	**Kifungu cha 6** kinaweka adhabu ya faini **isiyopungua** Sh. 100,000/= ambayo iko kinyume na masharti ya Sheria Mama ambayo inataka adhabu yoyote faini iwe isiyozidi Sh. 50,000/=. *Ultra Vires.*	Kifungu kirekebishwe au Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (TAMISEMI) atoe ufafanuzi	Halmashauri itaelekezwa kufanya marekebisho ya kifungu hicho ili yaendane na matakwa ya Sheria Mama.
17.	**GN Na.579** 18/12/2015	SHERIA NDOGO ZA(USHURU WA MINADA YA MIFUGO) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA SIKONGE, 2015	SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA(SURA 290) Kifungu 7 (1) na 16 (1)	OFISI YA RAIS/TAMISEMI	Kifungu cha 8 (1) kinaweka adhabu ya faini **isiyopungua** Sh. 50,000/= ambayo iko kinyume na masharti ya Sheria Mama ambayo inataka adhabu yoyote faini iwe isiyozidi Sh. 50,000/=. *Ultra Vires.*	Kifungu kirekebishwe	Halmashauri itaelekezwa kufanya marekebisho ya neon isiyopungua na kuweka neno isiyozidi kama Kamati ilivyoelekza,
18.	**GN Na.580** 18/12/2015	SHERIA NDOGO ZA(USHURU WA VIBAO VYA MATANGAZO YA BIASHARA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA SIKONGE,2015	SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA(SURA 290) Kifungu cha 7(1) na 16(1)	OFISI YA RAIS/TAMISEMI	1. **Kifungu cha 5 (1)** kinaweka sharti kwamba itakuwa ni jukumu la kila mfanyabiashara kuweka kibao cha tangazo kutangaza biashara yake. Sharti hili haliendani na uhalisia wa mambo (unreasonable) kwa sababu si kila mfanyabiashara ana wajibu wa kujitangaza na si kila mfanyabiashara	Kifungu kirekebishwe au Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (TAMISEMI) atoe ufafanuzi	Uwekaji wa mbao za matangazo unalenga kutambulisha biashara ya mfanyabiashara. Lengo la Sheria Ndogo hii nikuhamasisha uwekaji wa mabango ambayo ni chanzo cha mapato ya

S/N	NAMBA YA TANGAZO LA SERIKALI (GN NUMBER)	JINA LA SHERIA NDOGO (NAME)	SHERIA INAYOTOA MADARAKA (ENABLING PROVISION)	MAMLAKA INAYOHUSIKA	YATOKANAYO NA UCHAMBUZI (OBSERVATIONS)	MAONI NA MAPENDEKEZO (RECOMMENDATIONS)	MAJIBU YA SERIKALI
					ana uwezo wa kujitangaza.		Halmashauri.
					2. **Kifungu cha 6 (1)** cha sheria ndogo hii hakija ainisha muda gani unatakiwa utolewe kwenye Taarifa ya Afisa Muidhiniwa ya kumtaka Mfanyabiashara ambaye atashindwa kulipa ada ya vibao vya matangazo, kulipa ada stahiki ndani ya muda maalum kabla Afisa muidhiniwa kuchukua hatua chini ya kifungu kidogo cha (2).	Kifungu kirekebishwe au Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (TAMISEMI) atoe ufafanuzi	Sheria Ndogo imempa Afisa Muidhiniwa kuwa na uwezo wa kumpa muda atakaoona unafaa Mfanyabiashara ambaye ameshindwa kulipa ada ya vibao vya matangazo, kulipa ada stahiki.Ni wajibu wa kila Mtumishi wa Umma kutekeleza wajibu wake bila ya uonevu, upendeleo au kukomoa mtu. Hivyo ni matumaini ya Serikali kuwa Afisa Muidhiniwa atatumia vizuri madaraka hayo kwa lengo la kukusanya mapato kutoka kwa mtu ambaye hajatelekeza wajibu wake kwa hiari. Ni wajibu wa wafanyabiashara kuzingatia Sheria Ndogo zilizopo.
19.	**GN Na. 581** 18/12/2015	SHERIA NDOGO ZA (UTUNZAJI WA BARABARA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA SIKONGE, 2015	SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA) (SURA YA 287) KIFUNGU CHA 153	OFISI YA RAIS/TAMISEMI	**Kifungu cha 5 (b)** hakieleweki nini dhamira yake kutokana na maneno yaliyotumika. “Wanazingatia takataka kwenye maeneo ya barabara”	Kifungu kirekebishwe ili kuleta maana iliyokusudiwa	Hayo ni makosa ya kiuchapaji hivyo, Halmashauri itaelekezwa kuifanyia marekebisho Sheria Ndogo husika ili kuondoa kutoeleweka kwa kifungu hicho.

S/N	NAMBA YA TANGAZO LA SERIKALI (GN NUMBER)	JINA LA SHERIA NDOGO (NAME)	SHERIA INAYOTOA MADARAKA (ENABLING PROVISION)	MAMLAKA INAYOHUSIKA	YATOKANAYO NA UCHAMBUZI (OBSERVATIONS)	MAONI NA MAPENDEKEZO (RECOMMENDATIONS)	MAJIBU YA SERIKALI
20.	**GN Na. 582** 18/12/2015	SHERIA NDOGO ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA GEITA ZA (ADA NA USHURU) (MARAKEBISHO) ZA MWAKA, 2015.	SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA SURA YA 290 KIFUNGU CHA 16 (1) NA 7 (1)	OFISI YA RAIS/TAMISEMI	Sheria Ndogo hii imeidhinishwa/kukubaliwa na Mwenyekiti wa Halmashauri badala ya Waziri Mwenye Dhamana na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Kosa hili linaweza kuwa la kiuchapaji lakini athari yake ni kukosa uhalali wa matumizi yake kwa kutosainiswa/kuidhinishwa na mhusika.	Waziri atoe ufafanuzi	Kwa kuwa Sheria Ndogo haiwezi kuwasilishwa kwa Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali hadi imepata idhini *approval* ya Waziri mwenye Dhamana na Tawala za Mikoa, ni dhahiri kwamba hayo ni makosa ya kiuchapaji hivyo, marekebisho yatafanyika ili Sheria Ndogo hiyo iweze kuonyesha Jina la Waziri aliyeiidhinisha kipindi hicho.
21.	**GN Na. 583** 18/12/2015	SHERIA NDOGO ZA (AFYA NA USAFI WA MAZINGIRA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA GEITA, 2015.	SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA) (SURA YA 287) Kifungu cha 153	OFISI YA RAIS/TAMISEMI	1. **Kifungu cha 6** kinaweka marufuku ya kupanda mazao au mimea mirefu katika maeneo ya mjini pamoja na maeneo mengine yaliyozuiliwa. Sheria ingeainisha aina ya mimea ambayo kupandwa haitaruhusiwa maeneo ya mijini. Aidha, matumizi ya Kifungu hiki kwa upande mwingine yanaweza kuwa na matokeo hasi ya kuzuia suala la utunzaji wa mazingira hasa upandaji wa miti maeneo ya mjini kwakuwa nayo inaangukia katika kundi la mimea mirefu. Hivyo kwenda kinyume na wajibu unaowekwa na Sheria ya Mazingira ambayo chini ya Kifungu cha 6 inaweka wajibu wa wananchi kutunza mazingira, 2004.	Kifungu kirekebishwe au Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (TAMISEMI) atoe ufafanuzi	Zuio la kupanda mimea mirefu linahusu maeneo ya Mjini kama Sheria Ndogo inavyoeleza. Kwa mujibu wa Kifungu cha 3 cha Sheria Ndogo GN Na. 583, Neno Mazao au mimea mirefu limetafsiriwa kumaanisha:- *"ni mazao au mimea inayozidi sentimita 15 kwenda juu kama vile Mtama, Mihogo, Mahindi, Mbaazi, Uwele na mengine yote yale yanayofanana na hayo"* Hivyo, Sheria Ndogo hii haizuii mimea mingine kama

S/N	NAMBA YA TANGAZO LA SERIKALI (GN NUMBER)	JINA LA SHERIA NDOGO (NAME)	SHERIA INAYOTOA MADARAKA (ENABLING PROVISION)	MAMLAKA INAYOHUSIKA	YATOKANAYO NA UCHAMBUZI (OBSERVATIONS)	MAONI NA MAPENDEKEZO (RECOMMENDATIONS)	MAJIBU YA SERIKALI
							vile miti na mingine ya aina hiyo.
					2. **Kifungu cha 8 (1)** haki kinatoa wajibu wa kila mwananchi kujenga "Pavement" mbele ya Nyumba yake pasipo kubainisha juu ya umiliki wa hilo eneo atakalopaswa kujenga. Kifungu kinaweka wajibu wa mwananchi kuingia gharama ya kugharamia eneo ambalo si mali yake hivyo kumbebesha mwananchi mzigo ambao ilipaswa kufanywa na halmashauri yenyewe.	Kifungu kirekebishwe au Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (TAMISEMI) atoe ufafanuzi	Sheria Ndogo hii inamlenga zaidi mmiliki wa jengo na hususani kwa majengo ya Mijini. Mpangaji au mtu mwingine yeyote anayeishi kwenye jengo hilo hutekeleza kwa niaba ya mmiliki. Hatua ya kuwataka wamiliki wa majengo kutengeneza *pavement* ni kuuweka Mji katika hali ya usafi na pavement hizi hujengwa ndani ya Mita tano kutoka kwenye jengo.
					3. **Kifungu cha 21** Kuhusu upimaji wa afya kimegundulika kuwa na masuala yafuatayo:- a) Kifungu hiki kinaingilia uhuru wa mtu binafsi, kwani kupima afya ni suala la hiari. b) Sheria inaelekeza kulipa ada ya upimaji wa afya ya Shilingi 5,000/- pasipo kutaja inalipwa kwa nani. Na pia haielekezi wafanyakazi katika sehemu tajwa wanachukuliwa hatua zipi ikibainika wanaumwa magonjwa Fulani. Ikiwa kama akibainika	Kifungu kirekebishwe au Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (TAMISEMI) atoe ufafanuzi	Suala la kupima afya za watoa huduma za vyakula na vinywaji ni la msingi na linahitaji usimamizi thabiti wa Sheria. Lengo la Sheria Ndogo hii si kuingilia uhuru wa mtu binafsi bali kuweka wajibu kwa watoa huduma za vyakula na vinywaji kupima afya zao ili kujua kama wana magonjwa ya kuambukiza ili watibiwe na kuepuka wasiwaambukize wateja magonjwa hayo.

S/N	NAMBA YA TANGAZO LA SERIKALI (GN NUMBER)	JINA LA SHERIA NDOGO (NAME)	SHERIA INAYOTOA MADARAKA (ENABLING PROVISION)	MAMLAKA INAYOHUSIKA	YATOKANAYO NA UCHAMBUZI (OBSERVATIONS)	MAONI NA MAPENDEKEZO (RECOMMENDATIONS)	MAJIBU YA SERIKALI
					mgojwa Kifungu hiki kinaweza kusababisha ukiukaji wa Sheria ya mahusiano kazini Na. 6 ya 2004 ambayo imekataa ubaguzi maeneo ya kazi chini ya Kifugu cha 7 (4).		Kwa kuwa Sheria Ndogo hii ni mali ya Halmashauri, ada ya upimaji wa afya inapokusanywa huingizwa kwenye akaunti za Halmashauri kama chanzo cha mapato ya Halmashauri kwani kinapaswa kuonyeshwa kwenye bajeti ya Halmashauri, Kifungu cha 21 cha Sheria Ndogo hii kinatoa wajibu wa kupima afya ili kujua afya ya Mfanyakazi, Sheria ndogo hii inatoa adhabu kwa atakayekataa au kuacha kupima ili kujua hali yake, na haitoi adhabu kwa atakayebainika na ugonjwa, bali itamsaidia Mfanyakazi KUGUNDUA ugonjwa alionao na hivyo kumshauri kuanza matibabu mapema. Hatua hii itasaidia kuzuia kuenea kwa ugonjwa huo. KUMBUKA: Upimaji huu haufanywi na halmashauri na endapo mfanyakazi atakutwa na ugonjwa ni wajibu wa Mwajiri kumhudumia na siyo kumnyayapaa. Na kwa mujibu wa Sera ya Ukimwi mwajiri anapaswa kumpatia mfanyakazi wake mwenye

S/N	NAMBA YA TANGAZO LA SERIKALI (GN NUMBER)	JINA LA SHERIA NDOGO (NAME)	SHERIA INAYOTOA MADARAKA (ENABLING PROVISION)	MAMLAKA INAYOHUSIKA	YATOKANAYO NA UCHAMBUZI (OBSERVATIONS)	MAONI NA MAPENDEKEZO (RECOMMENDATIONS)	MAJIBU YA SERIKALI
							Ukimwi huduma maalum. Hivyo upimaji wa afya ni wa manufaa zaidi kwa mfanyakaziMfanyakazi KUGUNDUA ugonjwa alionao na hivyo kumshauri kuanza matibabu mapema. Hatua hii itasaidia kuzuia kuenea kwa ugonjwa huo. KUMBUKA: Upimaji huu haufanywi na halmashauri na endapo mfanyakazi atakutwa na ugonjwa ni wajibu wa Mwajiri kumhudumia na siyo kumnyayapaa. Na kwa mujibu wa Sera ya Ukimwi mwajiri anapaswa kumpatia mfanyakazi wake mwenye Ukimwi huduma maalum. Hivyo upimaji wa afya ni wa manufaa zaidi kwa mfanyakazi
22.	**GN NA. 584** 18/12/2015	SHERIA NDOGO ZA (KODI YA HUDUMA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA GEITA ZA MWAKA 2015	SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA (SURA YA 290) Kifungu cha 7 (1) (Z) na 16(1)	OFISI YA RAIS/TAMISEMI	**Katika kifungu 12 (2) na (3)** kuna mapungufu ya kiuandishi kwa sababu haijawekwa wazi kuwa tathmini ya kodi kwa kila biashara inayotakiwa kulipwa itafanyika vipi. Kwa jinsi kifungu hicho kilivyowekwa kunaweza kutoa mwanya wa rushwa kwamba aidha ili mtu alipe kodi ndogo tofauti na mapato au kuonewa katika kulipa kodi kubwa.	Kifungu kirekebishwe au Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (TAMISEMI) atoe ufafanuzi	Kifungu cha 4(2) cha Sheria Ndogo hizi kinaeleza kiwango cha kodi cha 0.3% kinachopaswa kulipwa na mfanya biashara. Kiwango hicho kinatokana na mahesabu ya shughuli zote zikiwemo za uzalishaji wa bidhaa au utoaji wa huduma ukiondoa ongezeko la

S/N	NAMBA YA TANGAZO LA SERIKALI (GN NUMBER)	JINA LA SHERIA NDOGO (NAME)	SHERIA INAYOTOA MADARAKA (ENABLING PROVISION)	MAMLAKA INAYOHUSIKA	YATOKANAYO NA UCHAMBUZI (OBSERVATIONS)	MAONI NA MAPENDEKEZO (RECOMMENDATIONS)	MAJIBU YA SERIKALI
							thamani yaani VAT. Kifungu cha 12(2) cha Sheria Ndogo hizi kinampa uwezo Afisa Muidhiniwa kupokea au kutopokea mahesabu endapo ataona hesabu hizo siyo sahihi, utekelezaji wa jambo hili unahitaji maadili kama inavyofanyika kwa Watumishi wa TRA. Maudhui ya Kifungu cha 12 cha Sheria Ndogo hizi hayana tatizo bali tatizo litabaki kwa Afisa Muidhiniwa kama ana maadili au laa.
23.	**GN Na. 585** 18/12/2015	SHERIA NDOGO ZA (KILIMO KWANZA NA USALAMA WA CHAKULA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA GEITA ZA MWAKA, 2015	SHERIA YA SERIKALI ZA MTAA (MAMLAKA ZA WILAYA) SURA YA 287 KIFUNGU CHA 153	OFISI YA RAIS/TAMISEMI	**Kifungu cha 16 (d)** cha Sheria Ndogo kinamlazimisha mfugaji kujiunga na vyama vya wafugaji na wajasiriamali. Kifungu hiki kinakinzana na Ibara ya 20 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya ambayo uhuru wa kukutana ni hiari na si lazima.	Kifungu hiki kifutwe kwakuwa kinakiuka Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania	Halmashauri itaelekezwa kuifanyia marekebisho Sheria Ndogo hii ili kuondoa ulazima wa kujiunga na vyama vya wafugaji. Hata hivyo ni vyema wafungaji wakashauriwa na kusisitizwa kujiunga kwanye umoja wao kama sheria ya ushirika inavyosisitiza.
24.	**GN Na.590** 25/12/2015	SHERIA NDOGO ZA(UANZISHWAJI WA BODI YA MFUKO WA ELIMU) ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILALA ZA	SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA(MAMLAKA ZA MIJI) (SURA YA 290) Kifungu cha 89	OFISI YA RAIS/TAMISEMI	1. Sheria haisemi moja kwa moja (Expressly) kwamba kipindi cha ukomo wa ujumbe wa bodi (Kifungu cha 8) kitakua ni miaka 6.	Kifungu kirekebishwe au Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (TAMISEMI) atoe ufafanuzi	Kwa kuwa Bodi za Mifuko ya Elimu katika Mamlaka za serikali za Mitaa ni za Kijamii zaidi, Sheria Ndogo hii haijaweka au kutamka Ukomo wa kuwa mjumbe bali inatoa fursa ya Mjumbe kuchaguliwa tena katika

S/N	NAMBA YA TANGAZO LA SERIKALI (GN NUMBER)	JINA LA SHERIA NDOGO (NAME)	SHERIA INAYOTOA MADARAKA (ENABLING PROVISION)	MAMLAKA INAYOHUSIKA	YATOKANAYO NA UCHAMBUZI (OBSERVATIONS)	MAONI NA MAPENDEKEZO (RECOMMENDATIONS)	MAJIBU YA SERIKALI
		MWAKA,2015					kipindi kingine cha miaka mitatu. Utaratibu huu upo pia kwanafasi ya Ubunge, na Udiwani ambapo Sheria husika hazitoi ukomo bali zinatoafursa kwa mgombea kugombea nafasi hiyo kwa mhula mwingine wa uongozi. Haya pia ni matakwa na haki ya Kikatiba isipokuwa kwa nafasi ya Urais tu.
25.	**GN Na.599** 25/12/2015	SHERIA NDOGO ZA(UANZISHAJI WA MFUKO WA AFYA YA JAMII)ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA MBOGWE,2015	SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA(MAMLAKA ZA WILAYA) (SURA 287) Kifungu 153	OFISI YA RAIS/TAMISEMI	**1.** Sheria ina makosa mengi ya uchapaji ambayo yanaweza kuharibu maana na kuleta mgogoro wa kitafsiri kama kuna suala la namna hiyo linalohitaji tafsiri sahihi ya mahakama. (Kwa mfano Vifungu vya 7(2), 21(1), 26(1), 30(1) na vingine vyenye makosa kama hayo vya uchapaji.	Vifungu vifanyiwe marekebisho	Hayo ni makosa ya uchapaji. Mpiga Chapa Mkuu wa serikali atajulishwa kufanya uchapaji upya wa Sheria Ndogo hii ili kurekebisha kasoro hii.
					2. Adhabu ya miezi 12 ambayo Kifungu cha 44 imetoa ni kubwa sana na inapingana na Sheria mama ambayo inasema kwamba adhabu yeyote iwe ya Sheria ndogo nyingi zilizopitiwa inaonyesha kwamba *''Wording''* ya kifungu hiki cha adhabu inaruhusu adhabu ya namna hii isizidi miezi 12 na haitoi fixed period ya miezi 12. Miezi 12 ni unreasonable na kifungu hiki kinatakiwa kutoa nafasi kwa mahakama kufikiria kutoa adhabu kulingana na uzito wa kosa na mazingira ya kosa husika.	Kifungu vifanyiwe marekebi	Halmashauri itaelekezwa kufanya marekebisho ya Sheria Ndogo hii ili kuweka adhabu ili kuondoa kasoro hizi.

S/N	NAMBA YA TANGAZO LA SERIKALI (GN NUMBER)	JINA LA SHERIA NDOGO (NAME)	SHERIA INAYOTOA MADARAKA (ENABLING PROVISION)	MAMLAKA INAYOHUSIKA	YATOKANAYO NA UCHAMBUZI (OBSERVATIONS)	MAONI NA MAPENDEKEZO (RECOMMENDATIONS)	MAJIBU YA SERIKALI
26.	**GN Na. 600** 25/12/2015	SHERIA NDOGO ZA(KILIMO KWANZA NA USALAMA WA CHAKULA)ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA MBOGWE,2015	SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA(MAMLAKA ZA WILAYA)(SURA 287) Kifungu cha 153	OFISI YA RAIS/TAMISEMI	1. **Kifungu cha 12 (a)** cha Sheria Ndogo kimetaja makosa mbalimbali kwa mmiliki wa ardhi ya kilimo. Baadhi ya makosa haya yanaingilia uhuru wa Kikatiba wa umiliki na utumiaji wa mali kwa mujibu wa Ibara ya 24 ya Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania.	Kifungu kirekebishwe au Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (TAMISEMI) atoe ufafanuzi	Halmashuri itaelekezwa kufanya marekebisho kama ilivyoelekezwa na Kamati.
					2. **Kifungu cha 12 (g)** cha Sheria Ndogo kinakataza kuuza mazao yakiwa shambani. Kifungu hiki Kinakinzana na Ibara ya 23 ya Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo inatambua haki ya kila mtu kupata mapato kulingana na kazi anayofanya.	Kifungu hiki kifutwe.	Halmashauri itaelekezwa kufanya marekebisho kama ilivyoelekezwa na Kamati. Hata hivyo, katazo hili linalenga kumsaidia mkulima asipunjwe kwa kuwa thamani halisi ya mazao yakiwa shambani haifahamiki, na pia mazao yakiuzwa shambani husababisha uhaba wa chakula kwa familia husika.
					3. **Kifungu cha 12 (f)** cha Sheria Ndogo Kinakataza kuuza mazao bila kuweka akiba ya mwaka mzima au zaidi. Kifungu hiki pia kinaingilia uhuru wa kikatiba wa mtu/mkulima kutumia mali yake kwa ajili ya kupata mapato yake ya maisha. Kwa mujibu wa **Ibara ya 22** ya Katiba ya Tanzania kila mtu anayo haki ya kufanya kazi na kuishi katika mapato aliyopata katika hiyo kazi.	Kifungu hiki kifutwe au Waziri atoe ufafanuzi	Kifungu hiki kinalenga kuhimiza familia kuweka akiba ya chakula ili kuepusha familia kukumbwa na baa la njaa. Kifungu hiki hakikusudii kuingilia uhuru wa kikatiba bali kinahimiza familia kutimiza wajibu kuwa na chakula cha kutosha.
27.	**GN NA. 601** LA TAREHE	SHERIA NDOGO ZA (UVUNAJI WA	SHERIA YA FEDHA ZA	OFISI YA	**Kifungu cha 6** kinaipa mamlaka Halmashauri kukataa kutoa kibali cha	Kifungu kifutwe au Waziri wa Nchi Ofisi ya	Halmashauri itaelekezwa kufanya marekebisho

S/N	NAMBA YA TANGAZO LA SERIKALI (GN NUMBER)	JINA LA SHERIA NDOGO (NAME)	SHERIA INAYOTOA MADARAKA (ENABLING PROVISION)	MAMLAKA INAYOHUSIKA	YATOKANAYO NA UCHAMBUZI (OBSERVATIONS)	MAONI NA MAPENDEKEZO (RECOMMENDATIONS)	MAJIBU YA SERIKALI
	25/12/2015	MAJI YA MVUA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA MBONGWE, 2015	SERIKALI ZA MITAA (SURA YA 287) Zimetungwa chini ya Kifungu cha 153	RAIS/TAMISEMI	ujenzi kwa mtu anayetaka kujenga iwapo tu jengo lake halitakuwa na miundo mbinu ya uvunaji maji. Kifungu hiki hakitoi uhuru wa mtu kuamua juu ya chanzo gani angelipenda kutumia katika nyumba yake.	Rais (TAMISEMI) atoe ufafanuzi	kwenye Sheria Ndogo hii ili kutoa uhuru huo. Hata hivyo sheria Ndogo kama hii kwa baadhi ya maeneo husidia kuhamisha Familia kuwa na hifadhi ya maji kutokana na maeneo hayo kuwa na upungufu au ukosefu wa maji ya uhakika.
28.	**GN Na. 606** 25/12/2015	SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA MADINI YA UJENZI NA CHUMVI) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA UVINZA, 2015	SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA (SURA 290) Kifungu cha 7(1) na 16(1)	OFISI YA RAIS/TAMISEMI	**Kifungu cha 7** kinatoa Msamaha wa Ushuru. Aidha, hakiainishi vigezo ambavyo Mkurugenzi wa Halmashauri atavitumia kuruhusu Madini ya Ujenzi kuchimbwa au kusombwa bila kulipiwa Ushuru. Pia kifungu hiki kilitakiwa kisomeke 7 badala 7(1) kwakuwa hakuna kifungu kidogo kingine kinachofuata. Kosa dogo la uchapaji.	Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (TAMISEMI) atoe ufafanuzi	Halmashauri itaelekezwa kurekebisha Sheria Ndogo hii ili kuweka vigezo vya msamaha kama vile madini ya ujenzi kwa ajili ya ujenzi wa shule, zahanati za serikali, au madini yanayotumika kwa ajili ya shughuli za kijamii mfano ujenzi wa baarabara iliyoharibiwa na mafuriko nk.
29.	GN Na. 610 25/12/2015	SHERIA NDOGO ZA (HIFADHI YA MAZINGIRA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA UVINZA ZA MWAKA, 2015	SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA) (SURA YA 287) Kifungu cha 153	OFISI YA RAIS/TAMISEMI	1. Uandishi wa kifungu cha 5 (a) unapaswa kurekebishwa kwa kuweka neno "AU" badala ya "NA" baada ya neno "kulisha" ili kujumuisha makosa yote.	Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (TAMISEMI) ashauriwe	Ushauri huu utazingatiwa kwa kurekebisha kifungu hicho kama kamati ilivyoshauri,
					2. Kifungu cha 6 (5) kinaondoa wajibu wa Halmashauri kulinda na kutunza mifugo/mali za raia kinyume na ibara ya 24 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977	Kifungu kifutwe au Waziri atoe maelezo ya ufafanuzi	Halmashauri itaelekezwa kuifanyia marekebisho Sheria Ndogo kama Kamati ilivyoelekeza.

S/N	NAMBA YA TANGAZO LA SERIKALI (GN NUMBER)	JINA LA SHERIA NDOGO (NAME)	SHERIA INAYOTOA MADARAKA (ENABLING PROVISION)	MAMLAKA INAYOHUSIKA	YATOKANAYO NA UCHAMBUZI (OBSERVATIONS)	MAONI NA MAPENDEKEZO (RECOMMENDATIONS)	MAJIBU YA SERIKALI
30.	**GN Na. 01** 01/1/2016	SHERIA NDOGO ZA (KILIMO KWANZA NA USALAMA WA CHAKULA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA MSALALA, 2015	SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA) (SURA YA 287) KIFUNGU CHA 153	OFISI YA RAIS/TAMISEMI	1. **Kifungu cha 12** cha Sheria Ndogo kimetaja makosa mbalimbali kwa mmiliki wa ardhi ya kilimo. Baadhi ya makosa haya yanaingilia uhuru wa Kikatiba wa umiliki na utumiaji wa mali kwa mujibu wa Ibara ya 24 ya Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania.	Kifungu hiki kifutwe kwakuwa kinakiuka Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania	Halmashauri itaelekezwa kufanya marekebisho kama Kamati ilivyoelekezwa. Kifungu hiki kinalenga kuhimiza familia kuweka akiba ya chakula ili kuepusha familia kukumbwa na baa la njaa. Kifungu hiki hakikusudii kuingilia uhuru wa kikatiba bali kinahimiza familia kutimiza wajibu kuwa na chakula cha kutosha
					2. **Kifungu cha 12 (g)** cha Sheria Ndogo kinakataza kuuza mazao yakiwa shambani. Kifungu hiki Kinakinzana na Ibara ya 23 ya Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo inatambua haki ya kila mtu kupata mapato kulingana na kazi anayofanya.	Kifungu kirekebishwe au Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (TAMISEMI) atoe ufafanuzi	Katazo hili linalenga kumsaidia mkulima asipunjwe kwa kuuza mazao yakiwa shambani kwa kuwa thamani halisi ya mazao yakiwa shambani haifahamiki, na pia mazao yakiuzwa shambani husababisha uhaba wa chakula kwa familia husika
31.	**GN Na. 02** 01/01/2016	SHERIA NDOGO ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA MSALALA (USHURU WA HUDUMA) ZA MWAKA, 2015	SHERIA YA FEDHA YA SERIAKALI ZA MITAA (SURA YA 290) KIFUNGU CHA 16 (1)	OFISI YA RAIS/TAMISEMI	**Kifungu cha 17** kinaweka adhabu ya juu ya kifungo cha miezi kumi na miwili jela tofauti na Sheria Mama ambayo inatoa nafasi kwa Mahakama kuamua adhabu ya kifungo jela isiyozidi miezi kumi na miwili. Kifungu cha 67 cha Sheria Mama ndicho kinachoweka adhabu ya juu kabisa ya kifungo ambacho kisichozidi miezi 12	Kifungu kirekebishwe au Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (TAMISEMI) atoe ufafanuzi	Halmashauri itaelekezwa kuifanyia marekebisho Sheria Ndogo kama Kamati ilivyoelekeza.
32.	**GN Na. 04**	SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA KUSAFIRISHA NA	SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA	OFISI YA RAIS/TAMISEMI	**Kifungu cha 3** kimetafsiri mifugo kwa kutaja kuwa ni ng'ombe, kondoo, mbuzi, punda na nguruwe. Tafsiri ya jinsi hii inaweka	Kifungu kifanyiwe marekebisho ili kupata tafsiri inayojumuisha	Halmashauri itaelekezwa kuifanyia marekebisho Sheria Ndogo kama Kamati

S/N	NAMBA YA TANGAZO LA SERIKALI (GN NUMBER)	JINA LA SHERIA NDOGO (NAME)	SHERIA INAYOTOA MADARAKA (ENABLING PROVISION)	MAMLAKA INAYOHUSIKA	YATOKANAYO NA UCHAMBUZI (OBSERVATIONS)	MAONI NA MAPENDEKEZO (RECOMMENDATIONS)	MAJIBU YA SERIKALI
	01/01/2016	KUPITISHA MIFUGO) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA MSALALA ZA MWAKA, 2015	(SURA YA 290) Kifungu cha 7		mipaka na haijumuishi mifugo mingine inayoweza kufugwa ndani ya halmashauri hiyo. **Sheria ya Mifugo Na. ya 2003** imefafanua mifugo kuwa inajumuisha wanyama mbalimbali kama ifuatavyo:- *"**any** domesticated animal **andincludes** cattle, water buffalo, sheep, goats, pigs, dogs, cats, donkeys, horses, camels, rabbits, guinea pigs and poultry;*	mifugo yote.	ilivyoelekeza.
33.	**GN Na. 05** 01/01/2016	SHERIA NDOGO ZA (AFYA NA USAFI WA MAZINGIRA) HALMASHAURI YA WILAYA YA MSALALA, 2015.	SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA) (SURA YA 287) KIFUNGU CHA 153	OFISI YA RAIS/TAMISEMI	1. **Kifungu cha 6** kinaweka katazo la kupanda mazao au mimea mirefu katika maeneo ya mjini pamoja na maeneo mengine yaliyozuiliwa. Sheria ingeainisha aina ya mimea ambayo kupandwa haitaruhusiwa maeneo ya mijini. Matumizi ya kifungu hiki kwa upande mwingine yanaweza kuwa na matokeo hasi ya kuzuia suala la utunzaji wa mazingira hasa upandaji wa miti maeneo ya mjini kwakuwa nayo inaangukia katika kundi la mimea mirefu. Hivyo kwenda kinyume na wajibu unaowekwa na Sheria ya Mazingira ambayo chini ya Kifungu cha 6 inaweka wajibu wa wananchi kutunza mazingira, 2004.	Kifungu kirekebishwe au Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (TAMISEMI) atoe ufafanuzi	Halmashauri itaelekezwa kuifanyia marekebisho Sheria Ndogo kama Kamati ilivyoelekeza.
					2. **Kifungu cha 8 (1)** haki kinatoa wajibu wa kila mwananchi kujenga "Pavement" mbele ya Nyumba yake pasipo kubainisha juu ya umiliki wa hilo eneo atakalopaswa kujenga. Kifungu kinaweka wajibu wa mwananchi kuingia gharama ya kugharamia eneo ambalo si mali yake hivyo	Kifungu kirekebishwe au Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (TAMISEMI) atoe ufafanuzi	Sheria Ndogo hii inamlenga zaidi mmiliki wa jengo na hususani kwa majengo ya Mijini. Mpangaji au mtu mwingine yeyote anayeishi kwenye jengo hilo hutekeleza kwa niaba ya mmiliki.

S/N	NAMBA YA TANGAZO LA SERIKALI (GN NUMBER)	JINA LA SHERIA NDOGO (NAME)	SHERIA INAYOTOA MADARAKA (ENABLING PROVISION)	MAMLAKA INAYOHUSIKA	YATOKANAYO NA UCHAMBUZI (OBSERVATIONS)	MAONI NA MAPENDEKEZO (RECOMMENDATIONS)	MAJIBU YA SERIKALI
					kumbebesha mwananchi mzigo ambao ilipaswa kufanywa na halmashauri yenyewe.		Hatua ya kuwataka wamiliki wa majengo kutengeneza *pavement* ni kuuweka Mji katika hali ya usafi na pavement hizi hujengwa ndani ya Mita tano kutoka kwenye jengo.
					3. **Kifungu cha 21** Kuhusu upimaji wa afya kimegundulika kuwa na masuala yafuatayo; a) Kifungu kinaingilia uhuru wa mtu binafsi, kwani kupima afya ni suala la hiyari; b) Kifungu kinaweka sharti la kulipa ada ya upimaji wa afya ya Shilingi 5,000/- pasipo kutaja inalipwa kwa nani; c) Kifungu hakiweki bayana kuwa wafanyakazi katika sehemu tajwa watachukuliwa hatua gani ikibainika kuwa wagonjwa. Tahadhari inatolewa kwamba Halmashauri kuhakikisha kuwa hakuna ukiukaji wa Sheria ya mahusiano kazini Na. 6 ya 2004 ambayo imekata ubaguzi maeneo ya kazi chini ya Kifugu cha 7 (4)	Kifungu kirekebishwe au Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (TAMISEMI) atoe ufafanuzi	Suala la kupima afya za watoa huduma za vyakula na vinywaji ni la msingi na linahitaji usimamizi thabiti wa Sheria. a) Lengo la Sheria Ndogo hii si kuingilia uhuru wa mtu binafsi bali kuweka wajibu kwa watoa huduma za vyakula na vinywaji kupima afya zao lengo likiwa ni kubaini kama wanamagonjwa ya kuambukiza ili wasiwaambukize wateja magonjwa hayo. b) Kwa kuwa Sheria Ndogo hii ni mali ya Halmashauri, ada ya upimaji wa afya inapokusanywa huingizwa kwenye akaunti za Halmashauri kama chanzo cha mapato ya Halmashauri

S/N	NAMBA YA TANGAZO LA SERIKALI (GN NUMBER)	JINA LA SHERIA NDOGO (NAME)	SHERIA INAYOTOA MADARAKA (ENABLING PROVISION)	MAMLAKA INAYOHUSIKA	YATOKANAYO NA UCHAMBUZI (OBSERVATIONS)	MAONI NA MAPENDEKEZO (RECOMMENDATIONS)	MAJIBU YA SERIKALI
							kwani kinapaswa kuonyeshwa kwenye bajeti ya Halmashauri, c) Kifungu cha 21 cha Sheria Ndogo hii kinatoa wajibu wa kupima afya ili kujua afya ya Mfanyakazi, Sheria ndogo hii inatoa adhabu kwa atakayekataa au kuacha kupima ili kujua hali yake, na haitoi adhabu kwa atakayebainika na ugonjwa, bali itamsaidia Mfanyakazi KUGUNDUA ugonjwa alionao na hivyo kuanza matibabu mapema. Hatua hii itasaidia kuzuia kuenea kwa ugonjwa huo. KUMBUKA: Upimaji huu haufanywi na halmashauri na endapo mfanyakazi atakutwa na ugonjwa ni wajibu wa Mwajiri kumhudumia na siyo kumnyayapaa. Na kwa mujibu wa Sera ya Ukimwi mwajiri anapaswa kumpatia mfanyakazi wake mwenye Ukimwi huduma maalum. Hivyo

S/N	NAMBA YA TANGAZO LA SERIKALI (GN NUMBER)	JINA LA SHERIA NDOGO (NAME)	SHERIA INAYOTOA MADARAKA (ENABLING PROVISION)	MAMLAKA INAYOHUSIKA	YATOKANAYO NA UCHAMBUZI (OBSERVATIONS)	MAONI NA MAPENDEKEZO (RECOMMENDATIONS)	MAJIBU YA SERIKALI
							upimaji wa afya ni wa manufaa zaidi kwa mfanyakazi
34.	**GN Na. 07** 01/01/2016	SHERIA NDOGO ZA (HIFADHI YA MAZINGIRA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA MSALALA ZA MWAKA, 2015	SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA) (SURA YA 287) Kifungu cha 153	OFISI YA RAIS/TAMISEMI	**Kifungu cha 6 (5)** kinaondoa wajibu wa Halmashauri kulinda na kutunza mifugo/mali za raia kinyume na Ibara ya 24 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977	Kifungu kifutwe	Halmashauri itaelekezwa kufanya marekebisho kwenye Sheria Ndogo ili kufafanua mazingira ya endapo itatokea mifugo kufa ikiwa chini ya ulinzi wake basi Halmashauri isihusike mfano mifugo ikipigwa na radi, au iugue na kufa kwa ugonjwa n.k
35.	**GN Na. 10** 01/01/2016	SHERIA NDOGO ZA (ADA NA USHURU) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA MSALALA, ZA MWAKA 2015.	SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA. (SURA YA 290) KIFUNGU 7 (1) NA 16 (1)	OFISI YA RAIS/TAMISEMI	**Kifungu cha 4 (3) (iv)** kinazungumzia ushuruwa kupima afya, ambapo Jedwali D linataja kiasi cha Tsh. 10,000 kuwa ni ushuru kwa miezi sita. Kifungu hiki kinaingilia uhuru wa mtu binafsi, kwani kupima afya ni suala la hiyari. Sheria Ndogo haijaweka wazi kuwa ada ya upimaji wa afya ya Shilingi 10,000/- inawasilishwa kwa nani. Na pia haielekezi wafanyakazi katika sehemu tajwa wanachukuliwa hatua zipi ikibainika wanaumwa.	Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (TAMISEMI) atoe ufafanuzi	Kifungu cha 4(3) (iv) cha Sheria Ndogo hii kinatoza ushuru wa kupima afya huduma ambayo hulipiwa kwa mujibu wa Sera ya uchangiaji huduma za Afya. Upimaji huu umebainishwa na Halmashauri kama chanzo chake cha mapato na inapaswa kuwekwa kwenye bajeti ya Halmashauri, Ada ya kupia Afya inapaswa pia kuingizwa kwenye bajeti ya Halmashauri kwa hali hiyo, malipo ya ada hiyo huingizwa kwenye akaunti ya Halmashauri.

S/N	NAMBA YA TANGAZO LA SERIKALI (GN NUMBER)	JINA LA SHERIA NDOGO (NAME)	SHERIA INAYOTOA MADARAKA (ENABLING PROVISION)	MAMLAKA INAYOHUSIKA	YATOKANAYO NA UCHAMBUZI (OBSERVATIONS)	MAONI NA MAPENDEKEZO (RECOMMENDATIONS)	MAJIBU YA SERIKALI
							Upimaji wa afya hufanywa na vituo vya kutolea huduma za afya, endapo mfanyakazi atakutwa na ugonjwa ni wajibu wa Mwajiri kumhudumia na siyo kumnyayapa. Hivyo upimaji wa afya ni wa manufaa zaidi kwa mfanyakazi.
36.	**GN Na. 11** 01/01/2016	SHERIA NDOGO ZA (KILIMO NA USALAMA WA CHAKULA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA MOROGORO, 2015	SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA) (SURA YA 287) Kifungu cha 153	OFISI YA RAIS/TAMISEMI	**Kifungu cha 12 (g)** cha Sheria Ndogo kinakataza kuuza mazao yakiwa shambani. Kifungu hiki Kinakinzana na Ibara ya 23 ya Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo inatambua haki ya kila mtu kupata mapato kulingana na kazi anayofanya.	Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (TAMISEMI) atoe ufafanuzi	Halmashauri itaelekezwa kufanya marekebisho kama ilivyoelekezwa na Kamati. Hata hivyo, katazo hili linalenga kumsaidia mkulima asipunjwe kwa kuwa thamani halisi ya mazao yakiwa shambani haifahamiki, na pia mazao yakiuzwa shambani husababisha uhaba wa chakula kwa familia husika.
37.	**GN Na. 12** 1/1/2016	SHERIA NDOGO ZA (HIFADHI YA MAZINGIRA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA	SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA) (SURA YA 287)	OFISI YA RAIS/TAMISEMI	1. Uandishi wa **kifungu cha 5 (a)** unapaswa kurekebishwa kwa kuweka neno "AU" badala ya "NA" baada ya neno "kulisha" ili kujumuisha makosa yote.	Kifungu kirekebishwe	Ushauri huu utazingatiwa kwa kurekebisha kifungu hicho kama Kamati ilivyoshauri

S/N	NAMBA YA TANGAZO LA SERIKALI (GN NUMBER)	JINA LA SHERIA NDOGO (NAME)	SHERIA INAYOTOA MADARAKA (ENABLING PROVISION)	MAMLAKA INAYOHUSIKA	YATOKANAYO NA UCHAMBUZI (OBSERVATIONS)	MAONI NA MAPENDEKEZO (RECOMMENDATIONS)	MAJIBU YA SERIKALI
		MOROGORO, 2015	Kifungu cha 153		2. **Kifungu cha 6 (5)** kinaondoa wajibu wa Halamashauri kulinda na kutunza mifugo/mali za raia kinyume na ibara ya 24 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977.	Kifungu kifutwe	Halmashauri itaelekezwa kuifanyia marekebisho Sheria Ndogo kama Kamati ilivyoelekeza.
38.	**GN Na. 13** 1/1/2016	SHERIA NDOGO ZA (ADA NA USHURU) YA HALMASHAURI YA WILAYA YA MOROGORO, 2015	SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA (SURA YA 290) Kifungu cha 7 (1) na 16 (1)	OFISI YA RAIS/TAMISEMI	1. Kifungu cha 10 kikisomwa pamoja na kifungu cha 9 (4) kinatoa adhabu ya kifungo kisichozidi miezi 12 jela kwa kosa la kushindwa kulipa ada au ushuru. Adhabu hii ni kinyume na kifungu cha 24 (1) cha Sheria Mama kinachoweka adhabu ya kifungo kisichozidi miezi 3 kwa kosa la jinsi hiyo. *Ultra Vires* Kifungu cha 67 cha Sheria Mama kinaweka mashari ya jumla kwamba, iwapo Sheria iko kimya kuhusu adhabu ya kosa fulani, basi adhabu itakayotolewa haipaswi kuzidi kifungo cha miezi 12 jela.	Kifungu kirekebishwe	Halmashauri itaelekezwa kuifanyia marekebisho Sheria Ndogo kama Kamati ilivyoelekeza.
					2. Katika Sehemu "I" ya Jedwali: Ada za maegesho kwa siku ya gari chini ya tani 10 ni TZS 15,000/- kwa siku ambayo ni kubwa kuliko ada ya maegesho kwa siku ya malori zaidi ya tani 10 yanayopaswa kulipa Sh. 2,000/=.	Kifungu kirekebishwe	Halmashauri itaelekezwa kuifanyia marekebisho Sheria Ndogo kama Kamati ilivyoelekeza. Ni makosa ya uchapaji kwa kuwa ililenga kuweka kiwango cha shilingi 1500 badala ya 15,000/=
	GN Na. 14 1/1/2016	SHERIA NDOGO ZA HALMASHAURI YA MOROGORO (USHURU WA HUDUMA) ZA	SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA (SURA YA 290) KIFUNGU CHA 6(1) NA 16(1)	OFISI YA RAIS/TAMISEMI	**Kifungu cha 17** kinaweka adhabu ya juu ya kifungo cha miezi kumi na miwili jela tofauti na Sheria Mama ambayo inatoa nafasi kwa Mahakama kuamua adhabu ya kifungo jela isiyozidi miezi kumi na miwili.	Kifungu kirekebishwe	Halmashauri itaelekezwa kuifanyia marekebisho Sheria Ndogo kama Kamati ilivyoelekeza.

S/N	NAMBA YA TANGAZO LA SERIKALI (GN NUMBER)	JINA LA SHERIA NDOGO (NAME)	SHERIA INAYOTOA MADARAKA (ENABLING PROVISION)	MAMLAKA INAYOHUSIKA	YATOKANAYO NA UCHAMBUZI (OBSERVATIONS)	MAONI NA MAPENDEKEZO (RECOMMENDATIONS)	MAJIBU YA SERIKALI
		MWAKA, 2015					
	GN Na. 15 01/01/2016	SHERIA NDOGO ZA (AFYA NA USAFI WA MAZINGIRA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA MOROGORO, 2015.	SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA(MAMLAKA ZA WILAYA) (SURA YA 287) KIFUNGU CHA 153	OFISI YA RAIS/TAMISEMI	1. **Kifungu cha 6** kinaweka marufuku ya kupanda mazao au mimea mirefu katika maeneo ya mjini pamoja na maeneo mengine yaliyozuiliwa. Sheria ingeainisha aina ya mimea ambayo kupandwa haitaruhusiwa maeneo ya mijini. Matumizi ya kifungu Kifungu hiki kwa upande mwingine yanaweza kuwa na matokeo hasi ya kuzuia suala la utunzaji wa mazingira hasa upandaji wa miti maeneo ya mjini kwakuwa nayo inaangukia katika kundi la mimea mirefu. Hivyo kwenda kinyume na wajibu unaowekwa na Sheria ya Mazingira ambayo chini ya Kifungu cha 6 inaweka wajibu wa wananchi kutunza mazingira, 2004	Kifungu kirekebishwe au Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (TAMISEMI) atoe ufafanuzi	Zuio la kupanda mimea mirefu linahusu maeneo ya Mjini kama Sheria Ndogo inavyoeleza. Kwa mujibu wa Kifungu cha 3 cha Sheria Ndogo GN Na. 15, Neno Mazao au mimea mirefu limetafsiriwa kumaanisha:- *"ni mazao au mimea inayozidi sentimita 15 kwenda juu kama vile Mtama, Mihogo, Mahindi, Mbaazi, Uwele na mengine yote yale yanayofanana na hayo"* Hivyo Sheria Ndogo hii haizuii mimea mingine kama vile miti na mingine ya aina hiyo.

S/N	NAMBA YA TANGAZO LA SERIKALI (GN NUMBER)	JINA LA SHERIA NDOGO (NAME)	SHERIA INAYOTOA MADARAKA (ENABLING PROVISION)	MAMLAKA INAYOHUSIKA	YATOKANAYO NA UCHAMBUZI (OBSERVATIONS)	MAONI NA MAPENDEKEZO (RECOMMENDATIONS)	MAJIBU YA SERIKALI
					2. **Kifungu cha 8 (1)** kinawela masharti kwamba kila mwananchi anatakiwa *"Pavement"* mbele ya Nyumba yake pasipo kubainisha juu ya umiliki wa hilo eneo atakalopaswa kujenga. Kifungu kinaweka wajibu wa mwananchi kuingia gharama ya kugharamia eneo ambalo si mali yake hivyo kumbebesha mwananchi mzigo ambao ilipaswa kufanywa na halmashauri yenyewe.	Kifungu kifutwe au Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (TAMISEMI) atoe ufafanuzi	Sheria Ndogo hii inamlenga zaidi mmiliki wa jengo na hususani kwa majengo ya Mijini. Mpangaji au mtu mwingine yeyote anayeishi kwenye jengo hilo hutekeleza kwa niaba ya mmiliki. Hatua ya kuwataka wamiliki wa majengo kutengeneza *pavement* ni kuuweka Mji katika hali ya usafi na pavement hizi hujengwa ndani ya Mita tano kutoka kwenye jengo.
39.	**GN Na. 19** 08/01/2016	SHERIA NDOGO ZA (KODI YA HUDUMA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA KILWA, 2016	SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA (SURA YA 290) Kifungu cha 7 (2) na 16 (1)	OFISI YA RAIS/TAMISEMI	**1.** Kifungu cha 3 (2) kinaweka masharti kwamba makampuni makubwa ya simu za mkononi na mengineyyo yatalipa kodi ya huduma kwa makubaliano na halmashauri. Ni vyema Sheria Ndogo hii ingeweka kiwango/ukomo wa kodi hiyo bila kutoa mwanya wa majadiliano ambayo yanaweza kushawishi vitendo vya rushwa.	Kifungu kirekebishwe au Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (TAMISEMI) atoe ufafanuzi	Kifungu cha 3(2) cha Sheria Ndogo hiyo kinatoa ufafanuzi wa neno "shughuli za kiuchumi" zilizotajwa kwenye kifungu cha 3(1) cha Sheria Ndogo hiyo, kifungu cha 3(2) hakizungumzii chochote kuhusu majadiliano.
					2. Kifungu cha 13 kinaweka adhabu ya kifungo kisichopungua mwaka mmoja (1) ambayo inakwenda kinyume na Sheria Mama ambayo imeweka kifungo kisichozidi miezi 12. *Ultra Vires*.	Kifungu kifutwe	Halmashauri itaelekezwa kuifanyia marekebisho Sheria Ndogo kama Kamati ilivyoelekeza.
40.	**GN Na. 21**	SHERIA NDOGO ZA (UANZISHAJI	SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLKA ZA	OFISI YA	**Kifungu cha 25 (a)** kinaweka mchango wa asilimia **sio chini** ya tatu (3%) kutoka katika	Kifungu kirekebishwe	Halmashauri itaelekezwa kuifanyia marekebisho Sheria

S/N	NAMBA YA TANGAZO LA SERIKALI (GN NUMBER)	JINA LA SHERIA NDOGO (NAME)	SHERIA INAYOTOA MADARAKA (ENABLING PROVISION)	MAMLAKA INAYOHUSIKA	YATOKANAYO NA UCHAMBUZI (OBSERVATIONS)	MAONI NA MAPENDEKEZO (RECOMMENDATIONS)	MAJIBU YA SERIKALI
	8/1/2016	WA BODI YA MFUKO WA ELIMU) WA HALMASHAURI YA WILAYA YA KILWA, 2016.	WILAYA) (SURA YA 287) KIFUNGU CHA 153	RAIS/TAMISEMI	mapato ya Halmashauri kama moja ya vyanzo vya mapato ya Mfuko wa Elimu. Bila kuathiri uwezo wa halmashauri kuchangia, uandishi wa kifungu hiki unaweka masharti yasiyo na ukomo *(open ended)* ambayo yanaweza kutengeneza mazingira ya upotevu wa fedha za halmashauri.		Ndogo ili mchango unaokusudiwa ueleweke na usiwe na kikomo.
41.	**GN Na. 22** 08/01/2016	SHERIA NDOGO ZA (ADA NA USHURU) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA KILWA, ZA MWAKA 2016	SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA (SURA YA 290) Kifungu cha 7(1) na 16(1)	OFISI YA RAIS/TAMISEMI	1. **Kifungu cha 7** kinaweka adhabu ya juu ya kifungo cha miezi kumi na miwili jela tofauti na inayotolewa chini ya Kifungu 24 na 67 chaSheria Mama (Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa) ambayo inatoa nafasi kwa Mahakama kuamua adhabu ya kifungo jela isiyozidi miezi kumi na miwili.	Kifungu kirekebishwe	Halmashauri itaelekezwa kuifanyia marekebisho Sheria Ndogo kama Kamati ilivyoelekeza.
					2. **Kifungu cha 8** kinampa mamlaka Mkurugenzi kutoza faini isiyozidi Sh. 100,000/= baada kufifilisha kosa. Masharti haya ni kinyume na Sheria Mama ambayo inaweka ukomo wa faini wa Sh. 50,000/= kwa makosa mbalimbali.	Kifungu kirekebishwe	Halmashauri itaelekezwa kuifanyia marekebisho Sheria Ndogo kama Kamati ilivyoelekeza.
42.	GN NA. 24 8/1/2016	SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA MAGULIO NA MINADA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA BARIADI	SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA (SURA 290) (IMETUNGWA CHINI YA KIFUNGU CHA 16 (1))	OFISI YA RAIS/TAMISEMI	**Kifungu cha 11(3)** kinatoa adhabu ya kulipa faini ya shilingi 300,000/- ambayo inakinzana na Sheria Mama (Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa Sura, 290) inayoelekeza faini ya Shilingi 50,000/- chini ya Kifungu cha 24 na 67.	Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (TAMISEMI) atoe ufafanuzi	Halmashauri itaelekezwa kuifanyia marekebisho Sheria Ndogo kama Kamati ilivyoelekeza kwa kuondoa neno isiyopungua shilingi elfu hamsini na kuweka neno isiyozidi shilingi elfu hamsini.

S/N	NAMBA YA TANGAZO LA SERIKALI (GN NUMBER)	JINA LA SHERIA NDOGO (NAME)	SHERIA INAYOTOA MADARAKA (ENABLING PROVISION)	MAMLAKA INAYOHUSIKA	YATOKANAYO NA UCHAMBUZI (OBSERVATIONS)	MAONI NA MAPENDEKEZO (RECOMMENDATIONS)	MAJIBU YA SERIKALI
43.	**GN NA. 25** 8/1/2016	SHERIA NDOGO YA HIFADHI YA MAZINGIRA)YA HALMASHAURI YA WILAYA YA BARIADI ZA MWAKA,2016	SHERIA ZA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA) (SURA YA 287) KIFUNGU CHA 153	OFISI YA RAIS/TAMISEMI	1. Jedwali la Pili limeweka ada ya taka ya Sh. 300,000/= kwa kila kampuni au mtu binafsi anayezalisha/kusambaza takataka. Masharti haya yana mapungufu yafuatayo:- a) Kiasi kilichowekwa hakijabainisha kuwa kitatozwa kwa mwaka au kwa mwezi; b) Kiasi hicho ni kikubwa kwa baadhi ya wazalishaji wa taka hizo, mfano wasambazaji wa magazeti, vocha na maji ya kunywa.	Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (TAMISEMI) atoe ufafanuzi	Halmashauri itaelekezwa kuifanyia marekebisho Sheria Ndogo kama Kamati ilivyoelekeza.
					2. Sheria Ndogo hii haijaonesha mamlaka ya kuidhinishwa na hivyo basi inaweza kukosa uhalali wa kutumika. Kifungu cha 36 (2) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1 kinasema:- *"It shall be presumed, in the absence of evidence to the contrary, that all conditions and pleminary steps precedent to the making of subsidiary legislation have been complied with and perfomed."* Iwapo taratibu zote zilifuatwa, walipaswa kuonesha kuwa halmashauri ilipitisha, Mkurugenzi na Mwenyekiti kuthibitisha na Waziri Mwenye Dhamana kukubali.	Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (TAMISEMI) atoe ufafanuzi	Haya ni makosa ya uchapaji. Maelekezo yatatolewa kwa Mpiga chapa Mkuu wa Serikali ili kurekebisha kwa ukamilifu kasoro hii kwa kuchapisha Sheria Ndogo hii.

S/N	NAMBA YA TANGAZO LA SERIKALI (GN NUMBER)	JINA LA SHERIA NDOGO (NAME)	SHERIA INAYOTOA MADARAKA (ENABLING PROVISION)	MAMLAKA INAYOHUSIKA	YATOKANAYO NA UCHAMBUZI (OBSERVATIONS)	MAONI NA MAPENDEKEZO (RECOMMENDATIONS)	MAJIBU YA SERIKALI
44.	**GN Na. 27** 18/1/2016	SHERIA NDOGO ZA (KILIMO NA HIFADHI YA CHAKULA) ZA HALMASHAURI YA BARIADI ZA MWAKA, 2016	SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA) (SURA YA 287) Kifungu cha 153)	OFISI YA RAIS/TAMISEMI	**Kifungu cha 17(3)** Kinamtaka mfugaji kuhakikisha anapeleka kipato chake katika familia baada ya kuvuna mifugo yake. Kifungu hiki kinakiuka uhuru wa mtu binafsi kwani halmashauri haina mamlaka ya kumpangia mwananchi ni kwa jinsi gani atatumia kipatoe. Kifungu hiki kinakinzana na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 16 inayosema:- *"Kila mtu anastahili kuheshimiwa na kupata hifadhi kwa nafsi yake, maisha yake binafsi na familia yake na unyumba wake, na pia heshima na hifadhi ya maskani yake na mawasiliano yake ya binafsi."*	Kifungu hiki kifutwe kwakuwa kinakiuka Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania	Kwa kuwa Sheria Ndogo hutungwa kulingana na mazingira ya sehemu husika bila kukiuka Katiba au Sheria Mama, lengo la Kifungu cha 17(3) ni kuhakikisha familia za wafugaji zinawajibika kuendeleza familia zao kutokana na mapato yatokanayo na mauzo ya mifugo. Kifungu hiki kwa ujumla hakikusudii kukinzana na Katiba kwani Wafugaji wengi hawajali kusomesha au kuendeleza familia zao.
45.	**GN Na. 28** 8/01/2016	SHERIA NDOGO ZA (ADA NA USHURU) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA NGORONGORO, ZA MWAKA 2016	SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA (SURA YA 290) Kifungu cha 7(1) na 16(1))	OFISI YA RAIS/TAMISEMI	**Kifungu cha 8** kinampa mamlaka Mkurugenzi kutoza faini isiyozidi Sh. 100,000/= baada kufifilisha kosa. Masharti haya ni kinyume na Sheria Mama ambayo inaweka ukomo wa faini wa Sh. 50,000/= kwa makosa mbalimbali.	Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (TAMISEMI) atoe ufafanuzi	Halmashauri itaelekezwa kuifanyia marekebisho Sheria Ndogo kama Kamati ilivyoelekeza.
46.	**GN Na. 29** 8/1/2016	THE COPYRIGHT AND NEIGHBOURING RIGHTS (COPYRIGHTED WORKS - COMMUNICATION TO THE PUBLIC) REGULATIONS, 2016.	THE COPYRIGHT AND NEIGHBOURING RIGHTS ACT (CAP. 218) KIFUNGU CHA 45	WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI	Baada ya Kamati kufanya uchambuzi wake na kusikiliza maoni ya wadau, imebaini kuwa, maandalizi ya Sheria Ndogo hayakufuata taratibu za msingi za utungaji wa Sheria kwa kutowashirikisha wadau kwa ukamilifu.	Waziri atoe ufafanuzi.	Katika utungaji wa Sheria Ndogo hii, Wizara iliwashirikisha wadau ipasavyo.

S/N	NAMBA YA TANGAZO LA SERIKALI (GN NUMBER)	JINA LA SHERIA NDOGO (NAME)	SHERIA INAYOTOA MADARAKA (ENABLING PROVISION)	MAMLAKA INAYOHUSIKA	YATOKANAYO NA UCHAMBUZI (OBSERVATIONS)	MAONI NA MAPENDEKEZO (RECOMMENDATIONS)	MAJIBU YA SERIKALI
47.	**GN NA. 48** 15/01/2016	SHERIA NDOGO (UANZISHAJI WA MFUKO WA AFYA YA JAMII – TIBA KWA KADI ZA HALMASHAURI YA MANISPAA MOROGORO – MAREKEBISHO YA MWAKA, 2016	SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA MIJI) (SURA YA 288) *(Zimetungwa chini ya kifungu cha 89)*	OFISI YA RAIS/TAMISEMI	Sheria hii ilipaswa kuwasilishwa Bungeni katika Bunge la Kumi na Moja Mkutano wa Pili. Kwakuwa Sheria hii haikuwasilishwa chini ya Gazeti la Serikali la tarehe 15 Januari, 2015 Kifungu cha 38 (1) na 38 (2) cha Sheria ya Tafsiri, Sura 1 kama ilivyofanyiwa marejeo mwaka 2002 kinalipa uwezo Bunge wa kuzikataa Sheria zote ambazo zilipaswa kuwasilishwa na hazijawasilishwa Bungeni.	Sheria Ndogo hii inakosa sifa ya kuendelea kutumika. Waziri atoe ufafanuzi.	Uwezo wa Halmashauri kutunga Sheria Ndogo hadi kuanza kutumika umebainishwa kwenye Kifungu cha 90 cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji) Sura 288 na kifungu cha 153 cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya)Sura 287. Kifungu cha 90(5) cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji) Sura 288 kinaeleza Sheria Ndogo itaanza kutumika kwa mara baada ya kuidhinishwa na Waziri na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali. Kifungu hicho kinasema Nanukuu: (*5)upon approval being given by the Minister to any by-law, by-laws or amendment, with or without alteration pursuant to subsection (4), the by-law, by-laws or amendment shall be published in the Gazette, and shall have full force of law within the area of the urban authority from the date of publication or the date of commencement*

S/N	NAMBA YA TANGAZO LA SERIKALI (GN NUMBER)	JINA LA SHERIA NDOGO (NAME)	SHERIA INAYOTOA MADARAKA (ENABLING PROVISION)	MAMLAKA INAYOHUSIKA	YATOKANAYO NA UCHAMBUZI (OBSERVATIONS)	MAONI NA MAPENDEKEZO (RECOMMENDATIONS)	MAJIBU YA SERIKALI
							specified in the by law, by-laws or amendment" Kifungu cha 38(1) na 38(2) cha Sheria ya Tafsiri, Sura 1 kinazungumzia Regulations na sio By-Laws kuwasilishwa Bungeni yaani "laying regulations before tha National Assembly. Kifungu hicho kinasema nnanukuu: *38 (1) All regulations shall be laid before the National Assembly within 6 sitting days of the National Assembly next following publication of the regulations in the Gazette"* Ifahamike kwamba,Sheria Ndogo zinazotungwa na Halmashauri sio *Regulation,* bali ni moja ya *Subsidiary legislation* ambapo Sheria ya Tafsiri, Sura 1 inatafsiri Neno Subsidiary Legislation kama ifuatavyo Nanukuu: *Subsidiary Legislation means any order,proclamation,rule,rule of court, regulation, notice,by-law or instrument made under any Act or other lawful authroirty"*

S/N	NAMBA YA TANGAZO LA SERIKALI (GN NUMBER)	JINA LA SHERIA NDOGO (NAME)	SHERIA INAYOTOA MADARAKA (ENABLING PROVISION)	MAMLAKA INAYOHUSIKA	YATOKANAYO NA UCHAMBUZI (OBSERVATIONS)	MAONI NA MAPENDEKEZO (RECOMMENDATIONS)	MAJIBU YA SERIKALI
							Kutokana na tafsiri hii, endapo Kifungu cha 38(1) na 38(2) cha Sheria ya Tafsiri, Sura 1 kingesema All subsidiary Legislation shall be laid before National Assembly" ni dhahiri Sheria ndogo pamoja na Instrument zinazotengenzwa na Halmashauri pia zingepaswa kuwasilishwa Bungeni kama Kamati inavyoelekekeza. Kwa kuwa Sheria Ndogo siyo *Regulation* na regulation siyo Sheria Ndogo, hivyo basi Sheria Ndogo hii haikupaswa kuwasilishwa kwenye Bunge la Kumi na Moja Mkutano wa Pili hivyoina sifa ya kuendelea kutumika.
48.	**GN NA. 49** 15/01/2016	SHERIA NDOGO ZA (KODI YA HUDUMA) ZA HALMASHAURI YA MJI WA MASASI, 2016.	SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA (SURA YA 290) *Zimetungwa chini ya Vifungu vya 6 (1) na 16 (1).*	OFISI YA RAIS/TAMISEMI	Sheria hii ilipaswa kuwasilishwa Bungeni katika Bunge la Kumi na Moja Mkutano wa Pili. Kwakuwa Sheria hii haikuwasilishwa chini ya Gazeti la Serikali la tarehe 15 Januari, 2015 Kifungu cha 38(1) na 38 (2) cha Sheria ya Tafsiri, Sura 1 kama ilivyofanyiwa marejeo mwaka 2002 kinalipa uwezo Bunge wa kuzikataa Sheria zote ambazo zilipaswa kuwasilishwa na hazijawasilishwa Bungeni.	Sheria Ndogo hii inakosa sifa ya kuendelea kutumika. Waziri atoe ufafanuzi.	Jibu kama lilivyotolewa kwenye hoja kuhusu GN NA. 48 ya 15/01/2016
49.	**GN Na. 50** 15/01/2016	SHERIA NDOGO ZA (UANZISHAJI WA MFUKO WA	SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA	OFISI YA RAIS/TAMISEMI	1. Sheria inamzunguzia Mjumbe wa Bodi pasipo kutoa maana ya Mjumbe.	Wazir atoe ufafanuzi	Sheria Ndogo itafanyiwa marekebisho

S/N	NAMBA YA TANGAZO LA SERIKALI (GN NUMBER)	JINA LA SHERIA NDOGO (NAME)	SHERIA INAYOTOA MADARAKA (ENABLING PROVISION)	MAMLAKA INAYOHUSIKA	YATOKANAYO NA UCHAMBUZI (OBSERVATIONS)	MAONI NA MAPENDEKEZO (RECOMMENDATIONS)	MAJIBU YA SERIKALI
		AFYA YA JAMII) ZA HALMASHAURI YA MJI WA MASASI ZA MWAKA, 2016	MIJI) (SURA YA 288) *Chini ya kifungu cha 58*				
					2. Kifungu cha 9 cha Sheria Ndogo hii kinatoa sifa kadhaa za Mjumbe pasipo kuhusisha sharti la Mjumbe kuwa na akili timamu.	Waziri ashauriwe	Sheria Ndogo itafanyiwa marekebisho
50.	**GN Na. 52** 15/01/2016	KANUNI ZA KUDUMU ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA SHINYANGA ZA MWAKA, 2016	SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA) Kifungu cha 70 (1)	OFISI YA RAIS/TAMISEMI	1. Kanuni ya 67 inayohusu uvunjaji wa Mikataba inapaswa kutamka wazi kwamba, uvunjaji wa Mkataba utazingatia masharti yaliyowekwa katika Sheria ya Mikataba, Sura ya 345 iliyofanyiwa marejeo mwaka 2002.	Waziri ashauriwe	Sheria Ndogo itafanyiwa marekebisho
					2. Kanuni ya 69 imeanisha masuala kadhaa kuhusu Diwani kutokuwa na maslahi binafsi katika Mikataba inayoingiwa na Halmashauri juu utoaji wa huduma mbalimbali. Kanuni imemtaka Diwani kubainisha maslahi yake wazi wazi, lakini haijaweka adhabu au hatua inayopaswa kuchukuliwa pale ambapo Diwani akigundulika kwamba hakuweka wazi maslahi aliyokuwa nayo katika Mkataba Fulani uliongiwa na Halmashauri.	Kifungu kifanyiwe marekebisho	Kifungu kitafanyiwa marekebisho
51.	**GN Na. 53** 15/01/2016	4. KANUNI ZA KUDUMU ZA HALMASHA URI YA WILAYA YA BABATI ZA	SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA) (SURA YA 287)	OFISI YA RAIS/TAMISEMI	1. Kanuni ya 67 inayohusu uvunjaji wa Mikataba inapaswa kutamka wazi kwamba, uvunjaji wa Mkataba utazingatia masharti yaliyowekwa katika sheria ya Mikataba, Sura ya 345 iliyofanyiwa marejeo mwaka 2002.	Waziri ashauriwe kufanya marekebisho	Marekebisho yatafanyika

S/N	NAMBA YA TANGAZO LA SERIKALI (GN NUMBER)	JINA LA SHERIA NDOGO (NAME)	SHERIA INAYOTOA MADARAKA (ENABLING PROVISION)	MAMLAKA INAYOHUSIKA	YATOKANAYO NA UCHAMBUZI (OBSERVATIONS)	MAONI NA MAPENDEKEZO (RECOMMENDATIONS)	MAJIBU YA SERIKALI
		MWAKA, 2016	*Kifungu cha 70 (1)*		2. Kanuni ya 69 imeanisha masuala kadhaa kuhusu Diwani kutokuwa na maslahi binafsi katika Mikataba inayoingiwa na Halmashauri juu utoaji wa huduma mbalimbali. Kanuni imemtaka Diwani kubainisha maslahi yake wazi wazi, lakini haijaweka adhabu au hatua inayopaswa kuchukuliwa pale ambapo Diwani akigundulika kwamba hakuweka wazi maslahi aliyokuwa nayo katika Mkataba Fulani uliongiwa na Halmashauri.	Kifungu kifanyiwe marekebisho	Kifungu kitafanyiwa marekebisho
					3. Kanuni ya 38 (1) haijaweka bayana ni ndani ya kipindi cha muda gani mkazi anapaswa kuwasilisha hoja yake kwa maandishi kabla ya kikao cha Halmashauri kuanza.	Kifungu kifanyiwe marekebisho	Kifungu kitafanyiwa marekebisho
52.	**GN Na. 54** la tarehe 15/1/2016	5. KANUNI ZA KUDUMU ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA ILEJE	SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA) (SURA YA 287) *Zimetungwa chini ya*	OFISI YA RAIS/TAMISEMI	1. Kanuni ya 67 inayohusu uvunjaji wa Mikataba inapaswa kutamka wazi kwamba, uvunjaji wa Mkataba utazingatia masharti yaliyowekwa katika Sheria ya Mikataba, Sura ya 345 iliyofanyiwa marejeo mwaka 2002.	Waziri ashauriwe kufanya marekebisho	Marekebisho yatafanyika

S/N	NAMBA YA TANGAZO LA SERIKALI (GN NUMBER)	JINA LA SHERIA NDOGO (NAME)	SHERIA INAYOTOA MADARAKA (ENABLING PROVISION)	MAMLAKA INAYOHUSIKA	YATOKANAYO NA UCHAMBUZI (OBSERVATIONS)	MAONI NA MAPENDEKEZO (RECOMMENDATIONS)	MAJIBU YA SERIKALI
		6. ZA MWAKA 2016	*kifungu cha 70(1)*		2. Kanuni ya 69 imeanisha masuala kadhaa kuhusu Diwani kutokuwa na maslahi binafsi katika Mikataba inayoingiwa na Halmashauri juu utoaji wa huduma mbalimbali. Kanuni imemtaka Diwani kubainisha maslahi yake wazi wazi, lakini haijaweka adhabu au hatua inayopaswa kuchukuliwa pale ambapo Diwani akigundulika kwamba hakuweka wazi maslahi aliyokuwa nayo katika Mkataba Fulani uliongiwa na Halmashauri.	Kifungu kifanyiwe marekebisho	Kifungu kitafanyiwa marekebisho
53.	**GN Na. 58** 22/01/2016	SHERIA NDOGO ZA (HIFADHI YA MAZINGIRA) ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA LINDI ZA MWAKA 2016	SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA MIJI) (SURA YA 2) *Zimetungwa chini kifungu cha 89*	OFISI YA RAIS/TAMISEMI	1. Kifungu cha 6 (3) hakijaweka ukomo wa muda ambao mwenye mifugo atapaswa kutokea kabla ya mifugo iliyokamatwa kulipiwa faini.	Kifungu kifanyiwe marekebisho kuainisha ukomo wa muda	Kifungu kitafanyiwa marekebisho
					2. Kifungu cha 16 (3) kinatoa marufuku kwa mtu kumiliki eneo la chanzo cha maji. Kifungu hiki kinaweza kuleta utata juu ya kipi ni chanzo cha maji hasa ukizingatia Sheria haijatoa tafsiri ya neno "Chanzo cha Maji."	Kifungu kifanyiwe marekebisho	Kifungu kitafanyiwa marekebisho
					3. Kifungu cha 18 (3) na 18 (4) kimejirudia kama kilivyo.	Kifungu kifutwe	Kifungu kitafutwa
					4. Kifungu cha 28 (2) kimewekwa kwa makosa badala yake kilipaswa kuwa katika kifungu 29.	Waziri ashauriwe kufanya marekebisho	Kifungu kitafanyiwa marekebisho

S/N	NAMBA YA TANGAZO LA SERIKALI (GN NUMBER)	JINA LA SHERIA NDOGO (NAME)	SHERIA INAYOTOA MADARAKA (ENABLING PROVISION)	MAMLAKA INAYOHUSIKA	YATOKANAYO NA UCHAMBUZI (OBSERVATIONS)	MAONI NA MAPENDEKEZO (RECOMMENDATIONS)	MAJIBU YA SERIKALI
54.	**GN NA. 59** 22/01/2016	SHERIA NDOGO ZA (KODI YA MAJENGO) ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA LINDI ZA MWAKA 2016	SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA (SURA YA 290) *Zimetungwa chini ya vifungu 6 na 16 (1)*	OFISI YA RAIS/TAMISEMI	1. Jedwali la Kwanza limeanisha kodi kwa mita za mraba ya kiasi cha Shilingi milioni mbili kwa mwaka inayopaswa kulipwa na mmiliki wa ukumbi wa Sinema. Utozaji wa Kodi hii unaweza kutumika vibaya kwakuwa Sheria haijatafsiri neno Ukumbi wa Sinema, hasa ukizingatia kuna vibanda vidogo vidogo ambavyo navyo huonyesha Sinema kwa kipato kidogo hivyo kimantiki hawataweza kulipa kiwango hiki cha Kodi.	Jedwali lifanyiwe marekebisho	Ushauri umepokelewa
					2. Pia Kodi kwa vituo vya kujazia mafuta, maghala, majengo ya taasisi za Serikali na yasiyo ya Serikali, maeneo ya kuoshea magari haziko halisi kwani ni kubwa kulinganisha na kipato cha biashara husika.	Jedwali lifanyiwe marekebisho	Ushauri umepokelewa
55.	**GN NA. 60** 22/01/2016	SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA MASOKO) ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA LINDI ZA MWAKA 2016	SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA (SURA YA 290) *Kifungu cha 6 (1) na 16 (1)*	OFISI YA RAIS/TAMISEMI	Maudhui ya Kifungu cha 13 cha Sheria hii hayaendani na Lengo la Sheria hii ambalo ni kusimamia Ushuru wa Masoko. Mfano:- a) Kifungu cha 13 (d) kinaweka marufuku ya matumizi ya lugha ya matusi katika eneo la soko kitu ambacho hakina mahusiano na Ushuru wa Masoko. b) Kifungu cha 13 (g) Kinatoa katazo la ukiukwaji wa kanuni za afya ambapo kimsingi jambo hili lilipaswa kuwekwa katika Sheria inayohusika na masuala ya Mazingira au Afya.	Waziri atoe ufafanuzi	Marekebisho yatafanyika

S/N	NAMBA YA TANGAZO LA SERIKALI (GN NUMBER)	JINA LA SHERIA NDOGO (NAME)	SHERIA INAYOTOA MADARAKA (ENABLING PROVISION)	MAMLAKA INAYOHUSIKA	YATOKANAYO NA UCHAMBUZI (OBSERVATIONS)	MAONI NA MAPENDEKEZO (RECOMMENDATIONS)	MAJIBU YA SERIKALI
56.	**GN Na. 62** 22/01/2016	7. KANUNI ZA KUDUMU ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA BUTIAMA ZA MWAKA 2016	SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA YA (SURA YA 287) *Kifungu cha 70(1).*	OFISI YA RAIS/TAMISEMI	1. Kanuni ya 67 inayohusu uvunjaji wa Mikataba inapaswa kutamka wazi kwamba, uvunjaji wa Mkataba utazingatia masharti yaliyowekwa katika Sheria ya Mikataba, Sura ya 345 iliyofanyiwa marejeo mwaka 2002.	Waziri ashauriwe kufanya marekebisho	Marekebisho yatafanyika
					2. **Kanuni ya 13 (1) (c)** jinsi ilivyo andikwa inaweza kutafsiriwa kutoa mwanya kwa mtu yeyote kukaimu nafasi ya Mwenyekiti hata kama si mjumbe. (Baada ya neno kikao kuongezwe maneno…….*kutoka miongoni mwa wajumbe waliohudhuria*)	Kanuni ifanyiwe marekebisho	Kanuni itafanyiwa marekebisho
					3. **Kanuni ya 69** imeanisha masuala kadhaa kuhusu Diwani kutokuwa na maslahi binafsi katika Mikataba inayoingiwa na Halmashauri juu utoaji wa huduma mbalimbali. Kanuni imemtaka Diwani kubainisha maslahi yake wazi wazi, lakini haijaweka adhabu au hatua inayopaswa kuchukuliwa pale ambapo Diwani akigundulika kwamba hakuweka wazi maslahi aliyokuwa nayo katika Mkataba Fulani uliongiwa na Halmashauri.	Kanuni ifanyiwe marekebisho	Kanuni itafanyiwa marekebisho

S/N	NAMBA YA TANGAZO LA SERIKALI (GN NUMBER)	JINA LA SHERIA NDOGO (NAME)	SHERIA INAYOTOA MADARAKA (ENABLING PROVISION)	MAMLAKA INAYOHUSIKA	YATOKANAYO NA UCHAMBUZI (OBSERVATIONS)	MAONI NA MAPENDEKEZO (RECOMMENDATIONS)	MAJIBU YA SERIKALI
57.	**GN Na. 146** 24/04/2016	THE COMMODITY EXCHANGES REGULATIONS, 2016	THE COMMODITY EXCHANGES ACT, 2015 (SURA YA 19) Kifungu 7 (4) na 86	WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO	1. **Kanuni ya 9 (1) (a) (iv)** inaweka masharti ambapo Mamlaka husiku *(The Capital Markets and Security Authority)* inaweza kumnyima leseni mtu yeyote *(natural person)* ambaye mamlaka ina maoni kwamba mtu huyo hana tabia au sifa njema *(no good reputation or character)*. Hata hivyo, Kanuni haijaweka wazi kuwa ni vigezo gani vitatumika kupima tabia na sifa njema za mtu huyo.	Waziri atoe ufafanuzi	Wizara ilikubaliana na Kamati kwamba Kanuni haijaainisha vema kuhusu nini maana ya maneno *"no good reputation or character"*. Kanuni itafanyiwa marekebisho kwa kurejea Sheria nyingine zinazofafanua maneno hayo.
					2. Masharti yaliyomo katika **Kanuni ya 9 (1) (a)** kwa ujumla wake yanakinzana na masharti ya Kifungu cha 7 na 8 cha Sheria Mama ambayo yameweka bayana kuwa maombi ya leseni lazima yafanywe na kampuni iliyosajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Makampuni.	Kanuni ifanyiwe marekebisho	Serikali itafanya marekebisho
58.	**GN Na. 162** 6 Mei, 2016	KANUNI ZA KUDUMU ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA SONGEA ZA MWAKA 2016	SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA MIJI) (SURA YA 288) Chini ya Kifungu cha 42(1)	OFISI YA RAIS (TAMISEMI)	1. **Kanuni ya 28** inazungumzia mazingira ambapo Mjumbe anaweza kuadhibiwa kwa kutoa kauli zenye kashfa dhidi ya mtu yeyote. Hata hivyo, Kanuni hii haijaweka wazi kuwa kauli zenye kashfa ni zipi. Aidha, adhabu inayotolewa na kanuni hii, inakiuka misingi ya kisheria kwa kumuondolea Mjumbe **HAKI ZOTE** ikiwa na pamoja na kinga, posho na upendeleo. Vilevile katika kanuni 28 (2) kuna maneno **Meya wa Mkutano** ambaye	Kanuni ifanyiwe marekebisho	Halmashauri ya Manispaa ya Songea imeelekezwa kwa barua Kumb. Na. CHB.42/332/05/17 ya tarehe 26/10/2016 kuifanyia marekebisho Kanuni ya Kudumu na 28 ya GN Na. 162 kwa kutoa tafsiri ya neno "kauli za kashfa" ili kuweka bayana kauli zinazoweza kuchukuliwa kuwa ni kauli zenye kashfa ambazo zinakatazwa. Halmashauri imeelekezwa

S/N	NAMBA YA TANGAZO LA SERIKALI (GN NUMBER)	JINA LA SHERIA NDOGO (NAME)	SHERIA INAYOTOA MADARAKA (ENABLING PROVISION)	MAMLAKA INAYOHUSIKA	YATOKANAYO NA UCHAMBUZI (OBSERVATIONS)	MAONI NA MAPENDEKEZO (RECOMMENDATIONS)	MAJIBU YA SERIKALI
					hajatolewa tafsiri katika Sheria yoyote.		kufanya marekebisho ya Kanuni hii kuondoa maneno "upendeleo na kinga" yanayosomeka katika Kanuni ya 28 (3) ili kumpa Mjumbe haki ya kuwa na kinga. Halmashauri imeelekezwa kuifanyia marekebisho Kanuni ya 28 (2) kwa kufuta neno "Meya" linalosomeka katika Kanuni Ndogo hiyo na badala yake kuweka neno "Mwenyekiti".

S/N	NAMBA YA TANGAZO LA SERIKALI (GN NUMBER)	JINA LA SHERIA NDOGO (NAME)	SHERIA INAYOTOA MADARAKA (ENABLING PROVISION)	MAMLAKA INAYOHUSIKA	YATOKANAYO NA UCHAMBUZI (OBSERVATIONS)	MAONI NA MAPENDEKEZO (RECOMMENDATIONS)	MAJIBU YA SERIKALI
					2. **Kanuni ya 70 (1)** imeanisha masuala kadhaa kuhusu Diwani kutokuwa na maslahi binafsi katika Mikataba inayoingiwa na Halmashauri juu utoaji wa huduma mbalimbali. Kanuni imemtaka Diwani kubainisha maslahi yake wazi wazi, lakini haijaweka adhabu au hatua inayopaswa kuchukuliwa pale ambapo Diwani akigundulika kwamba hakuweka wazi maslahi aliyokuwa nayo katika Mkataba Fulani uliongiwa na Halmashauri.	Kanuni ifanyiwe marekebisho	Halmashauri imeelekezwa kufanya marekebisho kwa Kanuni ya 70 (1) kwa kuongeza Kanuni ndogo ya (9) kama inavyosomeka kwenye Kanuni za Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji) Mitaa (Mamlaka za Miji) (Maadili ya Madiwani) GN. Na. 281 ya mwaka 2000. Kitasomeka kama ifuatavyo *"70(9) Diwani au mtu yeyote atakayekiuka vipengele vya Kanuni hizi atakuwa ametenda kosa chini ya Kifungu cha 65 (4) cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji) Sura 288 Toleo la 2002 na anaweza kuchukuliwa hatua kwa m,ujibu wa Kifungu cha 96 cha Kanuni za adhabu.*
					3. **Kanuni ya 75 (2)** kwa kuwa Halmashauri imepewa mamlaka ya kutunga Sheria endapo hakuna malalamiko na pingamizi zilizotolewa, maneno "**ikizingatia malalamiko na pingamizi zilizotolewa**" yanapaswa kufutwa.	Kanuni ifanyiwe marekebisho	Halmashauri imeelekezwa kufanyia marekebisho Kanuni ya 75(2) kwa kufuta maneno "ikizingatia malalamiko na pingamizi zilizotolewa" yanayosomeka kwenye Kanuni hiyo.

S/N	NAMBA YA TANGAZO LA SERIKALI (GN NUMBER)	JINA LA SHERIA NDOGO (NAME)	SHERIA INAYOTOA MADARAKA (ENABLING PROVISION)	MAMLAKA INAYOHUSIKA	YATOKANAYO NA UCHAMBUZI (OBSERVATIONS)	MAONI NA MAPENDEKEZO (RECOMMENDATIONS)	MAJIBU YA SERIKALI
					4. **Kanuni ya 76 (1)** inampa Mjumbe haki ya kupata waraka wowote uliojadiliwa na Kamati ya Halmashauri. Hata hivyo, Kanuni inaweka masharti ya upatikanaji wa waraka huo "**kama nakala zitapatikana**". Masharti haya yanakinzana na maudhui ya upatikanaji wa taarifa.	Kanuni ifanyiwe marekebisho	Halmashauri imeelekezwa kuifanyia marekebisho Kanuni ya 76(1) kwa kuondoa maneno "kama nakala zinapatikana".
					5. **Kanuni ya 89** inampa Meya mamlaka ya kutafsiri Kanuni na uamuzi wake ni mwisho. Hata hivyo, kwa utekelezaji bora wa Kanuni na Sheria ni vyema yakaongezwa masharti kwamba, Meya anapofanya uamuzi atazingatia Katiba, Sheria, Kanuni, Maamuzi ya Mameya waliopita na utamaduni wa uendeshaji bora wa baraza la madiwani.	Kanuni ifanyiwe marekebisho	Marekebisho yatafanyika
					6. **Kanuni ya 68** inayohusu uvunjaji wa Mikataba inapaswa kutamka wazi kwamba, uvunjaji wa Mkataba utazingatia masharti yaliyowekwa katika Sheria ya Mikataba, Sura ya 345 iliyofanyiwa marejeo mwaka 2002.	Kanuni ifanyiwe marekebisho	Ushauri umezingatiwa
59.	**GN Na. 163** 13 Mei, 2016	KANUNI ZA MAHABUSI ZA WATOTO ZA MWAKA 2012	SHERIA YA MTOTO (SURA YA 13) Kifungu cha 132	WIZARA YA AFYA MAENDELEO YA JAMII,JINSIA, WAZEE NA WATOTO	**Kanuni ya 4** imezitaja Haki za Mtoto aliyewekwa Mahabusi kutokana na amri ya mahakama. Kanuni ya 20 inazungumzia kuhusu mahabusu walio na watoto wachanga na pia Kanuni ya 21 inazungumzia haki ya mtoto mchanga kupata lishe bora. Hata hivyo, Sheria Ndogo hii haijabainisha kuhusu haki nyingine za msingi za mtoto aliyezaliwa	Waziri atote ufafanuzi	Wizara itafanya marekebisho kwa kubainisha haki zote za mtoto.

S/N	NAMBA YA TANGAZO LA SERIKALI (GN NUMBER)	JINA LA SHERIA NDOGO (NAME)	SHERIA INAYOTOA MADARAKA (ENABLING PROVISION)	MAMLAKA INAYOHUSIKA	YATOKANAYO NA UCHAMBUZI (OBSERVATIONS)	MAONI NA MAPENDEKEZO (RECOMMENDATIONS)	MAJIBU YA SERIKALI
					ndani ya mahabusi. Kimsingi Kanuni hii inakinzana misingi ya Sheria Mama, ambayo inatoa haki za msingi kwa kila mtoto pasipo kubagua.		
60.	**GN Na. 164** 13 Mei, 2016	KANUNI ZA UASILI WA WATOTO ZA MWAKA 2012	SHERIA YA MTOTO (SURA YA 13) Kifungu cha 75,157(c) na (9)	WIZARA YA AFYA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO	1. Kanuni ina makosa katika rejea ya Kifungu cha Sheria Mama (Sheria ya Mtoto) inavyoianzisha Kanuni hizi kwani, imeonyesha **Kanuni ya 157 (9)** ambayo haipo badala ya ile ya **157 (g)** ambayo ndio sahihi.	Kanuni ifanyiwe marekebisho	Wizara itafanya marekebisho
					2. **Kanuni ya 10 (1)** inaweka masharti kuhusu taarifa ya kusikilizwa kwa shauri kwa mfumo ulioainishwa katika **Fomu Na. A. C6** katika majedwali. Kanuni hiyo inamtambua Afisa wa Ustawi wa Jamii lakini katika fomu inayotajwa hakuna sehemu inayotambua ushiriki wake. Aidha katika Fomu hiyo kuna kosa la kiuandishi ambapo Kanuni inayotoa madaraka ya kuanzishwa kwake imekosewa kwa kutaja **Kanuni 13 (1)** inayohusu **amri ya kuasili** badala ya **Kanuni ya 10** inayohusu **taarifa ya kusikilizwa kwa shauri.**	Kanuni ifanyiwe marekebisho	Wizara itafanya marekebisho
					3. Katika **FOMU NA. A.C2** aya ya 5 (c) maneno "Mlezi wa kweli" yanahitaji kutafsiriwa.	Tafsiri sahihi itolewe	Wizara itafanya marekebisho

S/N	NAMBA YA TANGAZO LA SERIKALI (GN NUMBER)	JINA LA SHERIA NDOGO (NAME)	SHERIA INAYOTOA MADARAKA (ENABLING PROVISION)	MAMLAKA INAYOHUSIKA	YATOKANAYO NA UCHAMBUZI (OBSERVATIONS)	MAONI NA MAPENDEKEZO (RECOMMENDATIONS)	MAJIBU YA SERIKALI
					4. Katika FOMU NA. A.C7 aya ya 6.3 maneno "**mtoto ana kilema**" yanaweza kutafsiriwa kuwa yana unyanyapaa. Maneno yanayoweza kutumika ni "**mtoto mwenye ulemavu**"	Kanuni ifanyiwe marekebisho	Wizara itafanya marekebisho
					5. Katika Kanuni hizi, fomu mbalimbali zilizoainishwa katika majedwali zimerejea Kanuni ambazo hazitoi madaraka ya uwepo wa fomu hizo. Mfano, **FOMU NA. A.C3**, **FOMU NA. A.C4**, **FOMU NA. A.C5**, **FOMU NA. A.C6**, **FOMU NA. A.C7**, **FOMU NA. A.C8**, **FOMU NA. A.C9**	Fomu husika zifanyiwe marekebisho	Wizara itafanya marekebisho
					6. **Kanuni ya 16 (5)** inampa jukumu Kamishna kufuatilia taarifa za mtoto aliyeasiliwa na wazazi wanaoishi nje ya Tanzania pasipo kuweka muda ambao taarifa za mtoto zitafuatiliwa, kama ilivyo katika **Kanuni ya 16 (1)** inayohusu mtoto anayeasiliwa na wazazi wanaoishi Tanzania ambaye taarifa zake zitafuatilia miezi mitatu baada ya Amri ya kuasili kutolewa, ikihusisha kutembelea nyumba ambayo mtoto huyo anaishi.	Waziri atoe ufafanuzi	Wizara itafanya marekebisho kwa kuweka utaratibu na muda maalum wa kufuatilia watoto walioasiliwa nje ya nchi

S/N	NAMBA YA TANGAZO LA SERIKALI (GN NUMBER)	JINA LA SHERIA NDOGO (NAME)	SHERIA INAYOTOA MADARAKA (ENABLING PROVISION)	MAMLAKA INAYOHUSIKA	YATOKANAYO NA UCHAMBUZI (OBSERVATIONS)	MAONI NA MAPENDEKEZO (RECOMMENDATIONS)	MAJIBU YA SERIKALI
61.	**GN Na. 165** 13 Mei, 2016	KANUNI ZA MALEZI YA KAMBO ZA MWAKA 2012	SHERIA YA MTOTO (SURA YA 13) Kifungu cha 157(b)	WIZARA YA AFYA MAENDELEO YA JAMII,JINSIA, WAZEE NA WATOTO	1. **Kanuni ya 5 (5)** inaweka ukomo wa kulea watoto wakambo kuwa wasizidi watoto watatu wakati kuna uwezekano wa familia yenye watoto wakambo zaidi ya watatu. Hivyo kanuni hii inaweza kuleta usumbufu wakati wa utekelezaji wake kwani haijazingatia uhalisia wa mfumo wa Familia zetu.	Waziri atoe ufafanuzi	Wizara ilitoa ufafanuzi kwamba lengo la ukomo ni kuhakikisha idadi inakuwa ndogo ili kuhakikisha watoto wanapata matuzo yaliyo bora kwa kuzingatia hali halisi ya maisha. Kamati ilikubaliana na ufafanuzi wa Waziri.
					2. Aidha, **Kanuni ya 5** kwa ujumla haijatoa nafasi/kutambua uwepo wa Wazazi wengi wa Kambo katika Jamii yetu na namna ambavyo wanaweza kuwajibika chini ya Kanuni hii.	Waziri atoe ufafanuzi	Wizara ilifafanua kwamba, ufafanuzi umetolewa kwenye tafsiri ya Malezi ya kambo. Kamati imekubalina na ufafanuzi wa Wizara.
					3. **Kanuni ya 11 (1) (f)** inazuia adhabu ya viboko kwa watoto wa kambo. Kimsingi Kanuni hii kinyume na Sheria nyingine za nchi mfano, Sheria ya Elimu ambayo yenyewe inaruhusu adhabu ya viboko kwa watoto/wanafunzi.	Waziri atoe ufafanuzi	Wizara ilifafanua kwamba lengo ni kuondoa uwezekano wa mazingira ya watoto wa kambo kuteswa. Kamati iulikubaliana na uafafanuzi na kukubali kifungu kubaki kama kilivyo.
					4. **Kanuni ya 11(2)** inazuia kusafiri kwa Mtoto wa kambo bila ruhusa ya maandishi ya ustawi wa Jamii.Tafsiri ya Kanuni hii ina utata kwani haijaainisha aina gani ya safari kama ni ya nje au ya ndani ya nchi (miongoni mwa wanafamilia), inayohitaji kibali cha Kamishna wa Ustawi wa Jamii.	Waziri atoe ufafanuzi	Wizara ilifafanua kwamba safari ni za nje na ndani kwa lengo la kuhakikisha usalama wa mtoto unalindwa. Kamati ilikubaliana na uafafanuzi na kukubali kifungu kubaki kama kilivyo.

S/N	NAMBA YA TANGAZO LA SERIKALI (GN NUMBER)	JINA LA SHERIA NDOGO (NAME)	SHERIA INAYOTOA MADARAKA (ENABLING PROVISION)	MAMLAKA INAYOHUSIKA	YATOKANAYO NA UCHAMBUZI (OBSERVATIONS)	MAONI NA MAPENDEKEZO (RECOMMENDATIONS)	MAJIBU YA SERIKALI
					5. **Kanuni ya 11(5)** inamzuia Mzazi wa Kambo kutoacha majukumu ya kutunza mtoto wa kambo mikononi mwa mtu mwingine kwa kipindi cha zaidi ya wiki moja mfululizo bila ruhusa ya Afisa Ustawi wa Jamii. Kanuni haiko wazi kwa Mzazi wa kambo mwenye mwenza wake kama na yeye atahitji aombewe kibali cha kumhudumia Mtoto wa kambo kwa huo muda ambao Mzazi wa Kambo hatakuwepo.	Waziri atoe ufafanuzi	Wizara ilifafanua kwamba lengo la kuhakikisha usalama wa mtoto unalindwa. Kamati ilikubaliana na ufafanuzi na kukubali kifungu kubaki kama kilivyo.
					6. **Kanuni ya 15 (1)** maneno...*'hadi awe amefanyiwa vipimo'*...yafutwe na kuandikwa: "baada ya kuwa amefanyiwa vipimo" ili kuleta tafsiri sahihi.	Kanuni ifanyiwe marekebisho	Wizara itafanya marekebisho
					7. **Kanuni 15 (a)** neno ...*'kwanza'* lifutwe na kuandikwa...'Kuanza' ili kuleta tafsiri sahihi.	Kanuni ifanyiwe marekebisho	Wizara itafanya marekebisho
					8. **Kanuni ya 16 (1) (a)** neno...*'kwanza'* liandikwe ..*'kuanza'* ili liweze kuleta tafsiri sahihi.	Kanuni ifanyiwe marekebisho	Wizara itafanya marekebisho
					9. **Kanuni ndogo ya 1** katika **kanuni ya 20** ifutwe na kuandikwa kanuni ya 20 kwakuwa hakuna hoja inayofuata baada ya hiyo.	Kanuni ifanyiwe marekebisho	Wizara itafanya marekebisho

S/N	NAMBA YA TANGAZO LA SERIKALI (GN NUMBER)	JINA LA SHERIA NDOGO (NAME)	SHERIA INAYOTOA MADARAKA (ENABLING PROVISION)	MAMLAKA INAYOHUSIKA	YATOKANAYO NA UCHAMBUZI (OBSERVATIONS)	MAONI NA MAPENDEKEZO (RECOMMENDATIONS)	MAJIBU YA SERIKALI
					10. Sheria mama, chini ya **kifungu cha 14, 17 (3), 30 (1), 158 (2) na 159**, kumeainishwa adhabu mbalimbali chini ya sheria moja ya Sheria ya Mtoto. Hata hivyo, adhabu inayotajwa katika **kanuni ya 20 (1)** inakosa mahusiano ya moja kwa moja kutoka moja wapo ya vifungu vilivyotajwa chini ya Sheria mama husika.	Kanuni ifanyiwe marekebisho	Wizara itafanya marekebisho
					11. Aidha, **Kifungu cha 157 (b)** ambacho ni chimbuko la Kanuni hizi, kiko kimya kuhusiana na kiwango cha adhabu inayotakiwa kutolewa kutokana na ukiukwaji wa kanuni hizi.	Kanuni ifanyiwe marekebisho	Wizara itafanya marekebisho
62.	**GN Na. 166** 13 Mei, 2016	KANUNI ZA MAKAO YA WATOTO ZA MWAKA 2012	SHERIA YA MTOTO (SURA YA 13) Kifungu cha 145 na 175	WIZARA YA AFYA MAENDELEO YA JAMII,JINSIA, WAZEE NA WATOTO	1. **Kanuni ya 18 (7) (f)** ina makosa ya uandishi ambayo yanafanya kisisomeke na kuleta maana iliyokusudiwa kwani kinazungumzia choo kuwa na vifaa muhimu vya kupikia.	Kanuni ifanyiwe marekebisho	Wizara itafanya marekebisho
					2. **Kanuni ya 30** inatoa haki ya mtoto kulalamika kuhusu jambo lolote na pia imetaja sehemu/mamlaka ambazo mtoto anaweza kulalamika *(horizontal hiearchy)*. Hata hivyo, Kanuni hii haijaonyesha utaratibu wa kukata rufaa *(vertical hierarchy)* pindi ambapo malalamiko ya mtoto hayatashughulikiwa au yatapata majibu ambayo hayajamridhisha mtoto huyo.	Kanuni ifanyiwe marekebisho	Wizara itafanya marekebisho

S/N	NAMBA YA TANGAZO LA SERIKALI (GN NUMBER)	JINA LA SHERIA NDOGO (NAME)	SHERIA INAYOTOA MADARAKA (ENABLING PROVISION)	MAMLAKA INAYOHUSIKA	YATOKANAYO NA UCHAMBUZI (OBSERVATIONS)	MAONI NA MAPENDEKEZO (RECOMMENDATIONS)	MAJIBU YA SERIKALI
63.	**GN Na. 167** 13 Mei, 2016	KANUNI ZA VITUO VYA KULELEA WATOTO WADOGO MCHANA NA WATOTO WACHANGA ZA MWAKA 2014	SHERIA YA MTOTO, (SURA YA 13) Kifungu cha 145 na 175	WIZARA YA AFYA MAENDELEO YA JAMII,JINSIA, WAZEE NA WATOTO	1. Kanuni wala Sheria Mama hazijatoa tafsiri ya maneno "Mtoto mchanga". Aidha, ukomo wa umri wa mtoto mchanga haujawekwa bayana katika Kanuni hii.	Kanuni ifanyiwe marekebisho	Wizara itafanya marekebisho
					2. **Kanuni ya 3** inatoa tafsiri ya neno "**ulemavu**" kuwa ni hali inayotokana na dosari kwenye mwili, akili na milango ya fahamu ambayo inasababisha mtu kushindwa kutenda mambo fulani kikamilifu. Maneno "**dosari kwenye mwili**" yanaweza kutafsirika kumnyanyapaa mtu mwenye ulemavu. Aidha, Sheria Mama katika kumtafsiri "**Mtoto mwenye ulemavu**" hakuna neno "dosari".	Kanuni ifanyiwe marekebisho	Wizara itafanya marekebisho
					3. **Kanuni ya 4 (1)** inazungumzia maombi ya usajili wa kituo cha kulelea watoto wadogo mchana au watoto wachanga (daycare) bila kuainisha masharti yanayohusu kuwepo kwa vigezo vya utaalamu au mafunzo maalum ya kuendesha shughuli hiyo. Masharti haya, kwa sehemu yamegusiwa katika **Kanuni ya 6** lakini bado hayajitoshelezi kuainisha aina ya watumishi/rasilimali watu kwa kuzingatia vigezo vya utaalamu au mafunzo maalum.	Kanuni ifanyiwe marekebisho	Wizara itafanya marekebisho

S/N	NAMBA YA TANGAZO LA SERIKALI (GN NUMBER)	JINA LA SHERIA NDOGO (NAME)	SHERIA INAYOTOA MADARAKA (ENABLING PROVISION)	MAMLAKA INAYOHUSIKA	YATOKANAYO NA UCHAMBUZI (OBSERVATIONS)	MAONI NA MAPENDEKEZO (RECOMMENDATIONS)	MAJIBU YA SERIKALI
					4. Katika **Kanuni ya 6 (1) (c)** kunakosekana kiunganishi kati ya maneno "uthibitisho" na "mtiririko" na hivyo sentesi kukosa maana.	Kanuni ifanyiwe marekebisho	Wizara itafanya marekebisho
					5. **Kanuni ya 18 (9)** kinaweka masharti yanayokinzana na Kanuni yenyewe na pia **Kanuni ya 18 (10).** Kwa upande mmoja kinaweka sharti kwamba Kituo cha Kulelea Watoto Mchana au Watoto Wachanga hakitapaswa kuwa na bwawa la kuogelea *(swimming pool)* wakati huo huo kinaweka sharti la kwamba bwawa la kuogelea litakuwa chini ya usimamizi ili watoto wasizame au kujengwa kwa ustadi. Kanuni iweke wazi kuwa hakutakuwa na bwawa la kuogelea AU bwawa la kuogelewa likiwepo, kuwepo na masharti ya usimamizi wa wataalam kuhusiana na mabwawa ya kuogelea, waalimu wa kufundisha kuogelea na wataaalam wengine muhimu.	Kanuni ifanyiwe marekebisho	Wizara itafanya marekebisho

S/N	NAMBA YA TANGAZO LA SERIKALI (GN NUMBER)	JINA LA SHERIA NDOGO (NAME)	SHERIA INAYOTOA MADARAKA (ENABLING PROVISION)	MAMLAKA INAYOHUSIKA	YATOKANAYO NA UCHAMBUZI (OBSERVATIONS)	MAONI NA MAPENDEKEZO (RECOMMENDATIONS)	MAJIBU YA SERIKALI
					6. **Kanuni ya 25 (2)** inaweka masharti ya ukaguzi wa vituo vya kulelea watoto wachanga kwamba iwe angalau mara moja katika kila miezi sita (6). Kipindi hiki cha ukaguzi ni kirefu, kinaweza kusababisha ukiukwaji wa Haki za Msingi za mtoto chini ya Sheria ya Mtoto kwani itachochea kutofuatiliwa na kuchukuliwa hatua kwa wakati kwa haki hizo. Kanuni iweke sharti kwamba ukaguzi ufanyike **kila baada ya miezi mitatu** ili iendane na masharti yanayopatikana katika Kanuni **ya 27 (1)** inayomtaka mmiliki wa Kituo cha Kulelea watoto kuwasilisha taarifa ya robo mwaka.	Kanuni ifanyiwe marekebis	Wizara itafanya marekebisho
					7. Katika **Jedwali la Saba aya ya 14** la Kanuni hizi kuna matumizi ya maneno "HIV/AIDS" ambayo yako katika lugha ya Kiingereza. Lugha ya Kiswahili itumike.	Jedwali lifanyiwe marekebisho	Wizara itafanya marekebisho
64.	**GN Na. 168** 13 Mei, 2016	KANUNI ZA AJIRA ZA WATOTO ZA MWAKA 2012	SHERIA YA MTOTO, (SURA YA 13)	WIZARA YA AFYA MAENDELEO YA JAMII,JINSIA, WAZEE NA WATOTO	1. Kanuni haijaonyesha imetungwa chini ya Kifungu gani cha Sheria Mama.	Kanuni zifanyiwe marekebisho	Kanuni itarekebishwa kuonesha kuwa imetungwa chini ya Kifungu cha 157 (d) cha Sheria ya Mtoto
					2. **Kanuni ya 3** inatafsiri neno "*Kazi za hatari"* tofauti na maana inayotolewa katika **Kifungu cha 3** cha Sheria Mama (Sheria ya Mtoto, Sura ya 13).	Kanuni ifanyiwe marekebisho	Kanuni itafanyiwa marekebisho

S/N	NAMBA YA TANGAZO LA SERIKALI (GN NUMBER)	JINA LA SHERIA NDOGO (NAME)	SHERIA INAYOTOA MADARAKA (ENABLING PROVISION)	MAMLAKA INAYOHUSIKA	YATOKANAYO NA UCHAMBUZI (OBSERVATIONS)	MAONI NA MAPENDEKEZO (RECOMMENDATIONS)	MAJIBU YA SERIKALI
					3. **Kanuni ya 3** inatafsiri neno "majengo" kwa kujumuisha magari, ndege na maeneo mengine ambayo yangeweza kutolewa tafsiri zinazojitegemea.	Kanuni ifanyiwe marekebisho	Kanuni itafanyiwa marekebisho
					4. **Kanuni ya 4** inazungumzia umri wa chini wa kuajiriwa kuwa ni miaka kumi na nne (14). Hata hivyo **Kanuni 4 (2)** inaweka masharti ambapo mtoto mwenye umri **chini ya** miaka kumi na nne anaweza kuajiriwa. Kanuni iandikwe upya kuondoa maneno **"chini ya"** ili kuondoa mazingira ya mtoto mwenye umri chini ya miaka kumi na nne (14) kuajiriwa.	Kanuni ifanyiwe marekebisho	Kanuni itafanyiwa marekebisho
					5. **Katika Kanuni ya 4 (4)** kuna kosa la kiuchapaji. Neno "**Haziharibika**" halina maana. Huenda neno lililopaswa kutumika ni "**Hazitahesabika**".	Kanuni ifanyiwe marekebisho	Kanuni itafanyiwa marekebisho
					6. **Kanuni ya 5** inatoa katazo kumshirikisha mtoto katika kazi za unyonyaji na kurejea vifungu vya Sheria ya Mahusiano Kazini bila kurejea **Kifungu cha 78** cha Sheria ya Mtoto, Sura ya 13 ambayo ndiyo sheria inayoanzisha Kanuni hii na kuongelea masuala ya kazi za kinyonyaji.	Kanuni ifanyiwe marekebisho	Kanuni itafanyiwa marekebisho

S/N	NAMBA YA TANGAZO LA SERIKALI (GN NUMBER)	JINA LA SHERIA NDOGO (NAME)	SHERIA INAYOTOA MADARAKA (ENABLING PROVISION)	MAMLAKA INAYOHUSIKA	YATOKANAYO NA UCHAMBUZI (OBSERVATIONS)	MAONI NA MAPENDEKEZO (RECOMMENDATIONS)	MAJIBU YA SERIKALI
					7. **Kanuni ya 7 (1)** inazungumzia mtoto kutoajiriwa katika mazingira hatarishi lakini wakati huo huo inaweka masharti kuwa mazingira hayo hayatochukuliwa kuwa ni hatarishi ikiwa mtoto amefikisha umri chini ya miaka 16 na anafanya kazi chini ya uangalizi. Maneno "chini ya miaka kumi na sita" yanapaswa kufutwa ili dhana ya mtoto mwenye miaka kumi na sita kufanya kazi hizo iweze kujumuishwa.	Kanuni ifanyiwe marekebisho	Kanuni itafanyiwa marekebisho
					8. **Kanuni ya 7 (3)** kuna kosa la kiuchapaji. Neno "Wazira" linapaswa kusomeka kama "Waziri".	Kanuni ifanyiwe marekebisho	Kanuni itafanyiwa marekebisho
					9. **Kanuni ya 9 (3)** inaweka masharti yanayotambua mazingira ambayo ni hatarishi kufanya kazi ikijumuisha maeneo na hali ambazo kimsingi zinakosa uhalisia, Mfano joto, kuinama, kusimama au kukaa.	Kanuni ifanyiwe marekebisho	Kanuni itafanyiwa marekebisho
					10. **Kanuni ya 14 (3)** inazungumzia wajibu wa mwajiri kutombagua mwajiriwa mtoto kwa vigezo mbalimbali kama vile uyatima, hali ya UKIMWI na ukabila. Kanuni hii iandikwe upya na kuondoa maneno ambayo kimsingi ndiyo yanachochea ubaguzi. Sharti la mwajiri kutobagua na kutopendelea linapaswa kuwekwa kama lilivyo bila kutaja aina za ubaguzi kwa kuwa sio rahisi kuorodhesha aina hizo zote.	Kanuni ifanyiwe marekebisho	Kanuni itafanyiwa marekebisho

S/N	NAMBA YA TANGAZO LA SERIKALI (GN NUMBER)	JINA LA SHERIA NDOGO (NAME)	SHERIA INAYOTOA MADARAKA (ENABLING PROVISION)	MAMLAKA INAYOHUSIKA	YATOKANAYO NA UCHAMBUZI (OBSERVATIONS)	MAONI NA MAPENDEKEZO (RECOMMENDATIONS)	MAJIBU YA SERIKALI
					11. Jedwali la kwanza limeanisha kazi hatarishi katika Kipengele A-Kilimo, sehemu ya 8 kwamba itakuwa ni kazi hatarishi **kubeba uchafu kwa ajili ya kutupa**. Kimsingi maudhui ya maneno haya hayaelezi bayana ni uchafu wa namna ipi ambao mtoto hataruhusiwa kutupa.	Jedwali lifanyiwe marekebisho	Marekebisho yatafanyika
					12. Suala la Mtoto kutohusika katika biashara ya uuzaji wa vileo halijawekwa kama moja ya kazi hatarishi katika Jedwali, kwani suala la watoto kutohuhishwa na vileo limekatazwa katika Sheria ya Mtoto chini ya **Kifungu cha *17(1)(2)*** ambacho kinasema; *17(1) Mtu ambaye ni mmiliki au anaendesha au ni msimamizi wa ukumbi wa muziki,baa au klabu ya usiku, hatamruhusu mtoto kuingia katika maeneo hayo* *17(2) Mtu hatamuuzia mtoto, sigara, pombe, pombe kali, madawa ya kulevya au kitu chochote kinacholewesha.*	Jedwali lifanyiwe marekebisho	Marekebisho yatafanyika

S/N	NAMBA YA TANGAZO LA SERIKALI (GN NUMBER)	JINA LA SHERIA NDOGO (NAME)	SHERIA INAYOTOA MADARAKA (ENABLING PROVISION)	MAMLAKA INAYOHUSIKA	YATOKANAYO NA UCHAMBUZI (OBSERVATIONS)	MAONI NA MAPENDEKEZO (RECOMMENDATIONS)	MAJIBU YA SERIKALI
					13. **Kanuni ya 20** inaeleza kuhusu sheria zitakazotumika kutoa adhabu kuwa ni Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16 na Sheria ya Mahusiano Kazini, Sura 366, lakini **Kanuni ya 21** inaelekeza tu kwamba pale masharti ya ajira yanapovunjwa basi yapelekwa katika Mahakama za Sheria kwa mujibu wa Sheria ya Taasisi za Ajira, bila kubainisha mfumo wa upelekaji wa mashauri katika Mahakama za jinai pale ambapo uvunjaji wa masharti ya ajira una sura ya jinai. Aidha uandishi wa Kanuni hii uzingatie nyakati (tenses) kwa kusema kuwa "pale ambapo mtu atakiuka" badala ya kusema "pale ambapo mtu anakiuka".	Kanuni ifanyiwe marekebisho	Kanuni itafanyiwa marekebisho
65.	**GN Na. 169** 13 Mei, 2016	KANUNI ZA USALAMA WA WATOTO ZA MWAKA 2014	SHERIA YA MTOTO, (SURA YA 13) Kifungu 157(a)	WIZARA YA AFYA MAENDELEO YA JAMII,JINSIA, WAZEE NA WATOTO	1. **Kanuni ya 3 (2) (d)** inataja suala la kabila la mtoto kama miongoni mwa vipaumbele/misingi yakuzingatia wakati wa kufanya maamuzi kuhusu malezi salama ya mtoto.Hata hivyo, kulingana na mabadiliko ya kijamii na muingiliano wa watanzania kwa sasa na hata baadaye, kigezo cha ukabila ni suala lilopitwa na wakati kwa mantiki ya ulinzi na usalama wa mtoto.	Waziri atoe ufafanuzi	Wizara itafanya marekebisho kwa kuwa suala la ukabila limepitwa na wakati.

S/N	NAMBA YA TANGAZO LA SERIKALI (GN NUMBER)	JINA LA SHERIA NDOGO (NAME)	SHERIA INAYOTOA MADARAKA (ENABLING PROVISION)	MAMLAKA INAYOHUSIKA	YATOKANAYO NA UCHAMBUZI (OBSERVATIONS)	MAONI NA MAPENDEKEZO (RECOMMENDATIONS)	MAJIBU YA SERIKALI
					2. **Kanuni ya 4 (3)** imeainisha madhara yanayoweza kusababishwa kwa Mtoto, hata hivyo madhara ya kisaikolojia hayajabainishwa kana kwamba Mtoto hawezi kudhurika kisaikolojia.	Waziri atoe ufafanuzi	Madhara ya kisaikolojia yanahusisha ukatili wa kiakili, kihisia. Kwani kanuni hii imegusa madhara ya kihisia ambayo ni sehemu ya madhara hayo. Hivyo Kanuni ibaki kama ilivyo. Kamati imekubaliana na ufafanuzi wa Wizara.
					3. **Kanuni ya 4(4)(c)** inaainisha aina mbalimbali za udhalilishaji wa kijinsia. Hata hivyo, suala la upendeleo wa kijinsia kwa mtoto mmoja dhidi ya mwingine unaoweza kufanywa na mlezi/mzazi, halijaainishwa kama moja wapo ya udhalilishaji wa kijinsia.	Kanuni ifanyiwe marekebisho	Wizara itafanya marekebisho ili kuanisha aina zote za udhalilishaji wa kijinsia.
					4. **Neno** 'Rafaa' katika sehemu ya nne ya Kanuni liandikwe 'Rufaa' ili kuleta maana stahiki.	Kanuni ifanyiwe marekebisho	Kanuni itafanyiwa marekebisho
					5. **Kanuni ya 16 (6),(7)** inazungumzia hoja moja, kwahiyo, vyema kanuni ndogo ya 7 ikaunganishwa kwenye kanuni ndogo ya 6 ili kuleta mantiki stahiki.	Kanuni ifanyiwe marekebisho	Kanuni itafanyiwa marekebisho
					6. **Kanuni ya 20**: Neno *'kitatibu'* yaliyoko kwenye maneno ya kanuni (Marginal notes) liandikwe *'kitabibu'* ili kuleta maana stahiki.	Kanuni ifanyiwe marekebisho	Kanuni itafanyiwa marekebisho
					7. **Kanuni ya 20 (3)** neno …*'ana'*..Liandikwe…*'hana'*…ili kanuni ndogo hiyo isomeke kama ifuatavyo:- *Tathmini endapo mtoto hana umri na ukomavu wa kutosha itafanywa na daktari anayefanya uchunguzi.*	Kanuni ifanyiwe marekebisho	Kanuni itafanyiwa marekebisho

S/N	NAMBA YA TANGAZO LA SERIKALI (GN NUMBER)	JINA LA SHERIA NDOGO (NAME)	SHERIA INAYOTOA MADARAKA (ENABLING PROVISION)	MAMLAKA INAYOHUSIKA	YATOKANAYO NA UCHAMBUZI (OBSERVATIONS)	MAONI NA MAPENDEKEZO (RECOMMENDATIONS)	MAJIBU YA SERIKALI
					8. **Kanuni ya 22 (5),** neno ... 'ya'... lililopo kati ya maneno ...'mahali .... Usalama'..lifutwe na kuandikwa 'pa' ili kuleta tafsiri sahihi.Hivyo, maneno hayo yasomeke..*'mahali pa usalama'...*	Kanuni ifanyiwe marekebisho	Kanuni itafanyiwa marekebisho
					9. **Kanuni ya 22(9),** kuongezwe neno 'pa' katikati ya maneno...*'mahali'* na *'usalama'*	Kanuni ifanyiwe marekebisho	Kanuni itafanyiwa marekebisho
					10. Maneno ya **Kanuni ya 26 (Marginal Notes)** yameandikwa kwa kuchanganya lugha ya Kiswahili na Kiingereza...*'utaratibu endapo kuna cause for concern kufuatia Uchunguzi'*..	Kanuni ifanyiwe marekebisho	Kanuni itafanyiwa marekebisho
					11. **Kanuni ya 30 (2) (b) na (c),**vinazungumzia kitu kimoja: sifa za Mwenyekiti wa mkutano wa usalama wa mtoto , hivyo hoja iliyopo chini ya **kipengele (c)** ihamie katika **kipengele (b)** ili kuleta muunganiko mzuri wa mtiririko wa sifa husika za Mwenyekiti.	Kanuni ifanyiwe marekebisho	Kanuni itafanyiwa marekebisho
					12. **Kanuni ya 32(1),** neno *'atamkata'* liandikwe *'atamtaka'* ili kuleta maana stahiki.	Kanuni ifanyiwe marekebisho	Kanuni itafanyiwa marekebisho
					13. **Kanuni ya 39(2)...**neno '*uliyotolewa*' iandikwe '*iliyotolewa'*	Kanuni ifanyiwe marekebisho	Kanuni itafanyiwa marekebisho
					14. **Kanuni ya 39 (3) na (4)**, mtiririko wa hoja zake haujaunganishwa ili kuleta tafsiri iliyokusudiwa.	Kanuni ifanyiwe marekebisho	Kanuni itafanyiwa marekebisho

S/N	NAMBA YA TANGAZO LA SERIKALI (GN NUMBER)	JINA LA SHERIA NDOGO (NAME)	SHERIA INAYOTOA MADARAKA (ENABLING PROVISION)	MAMLAKA INAYOHUSIKA	YATOKANAYO NA UCHAMBUZI (OBSERVATIONS)	MAONI NA MAPENDEKEZO (RECOMMENDATIONS)	MAJIBU YA SERIKALI
					15. **Kanuni ya 46 (1)** na **(2)**:-kuna makosa ya kiuandishi katika kanuni hizo ndogo ambayo yanaathiri mtiririko wa maana halisi iliyokusudiwa. Hii ni pamoja na maneno:*'Ustawi wa Jamii ita'*- katika Kanuni ndogo ya (1) ambayo hayana muunganiko wowote na kipengele (a), sambamba na meneno: *'Pale ambapo Mtoto ame'*- chini ya kanuni ndogo ya (2) hayana mtiririko mzuri katika vipengele (a), (b) na (c).	Kanuni ifanyiwe marekebisho	Kanuni itafanyiwa marekebisho
66.	**GN Na. 170** 13 Mei, 2016	KANUNI ZA MWENENDO WA MAHAKAMA ZA WATOTO ZA MWAKA 2014	SHERIA YA MTOTO, (SURA YA 13) Kifungu cha 99(1)	WIZARA YA AFYA MAENDELEO YA JAMII,JINSIA, WAZEE NA WATOTO	1. **Kanuni ya 21 (3)** inahusu hati ya wito kwa mtoto *(summons)* bila kutaja mazingira ambayo mtoto anaweza kuhudhuria Mahakamani akiwa au akisindikizwa na mtu mzima. Hata hivyo, Kifungu **cha 99 (1) (f)** cha Sheria Mama kinatoa haki kwa mtoto kuwa na ndugu wa karibu au wakili katika taratibu za kimahakama. Hivyo basi, ni vyema Kanuni hii ikaweka sharti la kuwepo mtu wa kumsindikiza mtoto anapoitikia wito wa mahakama *(summons)*.	Kanuni ifanyiwe marekebisho	Kanuni itafanyiwa marekebisho

S/N	NAMBA YA TANGAZO LA SERIKALI (GN NUMBER)	JINA LA SHERIA NDOGO (NAME)	SHERIA INAYOTOA MADARAKA (ENABLING PROVISION)	MAMLAKA INAYOHUSIKA	YATOKANAYO NA UCHAMBUZI (OBSERVATIONS)	MAONI NA MAPENDEKEZO (RECOMMENDATIONS)	MAJIBU YA SERIKALI
					2. **Kanuni 23 (4) (a)** haijataja eneo mahsusi ambalo mtoto atawekwa kizuizini siku ya Ijumaa baada ya saa za kazi baada ya kukamatwa na polisi kwa hati ya kukamatwa *(warranty of arrest)*. Kwa kutotaja eneo mahsusi ambalo mtoto atawekwa kizuizini, kunahatarisha ustawi wa mtoto endapo atawekwa kizuizini eneo lolote kinyume na Kifungu cha 101 cha Sheria Mama.	Kanuni ifanyiwe marekebisho	Eneo mahsusi ambalo mtoto huyo atawekwa limeelezwa katika kanuni ya 23(5)(b) ambayo itajumuisha makao ya watoto au walezi wa kuaminika. Kamati inakubalina na ufafanuzi wa Wizara.
					3. **Kanuni ya 25 (1)** inaipa Mahakama uhuru wa kutoa *(may)* hati ya wito kwa mzazi/mlezi/mwangalizi kuhudhuria shauri la jinai linalomhusu mtoto pale ambapo ameshindwa kuhudhuria shauri la mtoto huyo. Katika hatua hii, ni vyema kanuni ikaweka masharti ambayo yatamlazimisha mzazi/mlezi/mwangalizi *(shall)* kuhudhuria shauri la jinai linalomshuru mtoto huyo.	Kanuni ifanyiwe marekebisho	Kanuni itafanyiwa marekebisho
					4. **Kanuni ya 38 (1)** inazungumzia kuhusu kuahirisha kesi *(adjournement)* bila kutaja muda. Kwa mshtakiwa ambaye yuko mahabusi, sharti hili linaweza kumfanya mtoto akae kizuizini kwa muda mrefu kinyume na dhana ya kuharakisha kesi za watoto.	Kanuni ifanyiwe marekebisho	Kanuni itafanyiwa marekebisho

S/N	NAMBA YA TANGAZO LA SERIKALI (GN NUMBER)	JINA LA SHERIA NDOGO (NAME)	SHERIA INAYOTOA MADARAKA (ENABLING PROVISION)	MAMLAKA INAYOHUSIKA	YATOKANAYO NA UCHAMBUZI (OBSERVATIONS)	MAONI NA MAPENDEKEZO (RECOMMENDATIONS)	MAJIBU YA SERIKALI
					5. **Kanuni ya 45 (4)** imetoa baadhi ya mambo ya kuzingatiwa **pale** ambapo maswali yataulizwa kwa mtoto anayeshitakiwa au anayetoa ushahidi, pasipo kuweka sharti la kuepuka kuuliza maswali kwa njia ya ukali jambo linaloweza kumtisha mtoto na kuathiri ushahidi wake.	Kanuni ifanyiwe marekebisho	Kanuni itafanyiwa marekebisho
					6. **Kanuni ya 54 (5)** inaweka utaratibu wa kufuatwa pale ambapo mtoto aliyewekwa kizuizini kwa muda mrefu zaidi ya kipindi alichopangiwa kuwasilisha maombi ya kuachiwa huru kwa mamlaka husika. Hata hivyo kanuni haijaweka masharti ambayo yanamuwezesha mtoto kupata msaada wa kuwasilisha maombi hayo kutoka kwa mzazi/mlezi/mwangalizi/afisa ustawi wa jamii au mtu mwingine yeyote.	Kanuni ifanyiwe marekebisho	Wizara itafanya marekebisho kwa kuweka sharti la mtoto kupata msaada kutoka kwa mzazi/mlezi/mwangalizi/afisa ustawi wa jamii au mtu mwingine yeyote.
67.	**GN Na. 172** 13 Mei, 2016	KANUNI ZA MAFUNZO YA UANAGENZI ZA MWAKA, 2012	SHERIA YA MTOTO (SURA YA 13)	WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO	Uanagenzi *(apprenticeship)* ni mafunzo ya ujuzi au weledi wa kazi unaoweza kutolewa chuoni au mahali pa kazi kwa muda fulani na yanaweza kufanyika kwa makubaliano ya malipo fulani. Mafunzo haya yanaweza kutolewa na sekta rasmi au isiyo rasmi. 1. Kanuni hazibainisha zimetungwa chini ya Kifungu gani cha Sheria Mama.	Kanuni ifanyiwe marekebisho	Wizara itafanya marekebisho na kuonyesha Kanuni imetungwa chini ya Kanuni ya 157 (e)

S/N	NAMBA YA TANGAZO LA SERIKALI (GN NUMBER)	JINA LA SHERIA NDOGO (NAME)	SHERIA INAYOTOA MADARAKA (ENABLING PROVISION)	MAMLAKA INAYOHUSIKA	YATOKANAYO NA UCHAMBUZI (OBSERVATIONS)	MAONI NA MAPENDEKEZO (RECOMMENDATIONS)	MAJIBU YA SERIKALI
					2. Kosa la kiuandishi katika **Kanuni ya 7 (3)** ambapo inaweka masharti kuwa mtoto wa miaka minne (4) au zaidi anaweza kujiunga na mafunzo yasiyo ya rasmi ya uanagenzi wakati huo huo Kanuni ya 7 (1) ikiweka sharti kuwa umri wa chini wa kujiunga na mafunzo hayo ni miaka kumi na nne (14).	Kanuni ifanyiwe marekebisho	Kanuni itafanyiwa marekebisho
					3. **Kanuni ya 5 (13) na 6 (10)** zinaweka jukumu kwa mamlaka za Serikali za Mitaa kutoa msaada wa kifedha kwa mwanagenzi anayetoka katika familia ya kipato cha chini. Hata hivyo Kanuni hii haijazingatia hali halisi ya uwezo wa kifedha wa Serikali za Mitaa.	Waziri atoe ufafanuzi	Sheria Mama katika kifungu cha 94 imetoa majukumu kwa serikali za mitaa kuhakikisha hali bora ya watoto kwenye mamlaka yao. Aidha, wanagenzi ni miongoni mwa watoto hao na serikali za mitaa wana jukumu la kutenga bajeti kwa ajili ya kutoa misaada kwa watoto wenye mahitaji maalum kwenye maeneo yao.
					4. **Kanuni ya 10 (2)** na **10 (3)** zina masharti ambayo **y**anafanana	Marekebisho yafanyike	Marekebisho yatafanyika
					5. **Kanuni ya 11 (5)** inaweka masharti yanayotambua mazingira ambayo ni hatarishi kufanya kazi ikijumuisha maeneo na hali ambazo kimsingi zinakosa uhalisia, Mfano joto, kuinama, kusimama au kukaa chini.	Waziri atoe ufafanuzi	Marekebisho yatafanyika ili kuhakikisha kanuni hii inaainisha masharti yanayotekelezeka na yenye uhalisia.

S/N	NAMBA YA TANGAZO LA SERIKALI (GN NUMBER)	JINA LA SHERIA NDOGO (NAME)	SHERIA INAYOTOA MADARAKA (ENABLING PROVISION)	MAMLAKA INAYOHUSIKA	YATOKANAYO NA UCHAMBUZI (OBSERVATIONS)	MAONI NA MAPENDEKEZO (RECOMMENDATIONS)	MAJIBU YA SERIKALI
					6. *Marginal notes* za **Kanuni ya 20** na **Kanuni ya 25** hazina uhusiano na masharti yaliyoandikwa katika Kanuni husika.	Marekebisho yafanyike	Marekebisho yatafanyika
68.	**GN Na. 173** 13 Mei, 2016	THE DRUGS CONTROL AND ENFORCEMENT (GENERAL) REGULATIONS, 2016	THE DRUGS CONTROL AND ENFORCEMENT ACT, (SURA YA 95) Kifungu cha 67	OFISI YA WAZIRI MKUU	1. **Kanuni ya 5 (5)** inakataza mmiliki wa mali inayopigwa mnada pamoja na ndugu zake kununua mali hiyo, lakini Kanuni haijatoa katazo la kununuia mali kwa Kampuni/Makampuni ambayo mwenye mali ni mmiliki au mbia, pia marafiki wa karibu,kiasi ambacho inaweza kutoa mwanya kwa mali hiyo kurudi kwa mmiliki	Kanuni ifanyiwe marekebisho	NIL
					2. **Kanuni ya 14 (2)** inatoa mamlaka kwa Kamishna wa Madawa ya kulevya kuharibu madawa yaliyokamatwa pasipo kushirikisha watu waliotajwa katika **Kanuni ya 14 (1)** pale atakapoona inafaa. Kimsingi kutoshirikisha watu wengine kunaweza kutumika vibaya na kusababisha rushwa na kurejea kwa madawa hayo katika mzunguko.	Kanuni ifanyiwe marekebisho	NIL

S/N	NAMBA YA TANGAZO LA SERIKALI (GN NUMBER)	JINA LA SHERIA NDOGO (NAME)	SHERIA INAYOTOA MADARAKA (ENABLING PROVISION)	MAMLAKA INAYOHUSIKA	YATOKANAYO NA UCHAMBUZI (OBSERVATIONS)	MAONI NA MAPENDEKEZO (RECOMMENDATIONS)	MAJIBU YA SERIKALI
					3. Pia kuna kukinzana na kukiukwa kwa misingi ya uandishi kwa **Kanuni ya 14 (1) na 14 (2),** kwasababu **Kanuni ya 14(1)** imetumia neno *shall* kuonyesha ulazima wa kuwepo kwa watu wengine waiotajwa katika zoezi la kuharibu madawa yaliyokamatwa; wakati **Kanuni ya 14(2)** inatumia neno ***May*** kuonyesha utashi anaoweza kutumia Kamishna kutowashirikisha wadau wengine katika zoezi la kuharibu madawa.	Marekebisho yafanyike	NIL
					4. Matakwa ya **Kanuni ya 14 (2)** yanakinzana na **Kanuni ya 14 (3)** inayotaka wakati wa kuharibu madawa basi kuzingatiwe ulinzi wa afya, usalama hali kadhalika ulinzi wa mazingira; hivyo kukosekana kwa wataalam walioanishwa katika **Kanuni ya 14 (1)** kunaweza kupelekea kukiukwa kwa **Kanuni ya 14 (3)**.	Marekebisho yafanyike	NIL
					5. Aidha **Kanuni ya 14 (2)** pia inakinzana na **Kanuni ya 14 (5)** na **14 (7)** zinazotoa sharti kwa Jaji au Hakimu aliyeshuhudia kuharibiwa kwa madawa kujiridhisha kwamba yote yameharibiwa na hatimaye kujaza fomu ya kuthibitisha hilo. Hivyo uwepo wa Kamishna pekee wakati wa zoezi kuharibu madawa kutaondoa utekelezaji wa matakwa ya Kanuni hii.	Marekebisho yafanyike	NIL

S/N	NAMBA YA TANGAZO LA SERIKALI (GN NUMBER)	JINA LA SHERIA NDOGO (NAME)	SHERIA INAYOTOA MADARAKA (ENABLING PROVISION)	MAMLAKA INAYOHUSIKA	YATOKANAYO NA UCHAMBUZI (OBSERVATIONS)	MAONI NA MAPENDEKEZO (RECOMMENDATIONS)	MAJIBU YA SERIKALI
69.	**GN Na. 174** 13 Mei, 2016	THE PETROLEUM (RETAIL OPERATIONS IN TOWNSHIPS AND VILLAGES) RULES, 2016	PETROLEUM ACT, (SURA YA 392) Kifungu cha 5(3)	WIZARA YA NISHATI NA MADINI	1. Kuna makosa juu ya **Kifungu cha 5 (3)** cha Sheria ya Petroli ambacho kimeandikwa kuwa ndiyo kinachoanzisha Kanuni hii, kimsingi Kifungu hiki kinataja tu majukumu ya Waziri pasipo kuanisha Mamlaka ya kuanzisha Kanuni hizi.	Waziri atoe ufafanuzi	Kanuni hizi ziliandaliwa na kupelekwa kwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuchapishwa kwenye Gazeti la Serikali wakati Sheria ya Petroli ya Mwaka 2008 bado inatumika. Kwa mujibu wa Sheria ya Mwaka 2008, kifungu kilichokuwa kinatoa madaraka kwa EWURA kupitisha Kanuni kilikuwa ni kifungu cha 5 (3). Kabla Kanuni hizo hazijatangazwa kwenye Gazeti la Serikali, ndio Sheria Mpya ya Mafuta ya Petroli ya Mwaka 2015 ikaanza kutumika. Kwa sasa EWURA inafanya marekebisho kwenye Kanuni husika kwa kuweka kifungu sahihi ambacho ni 259 (1) cha Sheria ya Mafuta ya Petroli ya Mwaka 2015.

S/N	NAMBA YA TANGAZO LA SERIKALI (GN NUMBER)	JINA LA SHERIA NDOGO (NAME)	SHERIA INAYOTOA MADARAKA (ENABLING PROVISION)	MAMLAKA INAYOHUSIKA	YATOKANAYO NA UCHAMBUZI (OBSERVATIONS)	MAONI NA MAPENDEKEZO (RECOMMENDATIONS)	MAJIBU YA SERIKALI
					2. Katika **Kanuni ya 11 (3)** adhabu ya faini ya shilingi milioni tano (5) kwa kosa la kuendesha shughuli bila kibali *(offence of conducting a regulated activity without a licence)* inaweza kuonekana kuwa ni ndogo kulingana na asili ya shughuli yenyewe. Kiwango cha faini kikokotolewe kulingana na faida ya kifedha aliyopata wakati akifanya shughuli bila leseni AU hasara aliyoisababishia Serikali kwa kufanya shughuli bila leseni.	Waziri atoe ufafanuzi kwa kuzingatia ushauri wa Kamati	Kwa kawaida adhabu kwenye kanuni zinaendana na adhabu zilivyowekwa kwenye sheria mama. Kwa mujibu wa Sheria ya Mafuta iliyofutwa ya mwaka 2008, adhabu ya faini ni Shilingi milioni tano. Kwa sasa adhabu hiyo imeongezwa na kuwa kiasi kisichopungua Shilingi milioni 20 (angalia kifungu cha 131 (4) cha Sheria hiyo). EWURA imeandaa rasimu ya mabadiliko ya kanuni husika ili ziendane na Sheria ya Mafuta ya Mwaka, 2015. Inategemewa kuwa kabla ya tarehe 31 Desemba, 2016 rasimu hiyo itakuwa imekamilika na kuchapishwa kwenye Gazeti la Serikali. EWURA itazingatia ushauri na maelekezo ya Kamati wakati wa kufanya marekebisho kwenye Kanuni husika.

S/N	NAMBA YA TANGAZO LA SERIKALI (GN NUMBER)	JINA LA SHERIA NDOGO (NAME)	SHERIA INAYOTOA MADARAKA (ENABLING PROVISION)	MAMLAKA INAYOHUSIKA	YATOKANAYO NA UCHAMBUZI (OBSERVATIONS)	MAONI NA MAPENDEKEZO (RECOMMENDATIONS)	MAJIBU YA SERIKALI
					3. **Kanuni ya 17** iweke ukomo wa muda ambapo Mamlaka itapaswa kutoa majibu iwapo mwombaji wa leseni amepewa leseni au amenyimwa leseni ili kuondoa urasimu.	Kanuni ifanyiwe marekebisho	Kwa mujibu wa kifungu cha 133 cha Sheria ya Mafuta ya Mwaka 2015, EWURA inatakiwa kutoa au kunyima leseni kwa mwombaji ndani ya siku 60 tangu kupokelewa kwa maombi kamili ya leseni. Muda huu pia utawekwa kwenye mabadiliko ya Kanuni ambayo yanayofanyiwa kazi na EWURA.
					4. Katika Kanuni ya 23, maneno "*serious violation*" yanapaswa kutolewa ufafanuzi kujua kiwango cha kosa. Aidha Kanuni iweke masharti ambapo Mamlaka inaweza kuondoa vikwazo kwa mwenye leseni aliyefungiwa endapo atarekebisha makosa yake *(a ban lift-up after compliance)*.	Kanuni ifanyiwe marekebisho	EWURA inaandaa rasimu ya mabadiliko ya kanuni husika kwa kubainisha makosa ambayo yatachukuliwa kuwa ni "*serious violation*". Rasimu hiyo itakamilika na kuchapishwa kwenye Gazeti la Serikali kabla ya tarehe 31 Desemba 2016. Katika mabadiliko ya kanuni itazingatia kuondoa vikwazo kwa mwenye leseni aliyerekebisha makosa (*lifting the suspension of a licence*) Kanuni hizi zilipitishwa kipindi ambacho Sheria ya Petroli ya Mwaka, 2008 haikuwa imeweka wajibu wa kuanzishwa (*Decommssioning Fund*).

S/N	NAMBA YA TANGAZO LA SERIKALI (GN NUMBER)	JINA LA SHERIA NDOGO (NAME)	SHERIA INAYOTOA MADARAKA (ENABLING PROVISION)	MAMLAKA INAYOHUSIKA	YATOKANAYO NA UCHAMBUZI (OBSERVATIONS)	MAONI NA MAPENDEKEZO (RECOMMENDATIONS)	MAJIBU YA SERIKALI
							Sheria ya Petroli ya Mwaka, 2015 kifungu cha 197 kuna wajibu wa kuanzishwa kwa Decommisioning Fund ambayo wenye leseni watatakiwa kuchangia katika kipindi cha leseni zao. EWURA kwa kushirikiana na mamlaka nyingine inaandaa Kanuni za kusimamia mfuko huu. Kanuni zitakuwa tayari ifikapo tarehe 31 Machi, 2017. Kifungu kinachoipa mamlaka EWURA kutunga Kanuni ndani ya Sheria ya Mafuta ya Petroli ya Mwaka 2015 ni kifungu cha 259 (1). Viwango vya ada ya leseni pamoja na ada mbalimbali kwenye Sekta Ndogo ya Mafuta vimewekwa kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni za Ada na Tozo mbalimbali "*the Petroleum (Licensing Fees) Rules*, 2016". Kanuni hizo zimeainisha viwango mbalimbali vya ada za leseni zinazolipwa katika Sekta Ndogo ya Mafuta kwa mkondo wa kati na chini. Katika Kanuni zinazoandaliwa na EWURA

S/N	NAMBA YA TANGAZO LA SERIKALI (GN NUMBER)	JINA LA SHERIA NDOGO (NAME)	SHERIA INAYOTOA MADARAKA (ENABLING PROVISION)	MAMLAKA INAYOHUSIKA	YATOKANAYO NA UCHAMBUZI (OBSERVATIONS)	MAONI NA MAPENDEKEZO (RECOMMENDATIONS)	MAJIBU YA SERIKALI
							kutawekwa masharti na mambo ya kuzingatia kwa wakaguzi wa EWURA pale wanapokuwa wanafanya ukaguzi kwa lengo la kuondoa uwezekano wa matumizi mabaya ya madaraka. EWURA pia inaandaa "Mwongozo wa Ukaguzi" (Inspection Manual) inayoelezea utaratibu mzima wa kufanya ukaguzi.
					5. **Kanuni ya 45** na **46** zinazungumzia utaratibu ambapo mwenye leseni atalipa gharama za *decommission* na *site restoration*. Utaratibu huu unaweza kumuongezea gharama endapo mwenye leseni atafunga biashara kutokana na sababu za kufilisika. Kanuni zinaweza kuweka utaratibu ambapo kutakuwa na mfuko maalum ambao wenye leseni watakuwa wanachangia pesa mara kwa mara ili mwenye leseni atakayehitajika kufanya *decommission* na *site restoration* asiingie gharama kubwa wakati wa kufunga biashara husika.	Waziri atoe ufafanuzi kwa kuzingatia ushauri wa Kamati	Kanuni itafanyiwa marekebisho kwa kuzingatia ushauri wa Kamati na masharti ya Sheria Mama.

S/N	NAMBA YA TANGAZO LA SERIKALI (GN NUMBER)	JINA LA SHERIA NDOGO (NAME)	SHERIA INAYOTOA MADARAKA (ENABLING PROVISION)	MAMLAKA INAYOHUSIKA	YATOKANAYO NA UCHAMBUZI (OBSERVATIONS)	MAONI NA MAPENDEKEZO (RECOMMENDATIONS)	MAJIBU YA SERIKALI
					6. **Kanuni ya 5 na 15**, hazitaji kiwango cha ada ya maombi (Application fee) ya ujenzi wa Kituo cha kuuzia Mafuta inayotakiwa alipe muombaji (kanuni ya 5) pamoja na ada ya maombi ya leseni (kanuni ya 15). Kanuni hizi zinajenga mazingira ya rushwa au ada zisizokuwa na uhalisia wowote.	Waziri atoe ufafanuzi kwa kuzingatia ushauri wa Kamati	Kanuni itafanyiwa marekebisho kwa kuzingatia ushauri wa Kamati na masharti ya Sheria Mama
					7. **Kanuni ya 52** inaainisha vitendo ambavyo mtoa huduma za mafuta hataruhusiwi kumfanyia Mkaguzi kutoka EWURA sambamba na adhabu zake pale ambapo atakiuka utaratibu. Hata hivyo, kanuni haitoi wajibu kwa Mkaguzi wa EWURA wala kuanisha taratibu za kuzingatiwa na Mkaguzi wakati wa zoezi za ukaguzi na adhabu stahiki pale ambapo atakiuka kanuni/taratibu za Utumishi/ukaguzi	Waziri atoe ufafanuzi kwa kuzingatia ushauri wa Kamati	Kanuni itafanyiwa marekebisho kwa kuzingatia ushauri wa Kamati na masharti ya Sheria Mama

S/N	NAMBA YA TANGAZO LA SERIKALI (GN NUMBER)	JINA LA SHERIA NDOGO (NAME)	SHERIA INAYOTOA MADARAKA (ENABLING PROVISION)	MAMLAKA INAYOHUSIKA	YATOKANAYO NA UCHAMBUZI (OBSERVATIONS)	MAONI NA MAPENDEKEZO (RECOMMENDATIONS)	MAJIBU YA SERIKALI
70.	**GN Na. 175** 13 Mei, 2016	THE ELECTRICITY (SUPPLY SERVICES) RULES, 2016	THE ELECTRICITY ACT, (SURA YA 131) Kifungu cha 45	WIZARA YA NISHATI NA MADINI	1. **Kanuni ya 5** inaweka adhabu ya faini ya shilingi milioni kumi (10) bila kuweka *flexibility* ya vyombo vya utoaji haki kutoa adhabu.	Waziri atoe ufafanuzi	Kwa mujibu wa kifungu cha 8 (5) cha Sheria ya Umeme, adhabu kubwa inayoweza kutolewa kwa mtu anayetoa huduma ya kusambaza umeme bila ya leseni si zaidi ya Shilingi milioni 10, hivyo sheria inatoa *flexibility*. EWURA itafanyia kazi marekebisho ya Kanuni husika kwa lengo la kuhakikisha *flexibility* iliyoko kwenye Sheria ya Umeme ya Mwaka 2008 inakuwapo pia kwenye Kanuni husika.

S/N	NAMBA YA TANGAZO LA SERIKALI (GN NUMBER)	JINA LA SHERIA NDOGO (NAME)	SHERIA INAYOTOA MADARAKA (ENABLING PROVISION)	MAMLAKA INAYOHUSIKA	YATOKANAYO NA UCHAMBUZI (OBSERVATIONS)	MAONI NA MAPENDEKEZO (RECOMMENDATIONS)	MAJIBU YA SERIKALI
					2. **Kanuni ya 24 (2)** inamtaka mtu aliyepata madhara kutokana na kusambaziwa umeme, kupeleka malalamiko yake Msambazaji umeme mwenye leseni alyemsambazia kwa usuluhishi *(Amicable Settlement)*. Kimsingi Kanuni haijaweka bayana ni ndani ya muda gaini shauri hili linapaswa kuwasilishwa kwa usuluhishi/makubaliano.	Waziri atoe ufafanuzi	Kanuni za kutatua malalamiko ya watumia huduma (EWURA (*Complaints Handling Procedure) Rules*, GN No. 10/2013 zinaanisha utaratibu mzima wa kutatua malalamiko ya watumia huduma. Kanuni hizi zinaelekeza namna na muda wa kuleta malalamiko ikiwa ni pamoja na kuweka ukomo wa muda wa kuwasilisha malalamiko (*limitation periods*). Muda wa kuwasilisha malalamiko unategemea na aina ya malalamiko husika. Kwa mfano: • Malalamiko ya bili ya umeme yanapaswa kuwasilishwa ndani ya miezi 12; • Malalamiko ya kukatiwa umeme, miezi 12; na • Huduma mbovu ya umeme, miezi 24. Hata hivyo, EWURA itaweka kwenye Kanuni husika wajibu, kwa EWURA, kumaliza kusikiliza na kutoa uamuzi kwenye malalamiko yanayoletwa kwake.

S/N	NAMBA YA TANGAZO LA SERIKALI (GN NUMBER)	JINA LA SHERIA NDOGO (NAME)	SHERIA INAYOTOA MADARAKA (ENABLING PROVISION)	MAMLAKA INAYOHUSIKA	YATOKANAYO NA UCHAMBUZI (OBSERVATIONS)	MAONI NA MAPENDEKEZO (RECOMMENDATIONS)	MAJIBU YA SERIKALI
					3. **Kanuni ya 24 (3)** inaelekeza mtu ambaye amedhurika iwapo hajaridhika na makubaliano kati yake na Msambazaji umeme mwenye wa leseni atapaswa kuwasilisha malalamiko yake EWURA. Kimsingi Kanuni hii pia haielezi ni ndani ya muda upi mgogoro huo unapaswa kuwasilishwa kwa EWURA sambamba na hatua na nyaraka zinatotakiwa kutumika kuwasilisha mgogoro huo.	Waziri atoe ufafanuzi	Kanuni za kutatua malalamiko ya watumia huduma (EWURA (*Complaints Handling Procedure) Rules*. GN No. 10/2013 zinaanisha utaratibu mzima wa kutatua malalamiko ya watumia huduma. Kanuni hizi zinaelekeza namna na muda wa kuleta malalamiko ikiwa ni pamoja na kuweka ukomo wa muda wa kulalamika (*limitation periods*). Muda wa kuwasilisha malalamiko unategemea na aina ya malalamiko husika. Kwa mfano: • Malalamiko ya bili ya umeme yanapaswa kufanyika ndani ya miezi 12; • Malalamiko ya kukatiwa umeme, miezi 12; na • Huduma mbovu ya umeme, miezi 24. Hata hivyo, EWURA itaweka kwenye Kanuni husika wajibu, kwa EWURA, kumaliza kusikiliza na kutoa uamuzi kwenye malalamiko yanayoletwa kwake.

S/N	NAMBA YA TANGAZO LA SERIKALI (GN NUMBER)	JINA LA SHERIA NDOGO (NAME)	SHERIA INAYOTOA MADARAKA (ENABLING PROVISION)	MAMLAKA INAYOHUSIKA	YATOKANAYO NA UCHAMBUZI (OBSERVATIONS)	MAONI NA MAPENDEKEZO (RECOMMENDATIONS)	MAJIBU YA SERIKALI
71.	**GN Na. 177** 13/05/2016	THE DISTRICT LAND AND HOUSING TRIBUNALS CODE OF CONDUCT, 2016	THE LAND DISPUTE COURTS ACT (CAP. 216) Section 56 (2)(j)	WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI	1. Jina la Sheria Ndogo linapaswa kubadilika kuainisha umaalum/umahususi wa Sheria Ndogo hii kwa Mwenendo wa Wenyeviti wa Mabaraza ***(The District Land and Housing Tribunals (Chairmen) Code of Conduct)*** ili kuakisi masharti yanayopatikana katika **Kanuni ya 1**	Kanuni ifanyiwe marekebisho	Kanuni itafanyiwa marekebisho
					2. **Kanuni ya 7 (e)** haijaweka ukomo wa muda ambao wenyeviti waliomaliza muda wao wanapaswa kukabidhi mashauri ambayo hayajatolewa uamuzi/hukumu.	Kanuni ifanyiwe marekebisho	Kanuni itafanyiwa marekebisho
					3. **Kanuni ya 9** inaweka utaratibu wa Mwenyekiti kujiuzulu. Hata hivyo, masharti ya kanuni hii yanaweka utaratibu ambao Mwenyekiti anahusika katika mwenendo huo kwa kupokea malalamiko, kuamua iwapo malalamiko dhidi yake yanaweza kushughulikiwa na Baraza au vinginevyo. Masharti haya yanaweza kutafsirika kuwa mlalamikiwa anakuwa hakimu wa kesi yake.	Kanuni ifanyiwe marekebisho	Kanuni itafanyiwa marekebisho
72.	**GN Na. 198** 17/06/2016	THE SURFACE AND MARINE TRANSPORT REGULATORY AUTHORITY (DRY PORT) REGULATIONS, 2016	THE SURFACE AND MARINE TRANSPORT REGULATORY AUTHORITY ACT, (SURA YA 413) Kifungu cha 39	WIZARA YA UCHUKUZI, UJENZI NA MAWASILIANO	**Kanuni ya 25** inaweka utaratibu wa kulipa faini kwa makosa mbalimbali, ambayo yameainishwa chini ya Kanuni hii. Kanuni inaelekeza mkosaji atapaswa kulipa faini ya kiasi kisichopungua shilingi milioni mbili na isiyozidi shilingi milioni tatu (3). Aidha, adhabu ni ndogo na zinaua msingi dhumuni la adhabu kwani haitazuia makosa kama vile kufanya biashara ya	Kanuni ifanyiwe marekebisho	NIL

S/N	NAMBA YA TANGAZO LA SERIKALI (GN NUMBER)	JINA LA SHERIA NDOGO (NAME)	SHERIA INAYOTOA MADARAKA (ENABLING PROVISION)	MAMLAKA INAYOHUSIKA	YATOKANAYO NA UCHAMBUZI (OBSERVATIONS)	MAONI NA MAPENDEKEZO (RECOMMENDATIONS)	MAJIBU YA SERIKALI
					bandari kavu pasipo na leseni. Pia haina uhalisia kutokana na madhara yakiuchumi yanayosababishwa na ukiukwaji wa taratibu zilizotajwa katika Kanuni hii.		
73.	**GN Na. 212** 24/06/2016	THE VALUE ADDED TAX (GENERAL) (AMENDMENT) REGULATIONS, 2016	THE VALUE ADDED TAX ACT (CAP. 148) Kifungu cha 29 (2), 84 and 94	WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO	**Kanuni ya 2** inafanya marekebisho ya Kanuni inayoitwa *The Value Added Tax (General) Amendment Regulations, 2015* kwa kufuta neno *"not"* katika Kanuni ya 35 (4) mwanzoni mwa aya (b). Kufutwa kwa neno hilo, kunampa haki mtoa bima *(insurer)* ya kudai *input tax credit* kutokana na gharama za mauzo na uendeshaji kwa malipo aliyoyafanya kwa mteja *(insured person)* chini ya mkataba wa bima. Awali mtoa bima hakuwa na haki hii katika Kanuni zinazofanyiwa marekebisho. Hata hivyo, Kanuni ya 35 (3) (b) bado inamyima haki the *insured person* ya kudai *input tax credit* chini ya mkataba wa bima.	Waziri atoe ufafanuzi	Kamati ilikubaliana na maelezo ya Wizara kwamba kodi ya ongezeko la thamanini kodi ya mlaji, hivyo mtu yeyote anayetumia bidhaa huduma au kununua nyumba mpya kwa ajili ya shughuli za uzalishaji ndiye pekaa anayestahili kudai kodi ya VAT aliyolipa kwa mujibu wa Kifungu cha 68(1)(a) cha Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani.
74.	**GN Na. 224** 22/07/2016	THE CYBER CRIMES (GENERAL) REGULATIONS, 2016	THE CYBERCRIMES ACT, (SURA YA 443) Kifungu cha 51	WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO	**Kanuni ya 6** inazungumzia utaratibu ambao mtu yeyote anaweza kumpa taarifa mtoa huduma *(service provider)* ili afute *any material* inayokiuka Sheria katika *(filing a take - down notification)* kutokana na Kifungu cha 45 cha Sheria Mama. Masharti ya Sheria Mama yamebainisha wazi mazingira ambapo mtoa huduma atashindwa kufuta material husika, mtu anayetoa taarifa anaweza kuitaarifu mamlaka husika *(competent authority)* ili iweze kuingilia kati. Ni vema, katika fomu	Kanuni ifanyiwe marekebisho	NIL

S/N	NAMBA YA TANGAZO LA SERIKALI (GN NUMBER)	JINA LA SHERIA NDOGO (NAME)	SHERIA INAYOTOA MADARAKA (ENABLING PROVISION)	MAMLAKA INAYOHUSIKA	YATOKANAYO NA UCHAMBUZI (OBSERVATIONS)	MAONI NA MAPENDEKEZO (RECOMMENDATIONS)	MAJIBU YA SERIKALI
					inayopatikana katika jedwali la Sheria Ndogo hii pawepo na sehemu ambayo nakala ya taarifa hiyo ipewe mamlaka husika ili kurahisisha rejea.		